# Mwongozo wa Mwalimu wa Kufundishia Elimu ya Awali

Taasisi ya Elimu Tanzania

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2019

ISBN 978  - 9976 - 61- 906 - 5

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam

Simu: + 255 22 277 3005 / + 255 22 277 1358
Nukushi: + 255 22 277 4420
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 2 9/18/19 4:59 PM

# Azimio

Mwongozo wa Mwalimu wa Kufundishia Elimu ya Awali umethibitishwa kwa matumizi katika Shule za Awali Tanzania.

Umethibitishwa na: Dkt Lyabwene M. Mtahabwa

Saini:______________________

Tarehe: 18 Septemba, 2019

Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
S.L.P 10
Dodoma

Simu: + 255 222 110150

+ 255 222 110179

+ 255 222 110146

Nukushi: + 255 222 11327



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 3 9/18/19 4:59 PM

## Yaliyomo

**Shukurani** .......... v

**Utangulizi** .......... vi

**Vifupisho** .......... viii

**Sura ya Kwanza**
Uchambuzi wa mtaala .......... 1

**Sura ya Pili**
Ujifunzaji na ufundishaji wa mtoto wa Elimu ya Awali .......... 4

**Sura ya Tatu**
Upimaji na tathmnini ya maendeleo ya mtoto katika Elimu ya Awali .......... 10

**Sura ya Nne**
Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Awali .......... 16

**Rejea** .......... 141

**Viambatisho** .......... 142

## Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa mwongozo huu.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu kutoka Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DUCE), Vyuo vya Ualimu vya Singa chini, Mhonda na Montessori-Msimbazi pamoja na Shule za Awali Chang'ombe, Tusiime na Mwere B.

Pia, TET inatoa shukurani kwa walimu wote walioshiriki katika ujaribishaji wa mwongozo huu. Vilevile, TET inatoa shukurani za pekee kwa Idara ya Uthibiti Ubora, Shirika la Kimataifa la Kuhudumia watoto "UNICEF" Tanzania pamoja na shirika la Right to Play (RTP) kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kuchapisha mwongozo huu.

Aidha, Taasisi ya Elimu Tanzania inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) kwa kutoa rasilimali fedha iliyofanikisha uandishi wa mwongozo huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

# Utangulizi

## Usuli

Mwalimu, ni muhimu kuelewa kuwa Elimu ya Awali inatolewa kwa watoto kwa lengo la kuwakuza kiakili, kimwili, kijamii na kihisia. Mtoto wa Elimu ya Awali anapaswa kujenga umahiri ambao atautumia katika maisha yake ya kila siku. Kwa kuzingatia hili, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) imeandaa Mtaala na Muhtasari wa Elimu ya Awali ambao unalenga kuwajengea watoto umahiri uliokusudiwa. Sanjari na Mtaala na Muhtasari, TET pia imeandaa Mwongozo wa Mwalimu wa Kufundishia Elimu ya Awali ambao utautumia katika kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji. Mwongozo huu umebainisha umahiri anaostahili kujenga mtoto wa Elimu ya Awali kupitia shughuli mbalimbali ambazo atazitenda. Pamoja na Mwongozo huu, mwalimu unatakiwa kuzingatia maudhui yote ya Mtaala wa Elimu ya Awali na kufanya maandalizi yanayostahili, ili kuleta ufanisi katika ufundishaji wako na ujifunzaji wa watoto.

## Lengo la mwongozo

Lengo kuu la kuandaa mwongozo huu ni kukusaidia wewe mwalimu kutafsiri na kutekeleza Mtaala wa Elimu ya Awali ambao unasisitiza ujenzi wa umahiri. Mwongozo huu umebainisha mchakato wa ujenzi wa umahiri kupitia shughuli mbalimbali ambazo zitatendwa na mtoto. Mwalimu unapaswa kumwezesha mtoto kujenga umahiri husika kupitia shughuli zilizobainishwa, mbinu, zana stahiki za kufundishia na kujifunzia, pamoja na kupima maendeleo ya mtoto hatua kwa hatua.

## Umuhimu wa mwongozo

Mwalimu, mwongozo huu ni muhimu kwako kwa kuwa utakusaidia kuboresha mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji. Mwongozo umebainisha shughuli za kutendwa na mtoto, ambazo zitamwezesha kujenga umahiri husika. Mwongozo huu pia umeelezea kwa kifupi kuhusu mtaala unaojenga umahiri na unasisitiza ujifunzaji na ufundishaji wa masuala mtambuka. Masuala hayo ni pamoja na stadi za maisha, mazingira, jinsia, Virusi Vya Ukimwi (VVU) na Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI). Mwalimu, unapaswa kuusoma na kuuelewa mwongozo huu ili uweze kutekeleza Mtaala wa Elimu ya Awali kwa ufanisi.


Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 6 9/18/19 4:59 PM

**Muundo wa mwongozo**

Mwongozo huu umegawanyika katika sura nne. Sura mbili za mwanzo zinatoa maelezo mafupi kuhusu uchambuzi wa mtaala na ujifunzaji na ufundishaji katika Elimu ya Awali. Sura ya tatu inaeleza kuhusu upimaji wa maendeleo ya mtoto wa Elimu ya Awali. Sura ya nne inatoa maelezo kuhusu maandalizi ya ufundishaji na namna ya kuwezesha ujenzi wa umahiri ambao mtoto wa Elimu ya Awali anastahili kuujenga. Mwalimu, unashauriwa kupitia sura mbili za mwanzo ili kupata uelewa wa kutosha kabla ya kuanza mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji wa shughuli zilizobainishwa ili kujenga umahiri uliokusudiwa.

**Walengwa wa mwongozo**

Walengwa wakuu wa mwongozo huu ni walimu wa Elimu ya Awali. Hata hivyo, mwongozo unaweza kutumiwa na wadau wengine wa elimu kama vile walimu wakuu, wathibiti ubora wa shule, wamiliki wa shule, kamati za shule, wakufunzi, wazazi/walezi na jamii.

**Matumizi ya mwongozo**

Wakati wa kufanya maandalizi ya ujifunzaji na ufundishaji, mwongozo huu utatumika sambamba na Muhtasari wa Elimu ya Awali. Mwalimu, inakupasa kuupitia mwongozo huu kwa makini ili kubaini umahiri anaotakiwa kuujenga mtoto na kufundisha ipasavyo.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 7 9/18/19 4:59 PM

# Vifupisho

| | | |
|---|---|---|
| RTP | : | Right To Play |
| TEHAMA | : | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | : | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| UKIMWI | : | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UNICEF | : | United Nations Children's Education Fund |
| VVU | : | Virusi Vya Ukimwi |
| WyEST | : | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 8 9/18/19 4:59 PM

# Sura ya Kwanza

## Uchambuzi wa mtaala

Mwalimu, karibu katika sura ya kwanza ya Mwongozo wa mwalimu wa kufundishia Elimu ya Awali. Katika sura hii utajifunza dhana ya mtaala unaojenga umahiri na jinsi ya kuchambua mtaala wa Elimu ya Awali na vifaa vyake. Vilevile, utajifunza uhusiano uliopo kati ya mtaala na vifaa vyake, ili kuweza kuutekeleza ipasavyo.

**Umahiri unaotarajiwa kujengwa**

Baada ya kusoma sura hii, mwalimu utaweza:

i. kueleza dhana ya mtaala unaolenga kujenga umahiri;
ii. kuchambua vifaa vya mtaala; na
iii. kueleza uhusiano kati ya mtaala na vifaa vyake.

### 1.1 Dhana ya mtaala unaolenga kujenga umahiri

Mtaala unaolenga kujenga umahiri ni ule unaomwezesha mtoto kujenga umahiri kupitia vitendo mbalimbali vya ujifunzaji. Mtaala huu umeandaliwa kwa kuzingatia umahiri anaostahili kuujenga mtoto katika nyanja zote za ukuaji na ujifunzaji kiakili, kimwili, kijamii na kihisia. Mtaala huu, utamwezesha mtoto kumudu maisha yake ya kila siku pamoja na kumwandaa kwa ngazi ya Elimu ya Msingi.

*Mwalimu, unafikiri mtaala unaozingatia ujenzi wa umahiri una sifa gani?* Pamoja na majibu yako, ni muhimu kutambua kwamba mtaala unaolenga kujenga umahiri una sifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujifunzaji unaolenga utendaji, kuhusisha ujifunzaji na maisha ya kila siku na kuchochea ubunifu pamoja na udadisi. Vilevile, mtaala huu una sifa ya kumshirikisha mtoto kama mtendaji mkuu katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji. Kazi yako ni kumwongoza mtoto kufanya shughuli mbalimbali ambazo zitamwezesha kujenga umahiri uliotarajiwa. Kwa kuwa umahiri unajengwa kupitia shughuli anazotenda mtoto, mwalimu unapaswa kutumia mbinu na zana stahiki za kufundishia na kujifunzia. Matumizi ya mbinu na zana hizo yataamsha ari ya mtoto kujifunza na kumjengea tabia ya udadisi itakayomsaidia kujenga dhana mbalimbali kuhusu kitu anachojifunza.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 1 9/18/19 4:59 PM

## 1.2 Vifaa vya mtaala

Mwalimu, unatakiwa kutumia vifaa mbalimbali ili kutekeleza mtaala unaolenga kujenga umahiri. *Hebu jiulize, ni vifaa gani muhimu unatakiwa kuwa navyo ili uweze kutekeleza mtaala kikamilifu? Je, kuna uhusiano gani kati ya vifaa hivyo na mtaala?* Bila shaka baadhi ya vifaa ambavyo utataja ni pamoja na Muhtasari, Kitabu cha kiada na Mwongozo wa mwalimu wa kufundishia Elimu ya Awali. Vifaa vyote hivi vitakusaidia katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji ili kumwezesha mtoto kujenga umahiri uliokusudiwa. Yafuatayo ni maelezo ya mchanganuo wa vifaa hivyo:

### 1.2.1 Muhtasari

Mwalimu, kumbuka kuwa muhtasari ndio unaobainisha mambo yote unayotakiwa kuwafundisha watoto katika muda maalum. Muhtasari wa Elimu ya Awali umeandaliwa ili kuwawezesha watoto kujenga umahiri uliokusudiwa. Muhtasari huu umeundwa na vipengele vitano ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mtoto, viashiria pendekezwa vya utendaji na idadi ya vipindi.

### 1.2.2 Mwongozo wa mwalimu

Mwongozo wa mwalimu ni kifaa kinachorahisisha tendo la ujifunzaji na ufundishaji ndani na nje ya darasa. Mwongozo huu utatumika sambamba na muhtasari pamoja na kitabu cha kiada. Mwalimu unatakiwa kuzingatia mwongozo huu katika kuwezesha shughuli mbalimbali za kutendwa na mtoto. Vilevile, mwongozo huu umeainisha baadhi ya nyimbo na michezo ambayo itakurahisishia kutekeleza shughuli husika kwa njia ya michezo. Unapaswa kukumbuka kwamba watoto hujifunza kwa njia ya michezo.

Baadhi ya faida za kujifunza kupitia michezo ni kama ifuatavyo:

i. kumkuza mtoto katika nyanja zote (kiakili, kimwili, kijamii na kihisia);
ii. kujenga misuli mikubwa na midogo;
iii. kuleta furaha;
iv. kujenga uhusiano;
v. kujenga stadi za utatuzi wa matatizo;
vi. kujifunza kufuata kanuni na taratibu za michezo;
vii. kujenga ubunifu na kukuza udadisi; na
viii. kujifunza dhana mbalimbali kwa wepesi.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 2 9/18/19 4:59 PM

### 1.2.3 Kitabu cha kiada

Hiki ni kitabu kilichoandaliwa kwa kuzingatia umahiri uliopo katika muhtasari. *Je, mwalimu unafikiri kitabu hiki kina umuhimu gani?* Bila shaka utaeleza kuwa kitabu hiki ni muhimu sana katika ufundishaji na kinamsaidia mtoto kupanua maarifa aliyoyapata wakati wa utendaji wa shughuli mbalimbali darasani. Vilevile, kitabu hiki kinamsaidia mtoto kuelewa dhana vizuri na kwa urahisi zaidi. Kitabu cha kiada kinapaswa kuwa na michoro au picha zaidi kuliko maandishi, kwa kuwa watoto bado hawajaweza kusoma maandishi. Baadhi ya sifa za kitabu cha kiada ni pamoja na kuwa na picha kubwa zenye rangi za kuvutia zinazowakilisha dhana moja. Vilevile, kitabu hiki kina maandishi ya chapa yanayoonekana kwa urahisi, jalada imara na la kuvutia na kurasa chache. Kitabu hiki pia kimeandikwa kwa kuzingatia umri na uwezo wa watoto.

Katika kutekeleza mtaala huu, kuna vitabu sita (6) vya kiada ambavyo vimeandaliwa kwa kuzingatia umahiri anaopaswa kujengwa kwa mtoto wa Elimu ya Awali. Vitabu hivyo ni:

i. Michezo na Sanaa
ii. Kuhesabu
iii. Kushirikiana
iv. Kuwasiliana
v. Kutunza Afya
vi. Kutunza Mazingira

Vitabu hivi vina picha za baadhi ya shughuli katika umahiri husika. Hata hivyo, kuna baadhi ya picha ambazo mwalimu unaweza kuzitumia kufundishia zaidi ya shughuli moja. Mwalimu unapaswa kuwa mnyumbufu na mbunifu kwa kutafuta picha nyingine ambazo zitakusaidia kufundisha shughuli mbalimbali.

Vilevile, Taasisi ya Elimu Tanzania imeandaa vitabu vya hadithi vitakavyomwezesha mtoto kujenga umahiri ulioainishwa katika muhtasari wa Elimu ya Awali.

## 1.3 Uhusiano kati ya mtaala na vifaa vyake

Mwalimu, baada ya kupitia vipengele vinavyoelezea vifaa vya mtaala utagundua kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya mtaala na vifaa vyake. Mtaala wa Elimu ya Awali umeandaliwa kwa kuzingatia falsafa ya nchi katika elimu na Sera ya elimu na mafunzo na ambavyo vinasisitiza elimu ya kujitegemea. Maudhui ya muhtasari yanatokana na mtaala. Mwongozo wa mwalimu na vitabu vya kiada vimeandaliwa kwa kuzingatia muhtasari. Hivyo, ufanisi wa utekelezaji wa mtaala utategemea jinsi utakavyohusianisha mtaala na vifaa vyake.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 3 9/18/19 4:59 PM

# Sura ya Pili

## Ujifunzaji na ufundishaji wa mtoto wa Elimu ya Awali

Mwalimu, karibu katika sura ya pili ya mwongozo. Katika sura hii utajifunza dhana mbalimbali kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa mtoto wa Elimu ya Awali. Dhana hizi ni pamoja na ujifunzaji na ufundishaji, mbinu na zana stahiki za kufundishia na kujifunzia katika Elimu ya Awali, Elimu jumuishi na taratibu za kufuata katika kutekeleza ratiba ya kila siku.

**Umahiri unaotarajiwa kujengwa**

Baada ya kusoma sura hii, mwalimu utaweza:

i. kueleza dhana ya ujifunzaji na ufundishaji wa mtoto;
ii. kubainisha mbinu stahiki za kufundishia;
iii. kubainisha zana stahiki za kufundishia na kujifunzia;
iv. kuzingatia elimu jumuishi katika ufundishaji wako; na
v. kutekeleza ratiba ya kila siku ipasavyo.

### 2.1 Dhana ya ujifunzaji na ufundishaji

Mwongozo huu umejikita zaidi katika kutoa maelezo ya namna ujifunzaji na ufundishaji unavyotakiwa kufanyika katika Elimu ya Awali. Maelezo haya yanamsaidia mwalimu kumwezesha mtoto kujenga umahiri uliokusudiwa. Kwa mujibu wa Mtaala na Muhtasari wa Elimu ya Awali wa mwaka 2016, ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Awali unapaswa kusisitiza ujenzi wa umahiri ambao unamlenga mtoto kama mtendaji mkuu katika shughuli za ujifunzaji. Ufanisi wa mtoto katika kutenda shughuli hizo huchochewa na uchangamshi wa awali unaomwezesha mtoto kuchunguza, kudadisi na kuwa mbunifu. Ujenzi wa umahiri kwa mtoto unategemea uzingatiwaji wa misingi ya ujifunzaji na ufundishaji katika Elimu ya Awali. Misingi hiyo ni pamoja na:

i. Kutumia mtaala unaosisitiza michezo kama njia ya kufundishia na kujifunzia;
ii. Maendeleo katika ukuaji na ujifunzaji wa mtoto vinahusiana;
iii. Kasi ya ujifunzaji hutofautiana kati ya mtoto mmoja na mwingine;
iv. Maendeleo ya mtoto na ujifunzaji wake vinategemea ushirikiano wa mwalimu, familia na jamii inayomzunguka;
v. Kuandaa mazingira rafiki ya ujifunzaji na ufundishaji kwa kutumia mbinu stahiki, zana au vifaa mbalimbali ili kukuza maarifa, stadi na mielekeo;



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 4 9/18/19 4:59 PM

vi. Kukuza uzoefu wa awali wa mtoto katika mambo anayoyafahamu na anayoweza kuyatenda; na
vii. Kutoa fursa kwa mtoto kucheza michezo iliyoandaliwa na wanayoiandaa na kuianzisha wenyewe.

Mwalimu, unapaswa kujua kwamba watoto wanatofautiana katika mahitaji yao ya ujifunzaji. Wapo watoto wenye mahitaji maalumu katika kujifunza na unapaswa kuwabaini na kuwasaidia ili waweze kujifunza na kujenga umahiri uliokusudiwa. Unaweza kuwabaini kwa njia zifuatazo:

i. kufanya upimaji gunduzi;
ii. kuchunguza mwenendo wao wakati wa vitendo vya ujifunzaji na ufundishaji;
iii. kupewa taarifa na wazazi au walezi wa watoto hao;
iv. kwa kuchunguza ushiriki wa watoto katika michezo mbalimbali.

## 2.2 Mbinu za kufundishia na kujifunzia zinazojenga umahiri

Ujifunzaji na ufundishaji wa watoto wa Elimu ya Awali unatakiwa uzingatie zaidi utendaji wa mtoto. Jukumu lako kama mwalimu ni kuwaongoza, kuwaelekeza au kuwaonesha namna ya kufanya vitendo mbalimbali. Hivyo, unapaswa kutumia mbinu za ujifunzaji na ufundishaji ambazo zinawashirikisha watoto kuwa watendaji zaidi katika kujifunza. Vigezo ambavyo unapaswa kuzingatia unapochagua mbinu za kufundishia na kujifunzia ni pamoja na:

i. wastani wa umri na uwezo wa watoto;
ii. mahitaji maalumu aliyonayo mtoto katika kujifunza;
iii. ushiriki wa mtoto katika kutenda;
iv. upatikanaji wa zana za kufundishia na kujifunzia;
v. idadi ya watoto darasani; na
vi. shughuli inayotarajiwa kutendwa na mtoto.

*Mwalimu je, unafikiri ni mbinu zipi zinafaa kufundishia darasa la Elimu ya Awali?* Pamoja na majibu uliyonayo, baadhi ya mbinu zinazopendekezwa kufundishia watoto wa Elimu ya Awali ni pamoja na onesho mbinu, uchunguzi, kazi mradi, ngonjera, michezo, nyimbo, kisa mafunzo, hadithi, maigizo, mashairi ya watoto, matembezi ya galari, maswali na majibu, bungua bongo na majadiliano. Mwalimu, unashauriwa kuwa mnyumbufu katika kuchagua mbinu kulingana na mahitaji, mazingira ya watoto na hali halisi ya darasa lako kwa wakati huo.

## 2.3 Zana za kufundishia na kujifunzia

Ujifunzaji na ufundishaji wa watoto utafanikiwa zaidi iwapo mwalimu utatumia zana stahiki za kufundishia na kujifunzia. Zana hizi zinamwezesha mtoto kujenga dhana ya kitu



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 5 9/18/19 4:59 PM

anachofundishwa kwa urahisi kwa kuwa anatumia milango mingi ya fahamu. Mwalimu, unashauriwa kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia zana halisi zinazopatikana katika mazingira ya watoto. Zana za kufundishia na kujifunzia zinatakiwa kuwa na sifa mbalimbali. Sifa hizo ni pamoja na:

i. ziendane na umri na uwezo wa mtoto;
ii. ziwe salama kwa watoto;
iii. ziwavutie watoto;
iv. zilenge kujenga ubunifu na udadisi;
v. ziwe imara na za kudumu;
vi. zilenge kujenga dhana iliyokusudiwa; na
vii. ziwe kubwa na zinazoonekana vizuri.

Mwalimu, unapochagua zana za kufundishia na kujifunzia, zingatia yafuatayo:

i. upatikanaji wa zana kwa urahisi katika mazingira husika;
ii. mahitaji ya watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalumu;
iii. shughuli utakayofundisha;
iv. mbinu utakayotumia kufundisha shughuli husika;
v. idadi ya watoto darasani; na
vi. mazingira na hali halisi ya darasa.

Baadhi ya zana ambazo mwalimu unaweza kutumia kufundishia watoto wa Elimu ya Awali ni pamoja na kibao fumbo, bao, karata, dadu, domino, chati ya mchezo wa nyoka na ngazi, drafti, vihesabio na midoli, kadi za herufi, kadi za namba, kadi za picha, vipande vya mbao, kanda za video, runinga na redio.

Zana nyingine ni kama simu, michoro mbalimbali, picha, filimbi, kengele, ngoma, zeze, kinanda, viongeza sauti, vikuza maandishi, zana mguso/mkwaruzo, kamusi ya lugha ya alama, alfabeti ya lugha za alama na mashine za braille. Vifaa unavyoweza kuvitumia nje ya darasa ni pamoja na kizimba cha mchanga, bembea za aina mbalimbali, michezo telezi, mipira, matairi na kamba.

## 2.4 Kona za ujifunzaji

Mwalimu, darasa la Elimu ya Awali linapaswa kuwa na kona za ujifunzaji. Kona za ujifunzaji ni maeneo yaliyowekewa vifaa/zana mbalimbali za kujifunzia.

Kona hizo watazitumia watoto wakati wa ujifunzaji darasani au kwa muda wao wenyewe kulingana na vionjo vyao. Baadhi ya kona hizo ni kona ya Hisabati, Sayansi, Nyumbani, Sanaa, Dukani, Lugha (Kusoma na Kuandika), Michezo na Eneo la Mchanga na Maji ambayo itakuwa nje ya darasa. Hata hivyo, kati ya kona hizo, kona ya Hisabati, Lugha na Michezo ni lazima ziwepo katika kila darasa la Elimu ya Awali.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 6 9/18/19 4:59 PM

Baadhi ya zana/vifaa vinavyoweza kuwepo katika kona za ujifunzaji:

| | |
|---|---|
| **Kona ya Hisabati:** | Vibao fumbo, kadi za namba, vihesabio, vipande vya mbao, mfuko wa hisabati na kichocheo cha kuhesabu. |
| **Kona ya Sayansi:** | Mzani, picha za wanyama, mimea, vifani, sumaku, vipimo na lenzi. |
| **Kona ya Lugha:** | Vitabu vya hadithi, vifani, kadi za herufi, chati ya herufi, chati za majina, kichocheo na vikaragosi. |
| **Kona ya Sanaa:** | Ngoma, filimbi, udongo wa mfinyanzi, ukili, kamba na nyuzi. |
| **Kona ya Nyumbani:** | Vifaa vya jikoni, kitanda, meza, viatu, nguo na mikoba. |
| **Kona ya Dukani:** | Sabuni, mafuta, chupa, kibiriti, daftari na makasha. |

Zana za kufundishia na kujifunzia katika Elimu ya Awali zinaweza kupatikana kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutengeneza, kununua, kufaragua na kukusanya makunzi yanayopatikana katika mazingira husika. Mwalimu, unapaswa kuwashirikisha watoto na wazazi katika kuaandaa na kutengeneza zana. Vilevile ni muhimu kuandaa zana za kutosha katika kila kona ya ujifunzaji. Aidha, kutakuwepo na kivunge cha kufundishia na kujifunzia katika Elimu ya Awali ambacho kitakuwa na vifaa mbalimbali na maelekezo ya namna ya kutumia vifaa hivyo.

### 2.5 Elimu jumuishi

Ni mfumo wa elimu unaotoa fursa sawa ya elimu kwa watoto wote bila kujali tofauti zao. Huu ni utaratibu unaozingatia mahitaji na ushirikishwaji wa kila mtoto wakiwemo wenye mahitaji maalumu kama vile watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, yatima, wenye usikivu na uoni hafifu, wenye kujifunza taratibu na wenye kujifunza kwa haraka, wenye magonjwa na ulemavu. Elimu hii inasaidia kubaini vikwazo vya ujifunzaji ili kuweka mikakati stahiki inayomwezesha kila mtoto kuwa na fursa ya kupata elimu.

#### 2.5.1 Darasa jumuishi

Ni darasa ambalo mwalimu na watoto wanashirikiana katika shughuli mbalimbali na kujenga mazingira ambayo kila mtoto anajisikia salama, anasaidiwa na kuhimizwa kutoa maoni yake. Watoto katika darasa hili wana mahitaji tofauti na changamoto za ujifunzaji. Mwalimu, ni vema kulifahamu darasa lako kwa idadi ya watoto, tabia na mitindo yao ya ujifunzaji ili uweze kutoa msaada stahiki. *Je, utafanya nini ili watoto hawa waweze kujifunza sawa na wengine?*

Pamoja na majibu yako uliyonayo, zingatia yafuatayo:

i. Mahitaji ya watoto na mazingira stahiki ya ujifunzaji;
ii. Ushiriki wa mtoto katika tendo la kujifunza;



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 7 9/18/19 4:59 PM

iii. Kuhamasisha watoto kushiriki kikamilifu katika kujifunza;
iv. Ushiriki wa wazazi katika maendeleo yao ya kitaaluma, afya, imani na malezi;
v. Kuweka mikakati ya upimaji na kufanya utambuzi wa mapema;
vi. Kuwepo kwa vifaa vinavyoendana na mahitaji ya watoto;
vii. Kutoa kazi zinazowashirikisha watoto wote;
viii. Kutumia vitendo na ishara zinazoendana na mitindo mbalimbali ya tabia ya ujifunzaji wa watoto, kwa mfano wale wanaojifunza kwa kuona, kusikia na kutenda; na
ix. Kuzingatia jinsi katika ujifunzaji na ufundishaji.

### 2.5.2 Wajibu wa mwalimu katika darasa jumuishi

Katika darasa jumuishi kila mtoto ni wa kipekee na anajifunza kulingana na mahitaji yake. Hivyo, wajibu wa mwalimu katika kutekeleza Elimu jumuishi ni pamoja na:

i. Kutumia mbinu na mikakati shirikishi inayokidhi mahitaji ya ujifunzaji pamoja na kutoa fursa sawa kwa watoto wote;
ii. Kuwezesha ujifunzaji kwa kumshirikisha kila mtoto kulingana na mahitaji yake;
iii. Kukuza uelewa katika stadi mbalimbali kwa kutumia zana za kuona, kusikia, kupapasa/kugusa, kuonja na kunusa. Utumiaji wa zana hizi uzingatie afya na usalama wa watoto;
iv. Kushiriki na watoto katika ujifunzaji ili kuwasaidia watoto kujenga dhana ya kile kilichokusudiwa kupitia mwalimu/mlezi. Hii itawasaidia watoto wote wenye mitazamo mbalimbali (mfano, siwezi kufanya, naweza kufanya lakini kwa kusaidiwa, naweza kufanya mwenyewe bila msaada);
v. Kuuliza/kudodosa kwa kutumia mbinu stahiki;
vi. Kutoa shughuli zinazomwezesha mtoto kujifunza kutumia milango ya fahamu zaidi ya mmoja;
vii. Kushirikisha watoto katika uandaaji na utengenezaji wa zana za kufundishia na kujifunzia; na
viii. Kushirikisha wazazi katika maendeleo ya kitaaluma, kiafya, kimaadili na kimalezi (tabia na mienendo) ya watoto.

## 2.6 Utekelezaji wa ratiba ya kila siku

*Mwalimu, unafikiri ni shughuli zipi zinafanyika katika shule ya awali kuanzia mtoto anapofika shuleni mpaka anaporudi nyumbani?* Shughuli zinazofanyika shuleni kuanzia mtoto anapofika mpaka anaporudi nyumbani, ndiyo zinazotengeneza ratiba ya siku. Kwa


Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 8 9/18/19 4:59 PM

kawaida mahitaji ya ujifunzaji ya mtoto ndiyo yatakayokuongoza kutengeneza ratiba ya kila siku. Ni muhimu kuzingatia kwamba watoto hawalingani bali hutofautiana kwa mahitaji na uwezo wa kujifunza.

*Unafikiri, kwa nini ni muhimu kuwa na ratiba katika shule ya awali?* Umuhimu wa kuwa na ratiba katika shule ya awali ni kukuwezesha kutekeleza Mtaala na Muhtasari wa Elimu ya Awali pamoja na majukumu mengine kikamilifu kwa kuzingatia muda uliopangwa. Ratiba katika Elimu ya Awali inawasaidia wazazi/walezi na watoto kujua mtiririko wa matukio ya kila siku shuleni. Mwalimu unapaswa kuandaa ratiba na kuitekeleza ipasavyo kama ilivyoainishwa katika Kiambatisho G. Katika kupanga ratiba kwa ajili ya Elimu ya Awali, unapaswa kuzingatia haki na wajibu wa mtoto kulingana na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009. Sheria hiyo inasisitiza kuwa kila kitu anachokifanya au kufanyiwa mtoto ni lazima kiwe na masilahi kwake. Mwalimu, kati ya mambo yaliyomo katika ratiba ya kila siku ni pamoja na mduara wa asubuhi na mduara wa kuagana.

### 2.6.1 Mduara wa asubuhi

Mwalimu, unaweza kufanya mduara ndani au nje ya darasa kutegemeana na hali ya hewa na miundombinu iliyopo. Watoto wanatarajiwa kuwa kwenye duara au nusu duara kutegemeana na idadi yao, mwalimu unapaswa kuwa sehemu ya watoto katika duara hilo. Katika mduara huu wa asubuhi mbali na mambo mengine, mwalimu anatakiwa kuwatambua watoto waliohudhuria na kufanya nao shughuli mbalimbali za kuwachangamsha ili kuwaandaa kuwa tayari katika ujifunzaji. Baadhi ya mambo ambayo mwalimu utayafanya katika mduara wa asubuhi ni kama ifuatavyo:

i. kusalimiana na watoto kwa kutumia wimbo wa kusalimia;
ii. kucheza mchezo rahisi kuchangamsha watoto kwa ajili ya kujifunza;
iii. kufanya ukaguzi wa afya kwa kujikita kwenye usafi binafsi na magonjwa; na
iv. kufuatilia shughuli za siku iliyopita ambazo watoto walipaswa kuzikamilisha wakiwa nyumbani.

### 2.6.2 Mduara wa kuagana

Ni muda ambao mwalimu unapaswa kupitia shughuli za siku kwa kuuliza watoto wamejifunza nini katika siku hiyo. Unapaswa uwakumbushe watoto juu ya shughuli ambazo wanatakiwa kuzifanya wakiwa nyumbani ili kuongeza maarifa yao. Vilevile, wakumbushe kuchukua tahadhari za kiusalama wakiwa njiani kuelekea nyumbani. Hitimisha siku kwa kuimba wimbo wa kuagana/muziki au mchezo.

# Sura ya Tatu

## Upimaji na tathmini ya maendeleo ya mtoto katika Elimu ya Awali

Mwalimu, karibu katika sura hii ya tatu. Katika sura hii utajifunza upimaji wa maendeleo ya mtoto wa Elimu ya Awali. Aidha, utajifunza aina za upimaji na zana za upimaji.

**Umahiri unaotarajiwa kujengwa**

Baada ya kusoma sura hii, mwalimu utaweza:

i. kueleza dhana ya upimaji wa maendeleo ya mtoto;
ii. kubainisha zana za upimaji; na
iii. kupima na kutathmini maendeleo ya mtoto.

### 3.1 Dhana ya upimaji wa maendeleo ya mtoto

*Mwalimu, unaelewa nini kuhusu dhana ya upimaji wa maendeleo ya mtoto?* Pamoja na majibu yako, ni muhimu kutambua kwamba upimaji wa maendeleo ya mtoto hufanyika kwa kufuatilia mabadiliko kila siku katika ujifunzaji na ukuaji wake kimwili, kiakili, kijamii na kihisia. Mtoto hapaswi kupewa mitihani wala majaribio kwa ajili ya kupima maendeleo yake. Mwalimu unatakiwa ufuatilie maendeleo ya kila mtoto ya ukuaji na ujifunzaji kila siku hatua kwa hatua na kuweka kumbukumbu itakayoonesha jinsi mtoto anavyobadilika. Unapopima maendeleo ya mtoto unatakiwa kuzingatia yafuatayo:

**a. Njia ya upimaji**

Zipo njia mbalimbali za kupima maendeleo ya mtoto, lakini njia ya uhakika ni ya uchunguzi na ufuatiliaji wa maendeleo ya kila siku ya mtoto. Uchunguzi huu unapaswa kufanyika wakati mtoto anatenda shughuli mbalimbali darasani au nje ya darasa. Kwa hiyo, upimaji si tukio la kufanyika kwa siku moja kwani ni vigumu kupata viashiria sahihi vya maendeleo ya mtoto kwa kutumia taarifa iliyokusanywa kwa siku moja.

**b. Muktadha wa upimaji**

Mwalimu, maendeleo ya mtoto yanapimwa kwa kutumia mbinu mbalimbali. Hata hivyo, mbinu iliyopendekezwa zaidi ni uchunguzi ambao hufanyika ndani na nje ya darasa wakati wa kutekeleza shughuli mbalimbali za ujifunzaji na ufundishaji



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 10 9/18/19 4:59 PM

kwa kuzingatia ratiba ya kila siku. Aidha, uchunguzi unaweza kufanywa na wazazi/walezi kwa kushirikiana na mwalimu. Fomu ya uchunguzi yenye vigezo maalumu iliyoandaliwa itawasaidia walimu na wadau wa elimu kubaini maendeleo na mabadiliko ya kila mtoto. Taarifa za uchunguzi wa maendeleo ya mtoto zitasaidia katika kuweka mikakati ya kuhakikisha kwamba mahitaji ya kila mtoto kiakili, kimwili, kijamii, na kihisia yanapatikana.

**c. Mchakato wa tathmini**

Mwalimu unapaswa kukusanya na kuunganisha taarifa za uchunguzi za kila mtoto mara kwa mara katika kipindi cha ujifunzaji wake. Upimaji haufanyiki kama tukio la mara moja bali ni tendo endelevu linalofanyika kwa kipindi fulani na kuweka kumbukumbu ya maendeleo na ukuaji wa mtoto hatua kwa hatua.

**d. Upimaji unaozingatia viwango**

Taratibu za upimaji zinasisitiza kuwa upimaji wa maendeleo ya mtoto usifanywe nje ya programu au mtaala husika. Upimaji unapaswa kuzingatia mtaala na mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji. Wajibu wa mwalimu ni kuchunguza maendeleo ya mtoto ya kila siku hatua kwa hatua na kurekodi taarifa kwa ajili ya kuboresha ujifunzaji na ufundishaji.

Mwalimu, zingatia viwango vya upimaji kama vilivyobainishwa katika kiambatisho C na E. Upimaji wa maendeleo ya mtoto unapaswa kuweka mkazo zaidi katika:

**i. Maendeleo ya mtoto kiakili**

Eneo hili linahusisha kiwango cha uelewa na utendaji wa mtoto wa stadi mbalimbali katika kutafsiri, kutofautisha, kulinganisha, kutambua alama, namba, herufi, michoro, picha na kutatua tatizo linalomkabili. Vilevile, maendeleo ya mtoto kiakili hujumuisha kuwasiliana, kusikiliza, kujieleza, kutumia misamiati katika lugha, kujenga dhana za kisayansi na kihisabati, kuuliza maswali ya kiudadisi, kufikiri na kutafakari kwa kina.

**ii. Maendeleo ya mtoto kimwili**

Eneo hili linahusu mabadiliko ya mtoto kimwili likihusisha mtoto kuongezeka uzito, kimo na umbo. Upimaji wa mtoto utahusisha mabadiliko ya mtoto katika maeneo hayo pamoja na matendo mbalimbali anayoweza kutenda

kulingana na hatua za makuzi. Matendo hayo ni yale yanayohusisha misuli mikubwa na midogo kama vile kukimbia, kucheza mpira, kuumba, kuchora na kupaka rangi. Mwalimu unatakiwa kutambua kuwa maendeleo ya mtoto yanategemea huduma za afya, lishe bora na usafi.

**iii. Maendeleo ya mtoto kijamii na kihisia**

Eneo hili linahusisha mabadiliko ya mtoto kitabia, kimahusiano, utayari katika kutenda, kuiga, kushirikiana na kuwasiliana. Vilevile, eneo hili linahusisha kuthamini utu wake na wa watu wengine na kuthamini vitu vilivyoko katika mazingira, kuonesha uvumilivu, uzalendo na kuwa na mtazamo chanya.

Mwalimu, unapaswa kuzingatia yafuatayo katika kupima maendeleo ya mtoto:

i. kumfahamu kila mtoto na mahitaji yake;
ii. kumpima kila mtoto peke yake bila kufanya ulinganifu na watoto wengine;
iii. kumpima mtoto kwa kila hatua ya ujifunzaji; na
iv. kutumia viashiria pendekezwa ili kubaini kiwango cha mabadiliko kilichofikiwa.

Taarifa zinazotokana na upimaji zitakuwezesha kupata picha halisi ya mabadiliko ya mtoto hatua kwa hatua katika vipindi tofauti.

## 3.2 Aina za upimaji

Aina tatu za upimaji zitatumika katika kupima maendeleo ya mtoto wa Elimu ya Awali.

**i. Upimaji wa awali**

Upimaji huu hufanywa na mwalimu wa darasa la awali kubaini uzoefu wa awali wa mtoto na vitu anavyoweza kuvifanya. Mtoto atapimwa mara tu anapofika shuleni kwa mara ya kwanza ili kubaini uwezo alionao kabla ya kuanza Elimu ya Awali. Aidha, upimaji huu utamwezesha mwalimu kubaini mahitaji binafsi ya mtoto, kutoa afua stahiki pamoja na kuandaa mpango wa kumwezesha kufikia malengo yaliyokusudiwa. Upimaji huu pia unatumika kubaini watoto wenye miaka 3 na 4 ambao wana utayari ili waweze kujiunga na Elimu ya Awali. Mwalimu unashauriwa kuzingatia viashiria vilivyoainishwa katika fomu ya viashiria vya utayari wa mtoto (Kiambatisho H) ili uweze kumwandikisha mtoto wa umri wa miaka 3 na 4 kujiunga na darasa la Elimu ya Awali. Pamoja na fomu hiyo, unatakiwa kuzingatia vigezo vingine kulingana na mahitaji ya mtoto na mazingira.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 12 9/18/19 4:59 PM

### ii. Upimaji endelezi

Upimaji huu unafanyika wakati wote wa ujifunzaji na ufundishaji ndani na nje ya darasa. Vilevile utamsaidia mwalimu kubaini ufanisi katika utendaji wa shughuli mbalimbali za kila siku za mtoto. Upimaji huu umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni upimaji gunduzi na upimaji chekeche. Taarifa za upimaji huu zitatumika katika kutoa msaada na ushauri stahiki katika malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto. Pamoja na upimaji gunduzi, upimaji chekeche utatumika kubaini mtoto mwenye vikwazo vya kujifunza ili kuchukua hatua za kumsaidia.

### iii. Upimaji tamati

Upimaji huu unafanyika mwisho wa mafunzo ambapo mwalimu anaangalia maendeleo ya mtoto tangu alipoanza mpaka anapomaliza Elimu ya Awali. Katika upimaji huu utatumia fomu iliyo katika kiambatisho F.

## 3.3 Zana za upimaji

Maendeleo ya mtoto katika shule yanategemea upimaji wa mara kwa mara unaofanywa na mwalimu. *Je, mwalimu unatumia nini unapopima maendeleo ya mtoto?* Bila shaka upimaji unafanyika kwa kutumia zana mbalimbali ili kupata na kutunza taarifa za maendeleo ya mtoto tangu anapojiunga na shule hadi anapomaliza. Baadhi ya zana zinazoweza kutumika katika ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya upimaji wa maendeleo ya mtoto ni pamoja na hojaji, dodoso, orodha hakiki, mkoba wa kazi na fomu ya kumbukumbu ya maendeleo ya mtoto.

Taarifa zinazotokana na matumizi sahihi ya zana hizi zitakusaidia mwalimu kubaini kiwango cha maendeleo alichofikia mtoto. Aidha, ni vyema kuwa na kumbukumbu zilizojazwa kwenye fomu maalumu au daftari ambazo zinaonesha shughuli mbalimbali alizotenda mtoto kwa kuzingatia viashiria vilivyowekwa. Zifuatazo ni baadhi ya zana za ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya upimaji wa maendeleo ya mtoto:

### i. Mkoba wa kazi

Ni kifaa kinachotumika kuhifadhi kazi za mtoto alizozifanya katika nyakati tofauti. Kutokana na kazi hizo unaweza kubaini kiwango cha mabadiliko ya utendaji wa mtoto. Mwalimu unatakiwa kumwandalia kila mtoto mkoba wake wa kazi ili kukuwezesha kupima mabadiliko katika nyanja za maarifa, stadi na mwelekeo.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 13 9/18/19 4:59 PM

**ii. Orodha hakiki**

Ni zana ya upimaji inayotumika kupima utendaji wa mtoto katika shughuli mbalimbali anazofanya katika tendo la ujifunzaji. Unapoandaa orodha hakiki unatakiwa kuandika vigezo ambavyo utavizingatia wakati wa kupima shughuli mbalimbali anazotenda mtoto. Vigezo vinavyoandaliwa vinatakiwa viendane na kile unachopima. Mwalimu, unaweza kutumia orodha hakiki baada ya kukamilisha shughuli za ujifunzaji na ufundishaji zinazotarajiwa kumwezesha mtoto kujenga umahiri mahususi mmoja ili kubaini ni kwa kiasi gani ameweza kujenga umahiri mahususi husika. Kiambatisho C kinatoa mfano wa ujazaji wa orodha hakiki kwa umahiri mahususi wa kujali.

**iii. Hojaji**

Ni zana ya upimaji yenye maswali ambayo mwalimu huyatumia kupata taarifa kupitia mazungumzo ya ana kwa ana na mtoto, mzazi/mlezi na mtu yeyote mwenye taarifa za maendeleo ya mtoto. Hojaji itakusaidia kubaini mahitaji na matatizo ya mtoto. Mfano wa hojaji ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho D.

**iv. Dodoso**

Ni maswali yaliyoandaliwa kwa lengo la kupata taarifa za maendeleo ya mtoto kwa njia ya maandishi. Dodoso huandaliwa na mwalimu na kujazwa na mtu yeyote ambaye ana taarifa sahihi kuhusu maendeleo ya mtoto husika.

**v. Fomu ya maendeleo ya mtoto**

Mwalimu, katika fomu hii utaonesha maendeleo ya mtoto katika nyanja zote za ukuaji na ujifunzaji ikiwa ni pamoja na umahiri alioujenga mtoto kwa kipindi husika. Fomu hii pia itaonesha maendeleo ya mtoto kitabia na kiafya. Mwalimu unaweza kujaza fomu hii ya maendeleo ya mtoto baada ya miezi mitatu, mwishoni mwa muhula wa masomo au mwishoni mwa mwaka kulingana na mahitaji yako. Mfano wa fomu ya maendeleo ya mtoto ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho E.

Pia unatakiwa kuandaa taarifa ya maendeleo ya kila mtoto ambayo itatumwa kwa mzazi kuonesha maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji, maendeleo ya kitabia na kiafya. Mfano wa fomu ya taarifa ya maendeleo ya mtoto ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho F. Mwalimu, taarifa sahihi zinazotokana na upimaji huo



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 14 9/18/19 4:59 PM

zinatakiwa kuhifadhiwa mahali salama ili ziweze kutumika katika kutathmini maendeleo ya mtoto katika hatua mbalimbali. Taarifa hizi zinaweza kutumiwa na wadau mbalimbali wakiwemo wazazi/walezi katika kutatua matatizo ya ukuaji na ujifunzaji wa mtoto na uboreshaji wa programu kwa ujumla.

### 3.4 Tathmini ya maendeleo ya mtoto

*Mwalimu, unaelewa nini kuhusu tathmini ya maendeleo ya mtoto?* Tathmini ni mchakato wa uchambuzi na tafsiri ya takwimu au taarifa ya upimaji ili kufanya maamuzi ya uboreshaji wa huduma stahiki kwa mtoto. Tathmini itakuwezesha kujua ni kwa kiasi gani mtoto anafanya vizuri katika nyanja zote za ukuaji na ujifunzaji.

Unapofanya tathmini, kumbuka kuzingatia maeneo yote ya ujifunzaji yaliyoainishwa katika Mtaala na Muhtasari wa Elimu ya Awali.

Faida ya tathmini ni kugundua mwenendo wa maendeleo ya mtoto na kuandaa mikakati ya uboreshaji. Tathmini kwa kawaida inapaswa kufanyika mwishoni mwa mwaka. Aidha, kutokana na tathmini uliyoifanya, unaweza kubuni maboresho muhimu yanayostahili kufanyika ili malengo ya Elimu ya Awali yaweze kufikiwa.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 15 9/18/19 4:59 PM

# Sura ya Nne

## Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Ewali

Uwepo wa Mtaala mzuri ni jambo moja muhimu, lakini utekelezaji wa mtaala huo kwa ufanisi ni jambo jingine ambalo mwalimu unahitaji kulizingatia sana. Sura hii inaeleza namna utakavyotekeleza Mtaala wa Elimu ya Awali. Utajifunza namna ya kufanya maandalizi ya ufundishaji na namna ya kumwezesha mtoto kujenga umahiri uliobainishwa katika Muhtasari.

**Umahiri unaotarajiwa kujengwa**

Baada ya kusoma sura hii, mwalimu utaweza:

i. kufanya maandalizi stahiki ya ufundishaji;
ii. kubainisha mbinu na zana zitakazomwezesha mtoto kujenga umahiri; na
iii. kueleza namna ya kupima maendeleo ya mtoto katika kutenda shughuli zilizokusudiwa.

### 4.1 Maandalizi ya ufundishaji

Maandalizi ya ufundishaji ni jambo la msingi sana ambalo mwalimu unatakiwa kufanya kabla ya kufundisha. Ili uweze kufundisha kwa ufanisi, yapo maandalizi muhimu ambayo unapaswa kuyafanya. Maandalizi hayo ni pamoja na kuandaa Azimio la kazi, Andalio la somo, Nukuu za somo na zana za kufundishia na kujifunzia kulingana na umahiri uliokusudiwa.

#### 4.1.1 Azimio la kazi

Ni mpango wa utekelezaji wa Muhtasari unaoutayarisha mwalimu ili kukuwezesha kuandaa andalio la somo na kufundisha kama ilivyoainishwa katika muhtasari. Mpango huu huonesha jinsi umahiri mkuu ulivyovunjwa katika umahiri mahususi ili uweze kujengwa kwa muda uliopangwa.

Muundo wa Azimio la kazi unahusisha vipengele vifuatavyo:

**Umahiri mkuu**

Ni uwezo wa kutenda jambo kwa usahihi na kwa ufanisi unaokusudiwa kufikiwa na mtoto baada ya kujifunza kwa muda fulani. Umahiri mkuu hujengwa na umahiri mahususi kadhaa atakazojenga mtoto hatua kwa hatua.

**Umahiri mahususi**

Ni uwezo maalum ambao mtoto anaujenga baada ya kutenda shughuli mbalimbali kwa muda maalum.

**Shughuli za kutendwa na mtoto**

Ni vitendo ambavyo mtoto anapaswa kuvifanya ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Kutakuwa na shughuli kuu ambazo zimeainishwa kwenye Muhtasari na shughuli ndogondogo ambazo zimeainishwa kwenye mwongozo huu. Mwalimu, unapaswa kuangalia ni vitendo gani vitafanywa na mtoto ili kutekeleza shughuli ndogo husika. Kumbuka kuwa shughuli ndogo moja inaweza kutekelezwa katika ufundishaji ndani ya kipindi kimoja au zaidi kutegemea ukubwa wa shughuli hiyo. Vilevile unakumbushwa kwamba shughuli zilizochakatwa humu ni baadhi ya shughuli anazoweza kutenda mtoto kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo, unapaswa kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kuandaa shughuli mpya kulingana na umahiri unaotaka kuujenga.

**Mwezi**

Kipengele hiki utajaza mwezi ambao utafundisha shughuli zinazojenga umahiri husika.

**Wiki**

Kipengele hiki utajaza wiki katika mwezi ambao shughuli husika itatekelezwa.

**Idadi ya vipindi**

Ni kadirio la muda utakaotumika katika ujifunzaji na ufundishaji kwa kuzingatia idadi ya shughuli za kutenda mtoto katika kujenga umahiri uliokusudiwa. Kadirio hili la muda limewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 20. Hata hivyo haya ni mapendekezo tu, idadi ya vipindi inaweza kubadilika kulingana na mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji.

**Vifaa/Zana za kufundishia na kujifunzia**

Hivi ni vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia zitakazotumika katika mchakato wa



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 17 9/18/19 4:59 PM

kutenda shughuli husika. Ni muhimu zana za kufundishia na kujifunzia zitaandaliwa kwa kuzingatia mazingira halisi na uelewa wa mtoto.

**Zana za upimaji**

Ni zana zitakazotumika kupima maendeleo ya mtoto katika kutenda shughuli zitakazomwezesha kujenga umahiri mahususi.

**Rejea**

Ni machapisho yote anayoyatumia mwalimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani.

**Maoni**

Sehemu hii unaandika maoni yako kuhusu mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji kulingana na kiwango kilichofikiwa au kutofikiwa kwa umahiri uliokusudiwa.

### 4.1.2 Andalio la somo

Ni mpango unaouandaa ambao utaufuata wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa shughuli mbalimbali zinazojenga umahiri mahususi. Katika Andalio la somo, utaonesha namna utakavyofundisha shughuli husika ukizingatia mbinu, zana na muda uliopangwa. Andalio la somo lina vipengele vifuatavyo: umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli kuu, shughuli ndogo, vifaa/zana, rejea, shughuli za kutendwa na mwalimu, shughuli za kutendwa na mtoto, viashiria pendekezwa vya utendaji, tathmini ya ufundishaji na ujifunzaji na maoni. Muundo wa andalio la somo ni kama unavyoonekana katika Kiambatisho B. Maelezo ya vipengele hivi ni sawa na yale yaliyotolewa katika vipengele vya Azimio la kazi isipokuwa vipengele vifuatavyo ambavyo havipo kwenye Azimio la kazi:

**Shughuli za kutendwa na mwalimu**

Ni vitendo anavyotenda mwalimu ili kumwezesha mtoto kujenga umahiri.

**Shughuli za kutendwa na mtoto**

Ni vitendo vinavyotendwa na mtoto ili kujenga umahiri husika.

**Viashiria pendekezwa vya utendaji**

Ni matendo yatakayooneshwa na mtoto baada ya kujenga umahiri uliokusudiwa kwa kipindi fulani.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 18 9/18/19 4:59 PM

**Tafakuri**

Ni hatua ya kutafakari somo kwa ujumla wake katika hatua zote. Mwalimu unaweza kutumia maswali na majibu kubaini stadi zilizojengeka, changamoto zilizojitokeza na mafanikio ya ufundishaji na ujifunzaji kwa ujumla. Katika sehemu hii mwalimu unapaswa kuonesha tafakuri ya mwenendo mzima wa somo.

**Tathmini ya ufundishaji na ujifunzaji**

Mwalimu, unatakiwa kutathmini ili kubaini kiwango kilichofikiwa katika lengo la ufundishaji na ujifunzaji, na kutoa maamuzi ya kuboresha ufundishaji wa mtoto.

**Maoni**

Katika sehemu hii mwalimu unapaswa kuonesha mtazamo wako wa jumla kuhusu somo na jinsi ya kuendelea mbele.

### 4.1.3 Nukuu za somo

Baada ya kuandaa Andalio la somo, unapaswa kuandaa nukuu za somo. Haya ni maudhui unayoyaandaa ili kukusaidia katika ufundishaji wa umahiri husika.

## 4.2 Kumwezesha mtoto kujenga umahiri

Mwalimu, baada ya kujifunza namna ya kufanya maandalizi ya ufundishaji, katika sehemu hii, utajifunza namna ya kumwezesha mtoto kujenga umahiri uliokusudiwa. Mtaala wa Elimu ya Awali unasisitiza ujenzi wa umahiri kwa mtoto katika maeneo yafuatayo: Kuhusiana, Kuwasiliana, Kutunza afya, Kutunza mazingira, Kumudu stadi za kisanii na Kutumia dhana za kihisabati. Ili kuwawezesha watoto kujenga umahiri, ni muhimu kuzingatia mbinu na zana za kufundishia na kujifunzia, shughuli za kutendwa na watoto na mbinu za upimaji. Katika kila umahiri mahususi kuna mbinu, zana, na shughuli pendekezwa zilizobainishwa. Hata hivyo, mwalimu unapaswa kuwa mnyumbufu katika kutumia mbinu, zana na shughuli nyingine ili kumwezesha mtoto kujenga umahiri uliokusudiwa.

Katika shughuli ndogo zinazopendekezwa, kuna mifano ya michezo ambayo imewekwa ili kusaidia kutekeleza shughuli hizo. Hata hivyo, mwalimu unapaswa kuwa mbunifu na mnyumbufu kutumia michezo mingine unayoona itakusaidia kutekeleza shughuli husika. Katika kila mchezo wanaocheza watoto kuna jambo wanalojifunza. Katika kujifunza



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 19 9/18/19 4:59 PM

jambo hilo, watatafakari **(tafakari)** vitendo muhimu vya ujifunzaji walivyotenda wakati wa mchezo ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Vilevile, watahusisha **(husisha)** maarifa waliyojifunza na vitendo vingine walivyowahi kuona au kutenda wakati mwingine. Aidha, watoto wanapaswa kujua ni kwa namna gani watatumia **(tumia)** stadi na maarifa waliyoyapata katika shughuli husika katika maisha yao ya kila siku. Hivyo basi, katika michezo iliyopendekezwa kuna mapendekezo ya maswali ya Tkutumika pamoja na maswali ya, **Tafakari, Husisha na Tumia** ambayo yatakusaidia kuongoza mjadala wakati wa ujifunzaji na ufundishaji. Ufuatao ni mchanganuo wa umahiri kama ulivyobainishwa katika mtaala pamoja na shughuli mbalimbali katika kujenga umahiri huo.

### 4.2.1 Kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kuhusiana

Ufanisi wa mtoto katika kujifunza unategemea kwa kiasi kikubwa stadi za uhusiano alizonazo. Kuhusiana kunamwezesha mtoto kukua kiakili, kimwili, kijamii na kihisia.
*Je, mwalimu utamwezeshaje mtoto kujenga uwezo wa kuhusiana?*
Pamoja na majibu uliyonayo, unatakiwa kujenga na kuimarisha uhusiano mzuri kati yako na mtoto na kuwa mfano mzuri wa kuigwa. Unatakiwa pia kukuza uhusiano mzuri kati ya mtoto mmoja na mwingine na kati ya shule na jamii inayowazunguka.

Mwalimu, katika eneo hili la kuhusiana utawawezesha watoto kujenga tabia zifuatazo: kujali, kuheshimiana na kujitawala. Pamoja na hayo, unaweza kuwashirikisha watoto katika mambo mengine yatakayowajengea uwezo wa kukuza uhusiano mwema. Mwalimu, kumbuka kuwa watoto wanatoka katika mazingira tofauti, hivyo ni muhimu kuzingatia mila na desturi za sehemu husika. Umahiri huu umejengwa na umahiri mahususi tatu kama ifutavyo:

#### 4.2.1.1 Kumwezesha mtoto kujenga tabia ya kujali

Mwalimu, ili kumwezesha mtoto kujenga tabia ya kujali, ni muhimu wewe mwenyewe uoneshe kwamba unawajali watoto na watu wengine pamoja na vitu vilivyopo katika mazingira. Hakikisha kuwa unakuwa makini katika maamuzi yako ya kila siku ikiwemo kujali muda na kuwa na haiba stahiki katika ufundishaji wako. Aidha, unapaswa kuwaongoza watoto kufanya shughuli mbalimbali zitakazowawezesha kujenga tabia ya kujali ikiwa ni pamoja na kutambulishana na kushirikiana katika kazi mbalimbali.

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kujenga tabia ya kujali**

Mtoto mwenye tabia ya kujali hujifunza vyema, hujijali na kuwajali wengine. Pia huzingatia muda, kanuni na taratibu, hujali shughuli anazozifanya na hupendwa na wengine.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 20 9/18/19 4:59 PM

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Onesho mbinu, kisa mafunzo, hadithi, ngonjera, maigizo, nyimbo, michezo, maswali na majibu.

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Runinga, kanda za video, redio, michoro, vitabu vya hadithi, picha

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kutambulishana**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kujitambulisha kwa kutaja majina yao kamili na jinsi zao;
ii. kutaja majina ya wazazi/walezi wao na watu wengine wanaoishi nao;
iii. kuelezea mahali wanapoishi;
iv. kutaja jina la shule wanayosoma;
v. kuwatambulisha watoto wengine kwa majina yao;
vi. kutaja majina ya watu wengine na kueleza uhusiano wao;

Mchezo na wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Jieleze, jieleze
b. Mchezo wa majina

**a. Wimbo: Jieleze, jieleze**

*Jieleze jieleze jieleze jieleze*
*Jieleze jieleze, najieleza mama*
*Mimi hapa ni Vida,*
*baba yangu ni Andrew,*
*mama yangu ni Anna*
*Nimejieleza mama.*

Hatua za Kufuata:

i. Wapange watoto katika mduara.
ii. Anza kwa kujitambulisha jina lako kwa kutumia wimbo wa 'jieleze jieleze'.
iii. Mtoto mmoja mmoja aingie ndani ya mduara na kujitambulisha kwa jina lake kwa kutumia wimbo wa 'jieleze jieleze' mpaka utakapoona inafaa kulingana na idadi ya watoto.
iv. Kwa siku ya kwanza, watoto wanaweza kujieleza kwa kutaja majina yao.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 21 9/18/19 4:59 PM

v. Unaweza kuongezea majina ya wazazi na mahali wanapoishi kutokana na uelewa wa watoto.

**Tafakari**

Ni majina gani umeyasikia yakitajwa wakati wa mchezo?

**Husisha**

Ni majina gani mengine umewahi kuyasikia?

**Tumia**

Je, inakusaidia nini kufahamu jina la rafiki yako au la mtu mwingine?

## b. Mchezo: Mchezo wa majina

Hatua za kufuata:

i. Wapange watoto kwenye mduara wenye kati ya watoto 10 hadi 15.

ii. Anza kwa kutaja jina lako na jinsi yako. Amua kuelekea upande mmoja wa kushoto au kulia.

iii. Mtoto anayefuata kwenye mduara upande wa kulia au kushoto arudie jina lako na jinsi yako na kisha ataje jina lake na jinsi yake. Kwa mfano, Jamila anaanza kwa kusema, "Jina la mwalimu wetu ni Ali ni mvulana, Jina langu ni Jamila ni msichana." Mohammed anafuata, "Huyu ni Jamila ni msichana na jina langu ni Mohammed ni mvulana." Sharifu anaendelea, "Huyu ni Mohammed ni mvulana na jina langu ni Sharifu ni mvulana." Janeth anaendelea, "Huyu ni Sharifu ni mvulana na jina langu ni Janeth ni msichana "

iv. Mchezo unaendelea hadi watoto wote watakapomaliza kujitambulisha.

**Tafakari**

i. Taja jina la mtoto mwenzako uliyemtambulisha na jinsi yake

ii. Umesikia majina gani mengine yaliyotajwa?

**Husisha**

Ni majina gani mengine umewahi kuyasikia?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 22 9/18/19 4:59 PM

**Tumia**

Je, inakusaidia nini kufahamu jina la rafiki yako au la mtu mwingine?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kujitambulisha kwa majina kamili na jinsi yake;
ii. kutaja jina la mahali anapoishi na shule anayosoma; na
iii. kuwatambulisha wengine kwa majina na uhusiano wao.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kushirikiana katika kazi mbalimbali**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja kazi wanazofanya pamoja;
ii. kushiriki katika kazi mbalimbali;
iii. kueleza umuhimu wa kufanya kazi kwa kushirikiana na;
iv. kutenda matendo ya kuvumiliana.

Michezo inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Kupeana kifurushi
b. Amini boda boda

## a. Mchezo: Kupeana kifurushi

Vifaa: Mpira, kifurushi kinacholingana na kasha la chaki, kamba ya katani, kitambaa

Hatua za kufuata:

i. Wagawe watoto katika vikundi kulingana na idadi yao.
ii. Teua kundi moja lijongee mbele ya darasa.
iii. Kundi lililojongea mbele ya darasa wakae katika duara.
iv. Waoneshe kifurushi ulichoandaa.
v. Anza kwa kumpa mtoto wa kwanza kifurushi naye ampe kifurushi mtoto anayefuata.
vi. Kifurushi kinapokuwa kinazunguka, mwalimu uwe unapiga makofi au unagonga meza au ngoma.
vii. Unapositisha kugonga meza au ngoma, mtoto aliye na kifurishi abadili mwelekeo. Iwapo mchezo ulikuwa unaelekea kulia, ubadilike na kuelekea kushoto kisha endelea kugonga meza au kupiga makofi.
viii. Mchezo utaisha ikiwa kila mtoto amepata nafasi ya kupokea kifurushi kutoka kwa mwenzake.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 23 9/18/19 4:59 PM

**Tafakari**

Ulijisikiaje ulipopokea kifurushi kutoka kwa mwenzako?

**Husisha**

i. Kazi gani nyingine huwa mnafanya pamoja mkiwa nyumbani? Huwa unafanya na nani?
ii. Huwa unajisikiaje unapofanya jambo lolote pamoja na wenzio?

**Tumia**

Utafanya nini ili marafiki zako wapende kucheza na wewe?

**b. Mchezo: Amini bodaboda**

Vifaa: Kitambaa, makopo, chupa tupu za maji, viunzi na mipira

Hatua za kufuata:

i. Chora mstari wa kuanzia upande mmoja wa eneo la kuchezea na wa kumalizia upande mwingine wa eneo la kuchezea. Acha nafasi yenye urefu wa meta 15 kati ya mistari hiyo kutegemeana na eneo lililopo.
ii. Tawanya vitu mbalimbali katika eneo la kuchezea ili viwe vizuizi (viunzi).
iii. Gawa watoto katika jozi. Iambie kila jozi isimame kwenye mstari wa kuanzia.
iv. Katika kila jozi mtoto mmoja ajitolee kufungwa macho kwa kutumia kitu chochote, kwa mfano, kitambaa safi. Mtoto huyo ataitwa Bodaboda, mwingine atakuwa mwongozaji. Bodaboda atasimama mbele ya mwongozaji.
v. Eleza kuwa mwongozaji atatumia ishara nne (4) za kumwongoza Bodaboda nazo ni:

| | | |
|---|---|---|
| a. NENDA | - | atagusa kisogo |
| b. SIMAMA | - | atagusa mgongo |
| c. KUELEKEA KUSHOTO | - | atagusa bega la kushoto |
| d. KUELEKEA KULIA | - | atagusa bega la kuli**a** |

vi. Eleza kuwa mwongozaji atatakiwa kumwongoza Bodaboda katika hali ya usalama ndani ya eneo la kuchezea akitembea miongoni mwa Boda boda wengine. Amwongoze Bodaboda kutembea bila kugusa kizuizi huku akihakikisha safari inakuwa ya kuvutia kutoka mstari wa kuanzia hadi mstari wa kumalizia. Endapo atagusa kikwazo watarudi tena kwenye mstari wa kuanzia na kuanza safari upya.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 24 9/18/19 4:59 PM

vii. Jozi zitakapofika mwisho, watoto watabadilishana nafasi. Bodaboda atakuwa mwongozaji na mwongozaji atakuwa Bodaboda. Katika hatua hii mstari wa kumalizia utakuwa mstari wa kuanzia.
viii. Mchezo utamalizika baada ya kila mtoto kucheza nafasi zote mbili.

**Tafakari**

i. Ulijisikiaje kumwongoza mwenzako kuvuka vizuizi?
ii. Ulijisikiaje kuongozwa na mwenzako kuvuka vizuizi?
iii. Ulimwamini mwenzako? Kwa nini?
iv. Nini kingetokea kama ungetakiwa kuvuka vizuizi bila kuongozwa?

**Husisha**

i. Ulishawahi kuwaongoza watoto wengine?
ii. Nitajie watu unaowaamini? Kwa nini?

**Tumia**

i. Kwa nini ni vizuri kumsaidia rafiki yako?
ii. Unaweza kufanya nini kumsaidia mwenzio mwenye tatizo?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kushirikiana na wenzake katika michezo;
ii. kuonesha uvumilivu; na
iii. kushiriki katika kazi mbalimbali.

**4.2.1.2 Kumwezesha mtoto kujenga tabia ya kuheshimu**

Mwalimu, mwongoze mtoto katika kujenga tabia ya kuheshimu ambayo itamwezesha kuthamini utu wake na watu wengine bila kujali rangi, dini, jinsi na kabila. Mtoto akiwezeshwa kujenga tabia hii atakuwa mwenye manufaa katika jamii. Mwalimu unaweza kuwaongoza watoto kufanya shughuli mbalimbali ambazo zitaonesha matendo ya tabia njema.

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kujenga tabia ya kuheshimu**

Mwalimu, kumbuka kuwa mtoto mwenye tabia ya kujiheshimu na kuwaheshimu wengine atajifunza vyema na ataishi vizuri katika jamii inayomzunguka.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Onesho mbinu, kisa mafunzo, maigizo, michezo, hadithi, maswali na majibu



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 25 9/18/19 4:59 PM

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Picha, michoro, runinga, redio, mipira na vitabu

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kujenga tabia ya kusalimiana**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuonesha jinsi wanavyosalimiana nyumbani;
ii. kusalimiana kwa kuzingatia rika; na
iii. kuigiza matendo mbalimbali ya kusalimiana.

Igizo na wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Igizo la kusalimiana
b. Wimbo wa tuamkapo asubuhi

**a. Mchezo: Igizo la kusalimiana**

Vifaa : Picha zinazoonesha watu wa rika mbalimbali wakisalimiana

Hatua za kufuata:

i. Chagua watoto wawili wasimame mbele ya darasa kisha waigize namna ya kusalimiana kwa usahihi wao kwa wao, wao na watu waliowazidi umri.
ii. Watoto waigize namna ya kusalimia kwa kuzingatia rika, kwa mfano, wazazi, kaka na watoto wenzao.
iii. Hakikisha kila mtoto ameshiriki tendo la kusalimiana kwa usahihi.

**Tafakari**

i. Je, ilikuwa rahisi kuigiza kama kaka, baba, mama au dada? Kwa nini?
ii. Je, umeigiza kama nani? Ulijisikiaje kuigiza kama baba, mama, dada, kaka…?

**Husisha**

i. Je, ukiamka asubuhi unamsalimiaje baba, mama, kaka, dada….?
ii. Je, ni watu gani wengine unaowasalimia kila siku?
iii. Je, unajisikiaje ukikutana na mtu asikusalimie?

**Tumia**

i. Kwa nini ni muhimu kusalimia?
ii. Utakapokutana na mtu asipokusalimia utafanyaje?

**b. Wimbo: Tuamkapo asubuhi**

Wafundishe watoto wimbo ufuatao wa kusalimiana

*Tuamkapo asubuhi tuwasalimu wazazi*
*shikamoo baba, shikamoo mama,*
*hiyo ndiyo tabia njema.*
*Tuendapo masomoni tuwasalimu walimu,*
*shikamoo mwalimu, shikamoo mwalimu,*
*hiyo ndiyo tabia njema.*
*Tukutanapo katika michezo tuwasalimu wenzetu,*
*hujambo rafiki, sijambo rafiki,*
*hiyo ndio tabia njema.*

Hatua za kufuata

i. Waulize watoto maswali kama vile, Unapoamka asubuhi unawasalimiaje wazazi?, Je unapokutana na rafiki yako unamsalimiaje?
ii. Waimbie watoto wimbo wa kusalimia huku wakikusikiliza.
iii. Waongoze watoto kuimba wimbo wa kusalimiana.
iv. Hakikisha kila mtoto anashiriki katika kuimba.

**Tafakari**

i. Je, wewe na mwenzako mmesalimianaje?
ii. Je, umemsalimiaje mwalimu?

**Husisha**

i. Je, ni watu gani wengine huwa unawasalimia nyumbani? Unawasalimiaje?
ii. Je, umewahi kusalimiwa na wenzako mnaolingana umri?
iii. Unapokutana na mwenzako mnayelingana umri unamsalimiaje asubuhi?
iv. Je, umewahi kuona watoto ambao huwa hawasalimii?

**Tumia**

i. Je ni vizuri kusalimia? Kwa nini?
ii. Utamwambia nini mtoto ambaye huwa hasalimii ili aanze kusalimia?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 27 9/18/19 4:59 PM

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kuonesha matendo ya kusalimiana; na
ii. kusalimiana kulingana na rika.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kutenda matendo ya tabia njema**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja matendo mbalimbali wanayoyatenda katika mazingira yao.
ii. kubaini matendo ya tabia njema;
iii. kubainisha matendo ya tabia mbaya; na
iv. kutenda vitendo vinavyoonesha tabia njema.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia shughuli hii ni Igizo la tabia njema

**Mchezo: Igizo la tabia njema**

Vifaa: Mkoba, kiti, mavazi mbalimbali

Hatua za kufuata:

i. Chagua watoto sita watakaoigiza/watakaocheza kama kaka, mama na babu;
ii. Chagua wengine wawili watakaocheza kama mtoto na mjukuu;
iii. Watoto sita wavae uhusika stahiki (mfano babu, mama, kaka) na wengine wawili wavae uhusika wa mtoto na mjukuu.

   Mama, kaka na mtoto waonekane wamekaa nyumbani wanaongea na babu anabisha hodi, anaingia amebeba mkoba wake, anakaribishwa na wote wanaamkia. Mtoto anampokea babu mkoba wake na kumkaribisha kiti.
iv. Mwalimu abadili makundi kadiri iwezekenavyo ili watoto wote/wengi washiriki.

**Tafakari**

i. Katika mchezo, kaka alimwamkia babu kwa kusemaje?
ii. Nani alimpokea babu mkoba wake?
iii. Mkoba wa babu uliwekwa wapi?
iv. Babu alikaribishwa nini?

**Husisha**

i. Nani mwingine huwa unamsalimia kila siku?
ii. Mgeni akifika nyumbani kwenu unamfanyia nini?

**Tumia**

i. Ni wakati gani watoto mnatakiwa kusalimia?
ii. Ukirudi nyumbani utamsalimia nani mwingine?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 28 9/18/19 4:59 PM

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kubaini matendo ya tabia njema.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kuvaa mavazi yanayokubalika kulingana na mazingira**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja mavazi yanayovaliwa kulingana na mazingira (shuleni, nyumbani, nyumba za ibada, michezo na hali ya hewa);
ii. kutaja mavazi yasiyokubalika kulingana na mazingira; na
iii. kuonesha mavazi yanayovaliwa kulingana na mazingira (shuleni, nyumbani, nyumba za ibada, michezo na hali ya hewa).

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Mavazi yanayokubalika:

**Mchezo : Mavazi yanayokubalika**

Vifaa : Picha zinazoonyesha mavazi na mazingira mbalimbali,

Hatua za kufuata

i. Andaa picha zinazoonesha mazingira mbalimbali (shuleni, nyumbani, nyumba za ibada, michezoni, hali ya hewa tofauti)
ii. Andaa kadi za picha za mavazi yanayovaliwa katika mazingira mbalimbali.
iii. Chagua mtoto mmoja aoneshe picha ya mazingira na mwingine achague picha ya mavazi yanayoendana na mazingira yaliyochaguliwa na mtoto wa kwanza.
iv. Watoto wote wawili waoneshe picha zao kwa darasa na kisha mwalimu aulize kama picha hizo zinaendana.
v. Fanya hivyo kwa watoto wengine kwa mazingira tofauti.

**Tafakari**

Uliona nini kwenye picha?

**Husisha**

i. Sweta unavaa wakati gani?
ii. Je, ulishawahi kumwona nesi, daktari, polisi au mwanajeshi? walikua wamevaaje?
iii. Ni mavazi gani huvaliwa wakati wa baridi, joto, mvua.

**Tumia**

Utavaa mavazi gani wakati wa baridi?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 29 9/18/19 4:59 PM

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kubaini mavazi yanayokubalika kulingana na mazingira.

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kucheza pamoja kwa kushirikiana**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja michezo wanayocheza nyumbani;
ii. kucheza michezo waliyoitaja; na
iii. kushiriki katika michezo ya vikundi.

Michezo inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Kumbuka aliyedaka
b. Kuvuta kamba
c. Mchezo wa juu chini

**a. Mchezo : Kumbuka aliyedaka**

Vifaa: Mpira

Hatua za kufuata:

i. Wagawe watoto katika vikundi vya watoto 10 -15 na kuunda mduara.
ii. Mpe mpira mtoto mmoja katika kila kikundi.
iii. Elekeza na onesha kuwa, mtoto mmoja mwenye mpira kwenye mduara ataita jina la mtoto mwingine katika mduara na kurusha mpira kwake. Hakikisha kabla ya kurusha mpira, mtoto anayerusha anamtazama machoni yule anayemrushia.
iv. Anayedaka mpira ataita jina la mtoto mwingine katika duara ambaye bado hajapokea mpira na atarusha mpira kwake.
v. Kila mtoto anapaswa kurusha na kupokea mpira mara moja tu hadi mzunguko utakapoisha.
vi. Mwambie kila mtoto akamguse aliyemrushia mpira.
vii. Waeleze watoto kuwa, mchezo utaendelea kwa mwelekeo ule ule ikiwa na maana kuwa kila mtoto ataendelea kumrushia mpira mtoto yule yule aliyemrushia katika mzunguko wa kwanza.
viii. Kadiri wanavyozoea mchezo wahamasishe waongeze kasi ili kupunguza muda wanaotumia kurusha mpira kuanzia mtoto wa kwanza hadi wa mwisho.
ix. Kadiri watoto wanavyomudu kuucheza mchezo ongeza mipira mingine.

Mchezo huu unaweza kuchezwa ndani au nje ya darasa.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 30 9/18/19 4:59 PM

**Tafakari**

i. Ni ugumu gani ulioupata katika kudaka mpira?
ii. Je, ilikuwa rahisi/ngumu kukumbuka jina la uliyemrushia mpira? kwa nini?
iii. Je, ulijisikiaje uliposhindwa/ulipofanikiwa kudaka mpira? kwa nini?

**Husisha**

i. Ni nani uliwahi kumtambulisha kwa wengine?
ii. Mpira unaweza kuufananisha na kitu gani kingine?

**Tumia**

Utafanyaje kujua jina la mgeni akija nyumbani?

**b. Mchezo : Kuvuta kamba**

Vifaa: Kijiti, kamba

Hatua za kufuata:

i. Watoe watoto nje ya darasa.
ii. Wagawe katika timu mbili zinazolingana.
iii. Chora mstari ardhini unaogawa eneo la kuchezea katika sehemu mbili.
iv. Weka alama inayoonekana katikati ya mstari.
v. Weka alama inayogawa kamba katika sehemu mbili zilizo sawa.
vi. Waoneshe kila timu namna ya kuvuta kamba pamoja kuelekea upande wao.
vii. Waambie watoto waanze kuvuta kamba kuelekea upande wao.
viii. Wahimize watoto wa pande zote mbili kuvuta kamba.
ix. Upande mmoja ukivutwa ukavuka alama utakuwa mwisho wa mchezo.
x. Endelea kuwagawa watoto wengine katika timu nao wacheze mpaka utakapoona watoto wengi/wote wameshiriki.

**Tafakari**

i. Timu yako ilifanya nini kuhakikisha inashinda?
ii. Ulijisikiaje baada ya timu yako kushinda katika mchezo wa kuvuta kamba? Kwa nini?
iii. Ulijisikiaje baada ya timu yako kushindwa katika mchezo wa kuvuta kamba?
iv. Unadhani nini kingetokea kama ungevuta kamba peke yako?

**Husisha**

i. Ni michezo gani mingine huwa unacheza na wenzako?
ii. Tofauti na michezo, kazi gani nyingine huwa unafanya na wenzako unapokuwa nyumbani?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 31 9/18/19 4:59 PM

**Tumia**

i. Kwa nini ni vizuri kucheza na wenzako?
ii. Kwa nini ni vizuri kufanya kazi pamoja?

**c. Mchezo: Juu, chini**

Vifaa: Mipira

Hatua za kufuata:

i. Wagawe watoto katika vikundi kulingana na idadi yao.
ii. Teua vikundi viwili vijongee mbele ya darasa.
iii. Wapange watoto wa vikundi hivyo katika mistari miwili, kisha kila kikundi kipe mpira mmoja.
iv. Waoneshe watoto namna ya kupitisha mpira juu ya kichwa na chini katikati ya miguu kwa kutumia mikono yao kutoka mtoto wa kwanza hadi wa mwisho.
v. Mtoto aliyeko mbele ataanza mchezo kwa kupitisha mpira juu ya kichwa chake. Anayefuata atapokea mpira na kuupitisha chini katikati ya miguu yake. Wanaofuata wataendelea kwa mtiririko huo wa kupitisha juu na chini hadi mtoto wa mwisho.
vi. Mchezaji wa mwisho katika mstari akipokea mpira akimbie nao hadi mbele ya mchezaji aliyeko mbele na kuanza kupitisha mpira kwa namna hiyo hiyo.
vii. Muhimize mtoto pindi anapoangusha mpira chini auokote na kuendelea kucheza.
viii. Unaweza kumaliza mchezo wakati wowote unapoona inafaa.

**Tafakari**

Ni ugumu gani ulioupata wakati wa kupitisha mpira juu na chini?

**Husisha**

i. Michezo gani mingine huwa unashirikiana kucheza na wenzako?
ii. Ni kazi gani huwa unafanya na wenzako?

**Tumia**

i. Kwa nini ni vizuri kucheza na wenzako?
ii. Kwa nini ni vizuri kufanya kazi na wenzako?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kucheza pamoja kwa kushirikiana;
ii. kucheza kwa kushirikiana katika vikundi;

iii. kutatua matatizo katika michezo; na
iv. kufuata taratibu na sheria za mchezo.

**4.2.1.3 Kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kujitawala**

Kujitawala ni sehemu muhimu ya kukuza uwezo wa mtoto katika kuhusiana na watu wengine katika mazingira yake. Katika eneo hili, mwalimu utamwezesha mtoto kujenga utayari wa kuyamudu mazingira yake kwa kufanya vitendo mbalimbali vya kujitegemea, kutunza vitu na kutumia njia zinazokubalika kutawala hisia zake.

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kujitawala**

Uwezo wa kujitawala unamsaidia mtoto kumudu mazingira yanayomzunguka.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Igizo dhima, nyimbo, simulizi, majadiliano, michezo, maigizo na kisa mafunzo

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Kibao fumbo, vifaa vya usafi binafsi, mwanasesere, runinga na kanda za video na za sauti

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kufanya vitendo vya kujitegemea**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuonesha vitendo vya namna ya kuvaa na kuvua mavazi;
ii. kufunga na kufungua vifungio mbalimbali (zipu, kamba za viatu, vifungo na vizibo vya chupa);
iii. kufanya usafi binafsi; na
iv. kula na kunywa wenyewe.

**Tafakari**

Ni vitendo gani ulivyoigiza?

**Husisha**

i. Nani anakusaidia kuvua nguo za shule ukifika nyumbani?

**Tumia**

i. Utamsaidiaje rafiki yako asiyeweza kufunga na kufungua vifungo vya shati?
ii. Kwa nini ni vizuri kufanya kazi na wenzako?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kuvaa na kuvua mavazi;
ii. kufunga na kufungua vifungio mbalimbali; na
iii. kufanya usafi binafsi



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 33 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kubaini namna ya kutawala hisia**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitendo vinavyoonesha hisia;
ii. kubaini vitendo vinavyosaidia kutawala hisia;
iii. kueleza namna ya kutawala hisia; na
iv. kufanya vitendo vya kutawala hisia.

Michezo inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:
a. Unajisikiaje
b. Dansi mgando

**a. Mchezo: Unajisikiaje**

Hatua za kufuata:

i. Wapange watoto katika nusu duara wakikutazama.
ii. Onesha ishara inayoashiria hisia ya kufurahi, kucheka, kukasirika au kulia na ishara nyingine.
iii. Watoto watazame ishara hizo kwa makini kisha waseme zinaashiria hisia gani?
iv. Katika jozi, mtoto mmoja aoneshe ishara inayoashiria hisia na mwingine aseme ishara hiyo inaashiria nini.
v. Hakikisha kila mtoto ameshiriki kikamilifu.

**Tafakari**

i. Kati ya ishara ya huzuni na furaha, ipi ilikuwa rahisi kwako kuionesha?
ii. Kati ya ishara ya huzuni na furaha, ipi ilikuwa ngumu kwako kuionesha?

**Husisha**

i. Je umewahi kufurahi? Nini kilikufurahisha?
ii. Je umewahi kukasirika? Nini kilikukasirisha?

**Tumia**

i. Utafanya nini ili mwenzako afurahi?
ii. Je, mwenzako akikutendea jambo baya utafanya nini?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza:

i. kubaini vitendo vinavyosaidia kutawala hisia; na
ii. kuonesha namna ya kutawala hisia.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 34 9/18/19 4:59 PM

**b. Mchezo: Dansi mgando**

Vifaa: Kanda za sauti, radio au kifaa chochote cha kucheza muziki

Hatua za kufuata:

i. Andaa sehemu kubwa na salama kwa watoto ili wacheze kwa uhuru.
ii. Fungulia muziki wowote wenye maadili mema kisha waambie watoto wote wacheze. Hakikisha muziki unasikika.
iii. Wakiwa wanaendelea kucheza, zima muziki kwa ghafla na kila mtoto agande kama alivyo, asiendelee kucheza.
iv. Chunguza tendo la kuganda kwa watoto huku ukiwaambia au kuonesha matendo ya kuchekesha yatakayowafanya watoto wacheke au watikisike.
v. Wale watakaocheka au kutikisika, wataungana na wewe kuwachekesha wengine hadi wote watakapocheka au kutikisika.
vi. Fungulia tena muziki na kuendelea na hatua kama zilezile za mwanzo.

Mwalimu, hakikisha kuwa watoto wote wanacheza, wanaganda na wanacheka. Angalia watoto wasiumizane wakati wa kucheza.

**Tafakari**

i. Je, ulijisikiaje muziki au ngoma ilipositishwa ghafla?
ii. Kitu gani kilikufanya ufurahi na kucheka?
iii. Kitu gani kilikufanya utikisike?

**Husisha**

i. Vitu gani vingine huwa vinakufanya ufurahi?
ii. Vitu gani vingine huwa vinakufanya usikitike?
iii. Huwa unajisikiaje ukikatazwa kwenda kucheza na wenzako?

**Tumia**

Utafanya nini mwezako akikunyang'anya vitu vyako?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kuonesha vitendo vya kuvaa na kuvua nguo;
ii. kufunga na kufungua vifungio;
iii. kula mwenyewe; na
iv. Kufanya usafi binafsi.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kujenga tabia ya kutunza vitu**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja mahali pa kutunzia vitu mbalimbali;
ii. kueleza umuhimu wa kutunza vitu;
iii. kupanga vitu mbalimbali mahali panapostahili; na
iv. kutumia na kurudisha kitu mahali panapostahili.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Mchezo wa ndoo

**Mchezo wa ndoo**

Vifaa: Karatasi, ndoo, makopo, kikapu


Hatua za kufuata:

i. Wapange watoto katika vikundi kutokana na idadi yao darasani.
ii. Weka vipande vya karatasi vyenye rangi tofauti kama vile njano, bluu, nyeupe, kijani, nyekundu katika kasha/kikapu kisha weka kasha/kikapu katikati ya eneo la kuchezea.
iii. Weka ndoo au makopo yaliyobandikwa vipande vya karatasi zenye rangi sawa na zilizotajwa.
iv. Wapange watoto katika mistari kulingana na idadi uliyoigawa kuelekea kwenye kasha/kikapu kama ilivyooneshwa kwenye mchoro.
v. Waeleze watoto namna ya kucheza kuelekea kwenye kikapu au kasha kwa kutembea au kurukaruka au kutambaa au kwa kuruka kama chura.
vi. Mtoto wa kwanza kwenye kila mstari akifika kwenye kikapu au kasha achukue kipande kimoja cha karatasi na kuweka kwenye kopo au ndoo iliyobandikwa rangi inayofanana na karatasi aliyoichukua.
vii. Kila mtoto katika mstari afanye kama mtoto wa kwanza alivyofanya.
viii. Mwalimu angalia kama kila mtoto ameweka rangi inayofanana na ndoo/kopo husika na anatembea kwa mwendo unaopendekezwa.

Angalia kielelezo kifuatacho kwa ufafanuzi wa mchezo huu



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 36 9/18/19 4:59 PM




**Tafakari**

i. Ulipochukua kipande cha karatasi ulikiweka wapi?
ii. Nini kilikuongoza kuweka karatasi katika ndoo/kopo?
iii. Ulitumia mwendo gani kwenda kuweka karatasi kwenye kopo au ndoo?
iv. Uliweza kuchukua karatasi ngapi kuweka kwenye ndoo/kopo?

**Husisha**

i. Ni sehemu gani huwa unaweka begi na sare zako unapotoka shule,?
ii. Je, ulishawahi kutunza vitu vya wenzio? Wapi? Ni vitu gani?

**Tumia**

i. Utafanya nini ukikuta kitu hakiko sehemu yake?
ii. Vitu gani unaweza kusaidia kuvipanga ukiwa nyumbani?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. Kupanga vitu mbalimbali mahali panapostahili; na
ii. Kutumia na kurudisha vitu mahali panapostahili.

**4.2.2 Kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kuwasiliana**

Mawasiliano yanamwezesha mtoto kukua kijamii, kiakili na kihisia. *Je, mwalimu utamwezeshaje mtoto kujenga uwezo wa kuwasiliana?* Pamoja na majibu uliyonayo,



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 37 9/18/19 4:59 PM

hakikisha kuwa unampa mtoto fursa ya kusikiliza na kuzungumza kwa ufasaha.

Katika eneo hili la kuwasiliana, utamwongoza mtoto katika: kusikiliza, kuzungumza, kumudu stadi za awali za kusoma na za kuandika. Pamoja na hayo, unaweza kuwashirikisha watoto katika mambo mengine yatakayowajengea uwezo wa kuwasiliana kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na kwa kutumia michezo ya kuigiza. Pia, watoto wanaweza kutumia vifani vya simu kuwasiliana na kutengeneza mfano wa runinga au redio na kuigiza kama watangazaji pamoja na kuweka magazeti na majarida katika kona ya lugha.

Mwalimu, unatakiwa kutambua kwamba darasa lina mchanganyiko wa watoto wenye mahitaji mbalimbali. Iwapo kuna watoto wenye mahitaji maalum, unapaswa kuwatambua na kuwapa afua stahiki ili waweze kumudu kuwasiliana.

Mwalimu kumbuka kuwa, watoto wanatoka katika mazingira yenye mila na desturi tofauti, hivyo ni muhimu kuzingatia mila na desturi za jamii husika ili kuwawezesha kujenga uwezo wa kuwasiliana. Umahiri huu umejengwa na umahiri mahususi nne kama ifuatavyo:

**4.2.2.1 Kumwezesha mtoto kumudu stadi za kusikiliza**

Mwalimu, ili kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kusikiliza, tumia vitu, mbinu na matendo mbalimbali yanayokuza usikivu. Hakikisha unakuwa mfano bora katika kuwasilikiza watoto na watu wengine. Stadi za kusikiliza zitamwezesha mtoto kujenga utayari katika kujifunza kwake hasa pale atakapohitaji kupata maelezo juu ya utendaji wa shughuli mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kujenga stadi za kusikiliza**

Mtoto mwenye stadi za kusikiliza atakuwa muelewa, makini na mwenye kufuata maelekezo na maagizo yanayotolewa. Pia atakuwa na uwezo mkubwa wa kufanya mawasiliano na kupokea taarifa mbalimbali na kuzifanyia kazi kadri inavyostahili.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Igizo dhima, nyimbo, hadithi, majadiliano, maswali na majibu, michezo na maigizo

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Michoro, picha, redio, runinga, ngoma, filimbi, binyanga, manyanga, kayamba, kanda za video, kinanda na piano

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kubaini vitu vinavyotoa sauti/milio**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitu mbalimbali vinavyotoa sauti/milio;
ii. kusikiliza vitu mbalimbali vinavyotoa sauti/milio;
iii. kubaini sauti/milio mbalimbali waliyosikia katika mazingira yao; na
iv. kufanya vitendo vya kuigiza sauti/milio ya vitu, watu na wanyama.

Michezo inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Mchezo wa sauti/milio ya vitu mbalimbali
b. Askari mnyama
c. Wimbo wa Hii sauti ya nini?

**a. Mchezo: Sauti/milio ya vitu mbalimbali**

Vifaa: Kiti, meza, chuma, kalamu, kopo, kikombe, ndoo, debe, ngoma, vitambaa

Hatua za kufuata:

i. Washirikishe watoto kutaja vitu mbalimbali vinavyotoa milio kama meza, ngoma, ndoo, debe, kopo na vikombe.
ii. Gonga kitu kimojawapo ili kitoe mlio.
iii. Waelekeze watoto kugonga kifaa ulichowaandalia ili waweze kutambua mlio wake.
iv. Wagawe watoto katika vikundi. Mtoto mmoja katika kikundi agonge kitu chochote wakati watoto wengine wamefungwa vitambaa machoni ili waweze kubaini mlio wa kitu hicho.
v. Hakikisha kila mtoto ameshiriki katika mchezo huo.
vi. Mchezo utamalizika utakapoona inafaa.

**Tafakari**

i. Uligonga kitu/kifaa gani?
ii. Ulisikia nini wakati kifaa kinagongwa? Mlio gani?
iii. Ni mlio wa kitu gani umeupenda zaidi?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 39 9/18/19 4:59 PM

**Husisha**

i. Vitu gani hapa darasani vinatoa mlio vikigongwa?
ii. Vitu gani nyumbani vinatoa mlio vikigongwa?
iii. Mlio gani unapenda kuusikia?
iv. Mlio gani mwingine ulishawahi kusikia?

**Tumia**

Tunawezaje kutumia milio katika kazi mbalimbali?

**b. Mchezo: Askari mnyama**

Vifaa: Picha za wanyama mbalimbali, kitambaa, fimbo

Hatua za kufuata:


i. Wagawe watoto katika vikundi kwa idadi utakayoona inafaa.
ii. Waelekeze watoto kwenye kila kikundi waunde duara.
iii. Eleza kuwa, mchezo huu unahitaji kila mmoja kwenye kikundi kujua jina la mwenzake na sauti yake.
iv. Waelekeze watoto waigize sauti za wanyama kama vile paka, ng'ombe, mbuzi, mbwa na wengine.
v. Mwambie mtoto mmoja katika kila kikundi ajitolee kucheza nafasi ya Askari mnyama.
vi. Mpe Askari mnyama kitambaa au kitu chochote cha kufunga macho na fimbo ya kushika. Mwambie Askari mnyama asimame katikati ya duara.
vii. Eleza na onesha kuwa
    - Watoto katika mduara watazunguka kwa mwelekeo wa mshale wa saa.
    - Askari mnyama akipiga fimbo yake chini mara tatu, watoto watasimama, watageuka na kumtazama.
    - Askari mnyama atanyoosha fimbo yake na mtoto aliye karibu atashika fimbo.
    - Mtoto aliyeshika fimbo atatoa sauti ya mnyama fulani.
    - Askari mnyama atajaribu kuotea mnyama gani anaigizwa na mtoto yupi ameshika fimbo.
    - Askari mnyama atakuwa na nafasi tatu za kuotea. Akipatia, mtoto aliyeshika fimbo atakuwa Askari mnyama.

viii. Mchezo utaendelea hadi watoto wote watakapokuwa wameshiriki kikamilifu.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 40 9/18/19 4:59 PM

Angalia kielelezo kifuatacho kwa ufafanuzi zaidi wa mchezo.




**Tafakari**

i. Ni sauti zipi za wanyama zilizowafurahisha zaidi? Kwa nini?
ii. Ulijisikiaje kutoa sauti ya mnyama uliyemchagua? Kwa nini?

**Husisha**

Ni sauti za wanyama gani ulishawahi kuzisikia? Ulizisikia wapi?

**Tumia**

Kwa nini ni vizuri kujua sauti za wanyama mbalimbali?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuchunguza kama kila mtoto ameweza kubaini vitu mbalimbali vinavyotoa sauti/mlio.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kusikiliza nyimbo, mazungumzo na hadithi fupi**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kusikiliza nyimbo, kutaja wahusika na kuelezea ujumbe wa wimbo waliousikiliza;
ii. kusikiliza mazungumzo, kutaja wahusika na kuelezea ujumbe kutokana na mazungumzo; na
iii. kusikiliza hadithi, kutaja wahusika na kuelezea ujumbe wa hadithi walizosikiliza.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 41 9/18/19 4:59 PM

Nyimbo na hadithi zinazopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Hii ni sauti ya nini
b. Mabata madogodogo
c. Hadithi

**a. Wimbo: Hii ni sauti ya nini?**

*Moooo, mooo*
*Hii ni sauti ya nini, sauti ya ng'ombe*
*Ng'ombe ng'ombe ni rafiki yetu anatupa maziwa*
*Meee, meee*
*Hii ni sauti ya nini, sauti ya mbuzi*
*Mbuzi mbuzi ni rafiki yetu anatupa nyama*
*Kokokooo koo*
*Hii ni sauti ya nini, sauti ya kuku*
*Kuku kuku ni rafiki yetu anatupa mayai*
*Beee beee*
*Hii ni sauti ya nini, sauti ya kondoo*
*Kondoo kondoo, ni rafiki yetu anatupa nyama*

Hatua za kufuata:

i. Waongoze watoto kukaa katika nusu duara.
ii. Tambulisha wimbo kwa watoto namna unavyoimbwa.
iii. Mchague mtoto mmoja awe mwanzilishi wa wimbo.
iv. Waongoze watoto kuimba huku wakimsikiliza mwongozaji kwa makini.

**Tafakari**

i. Igiza sauti za wanyama uliowasikia kwenye wimbo.
ii. Ng'ombe anatupatia nini?

**Husisha**

Igiza sauti za wanyama wengine unaowafahamu.

**Tumia**

i. Je, utaweza kutofautisha sauti za wanyama mbalimbali utakapozisikia?
ii. Je, ni wakati gani utaweza kuigiza sauti za wanyama?

**b. Wimbo: Mabata madogodogo**

Hatua za kufuata:

i. Waongoze watoto kusimama wakiwa ndani au nje ya darasa.
ii. Anza kwa kuwaimbia wimbo kwa sauti kisha nao wafuatishe.

iii. Imba tena kwa kuonesha matendo nao wafuatishe kuimba.

*Mabata madogodogo yanaogelea, yanaogelea*
*Katika shamba zuri la bustani,*
*katika shamba zuri la bustani x2*
*Yanapenda kutembea bila viatu*
*bila viatu katika shamba zuri la bustani,*
*katika shamba zuri la bustani x2.*
*Yanapenda kulia*
*kwa, kwa, kwa, kwa, kwa, kwa,*
*kwa, kwa, kwa, kwa, kwa, kwa*
*kwa, kwa, kwa, kwa, kwa, kwa,*
*kwa, kwa, kwa, kwa, kwa kwaaaaaa.*
*katika shamba zuri la bustaniiiiii x2.*

iv. Angalia kama watoto wanaimba kwa sauti na kufanya matendo yanayoendana na wimbo.

v. Endelea kufuatilia wanavyoimba hadi mwisho wa wimbo.

**Tafakari**

i. Bata walikuwa wanafanya nini bustanini?
ii. Je, bata walikuwa wanaliaje?

**Husisha**

i. Wewe huwa unaliaje?
ii. Ni kitu gani kingine ulichowahi kukisikiliza?

**Tumia**

i. Kwa nini ni vizuri kumsikiliza mtu akiwa anazungumza?
ii. Je, tusipo vaa viatu tutapata madhara gani?

**c. Hadithi**

Vifaa: Kitabu cha hadithi

Soma hadithi ifuatayo na kuilewa. Hadithi hii imetolewa kama mfano tu

**Kijiji cha Mwendokasi**

*Katika kijiji cha Mwendokasi kulikuwa na mtoto mmoja aitwaye Dino. Mtoto huyo alikuwa akiishi na bibi yake katika nyumba ya nyasi. Kila mara Dino hakupenda kunawa mikono. Siku moja bibi yake Dino alipika nyama.*

*Nyama ilipoiva bibi alipakua katika sahani mbili. Dino alichukua sahani yake,*



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 43 9/18/19 4:59 PM

*akaanza kula. Alipomaliza kula hakunawa mikono. Usiku huo panya alitoka juu ya dari, akaingia katika blanketi na kumng'ata Dino vidole. Dino alilia sana. Bibi yake aliamka kwenda kumuangalia. Alikuta vidole vya Dino vinatoka damu. Akasema, "Pole mjukuu wangu". Unatakiwa unawe mikono mara baada ya kula. Tangu siku ile, Dino akaanza kunawa mikono baada ya kula.*

Hatua za kufuata:

i. Wasimulie watoto hadithi
ii. Mpe nafasi mtoto yeyote katika darasa asimulie hadithi.
iii. Watoto wengine wasikilize hadithi inayosimuliwa na mwenzao.
iv. Kwa watoto ambao watakuwa wanaishiwa maneno wakati wa kusimulia, wahamasishe kwa kuwauliza maswali ya kuwaongoza ili wamalizie hadithi yao.
v. Hakikisha idadi kubwa ya watoto wameshiriki.

**Tafakari**

i. Kwa nini Dino aling'atwa na panya kwenye vidole?
ii. Kwa nini umechagua hadithi uliyosimulia?
iii. Hadithi uliyosimulia ulifundishwa na nani?
iv. Umejifunza nini kutokana na hadithi uliyoisikia?

**Husisha**

Je, ulishawahi kusimuliwa hadithi? Kama ndiyo, hadithi hiyo ilihusu nini?

**Tumia**

Utakaporudi nyumbani, nani ungependa umsimulie hadithi? Utamsimulia hadithi gani?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuchunguza kama kila mtoto ameweza kusikiliza na kuelezea ujumbe aliousikia katika nyimbo, mazungumzo na hadithi fupi.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kujenga uwezo wa kusikiliza maelekezo/ maagizo**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kusikiliza maelekezo na kutenda ipasavyo;
ii. kupokea maagizo na kutenda ipasavyo; na
iii. kutaja maelekezo au maagizo anayopewa mara kwa mara katika mazingira yake.

Michezo na nyimbo zinazopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 44 9/18/19 4:59 PM

a. Nenda, polepole, simama
b. Kuongoza mtu asiyeona
c. Wimbo wa simama kaa

**a. Mchezo: Nenda, polepole, simama**

Vifaa: Kadi zenye rangi ya njano, kijani na nyekundu

Hatua za kufuata:

i. Weka alama ya mipaka katika eneo la kuchezea ili kuruhusu watoto kukimbia na kukimbizana.
ii. Waelekeze watoto kutafuta nafasi katika eneo hilo na wakutazame.
iii. Waambie kuwa, wataigiza kuendesha pikipiki, baiskeli au gari.
iv. Elekeza kwamba mchezo huu una amri tatu za kuzingatia ambazo ni:
    - Unaposema NENDA watoto wazunguke kwa kasi katika eneo la kuchezea wakijifanya kuendesha vyombo vya usafiri.
    - Unaposema POLEPOLE, watoto waigize kuendesha polepole vyombo vyao vya usafiri.
    - Unaposema SIMAMA, watoto wasimame na kuganda bila kutikisika mpaka watakaposikia amri ya NENDA au POLEPOLE kwa mara nyingine.
v. Waelekeze watoto kutumia kadi yenye rangi husika kwa kuonesha (nyekundu simama, njano-polepole na kijani-nenda) pale unapotoa amri.
vi. Toa amri hizo kila baada ya sekunde kadhaa na kuangalia kama watoto wanafuata maelekezo yako.

**Tafakari**

i. Ni maelekezo gani yalitolewa wakati wa mchezo?
ii. Je, uliweza kufuata maelekezo yote?

**Husisha**

i. Ulishawahi kupewa maelekezo? Uliambiwa ufanye nini?
ii. Ni sehemu gani nyingine huwa tunapewa maelekezo?

**Tumia**

i. Unatakiwa ufanye nini ukipewa maelekezo?
ii. Kufuata maelekezo kutakusaidia nini?

**b. Mchezo: Kuongoza mtu asiyeona**

Vifaa: Kitambaa, ngoma/filimbi



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 45 9/18/19 4:59 PM

Hatua za kufuata:

i. Watoe watoto nje ya darasa.
ii. Wapange watoto katika duara kubwa.
iii. Mfunge mtoto mmojawapo kitambaa machoni.
iv. Simama katikati ya duara na upige makofi au ngoma ili mtoto aliyefungwa kitambaa akufuate na kukugusa akizingatia upande itokapo sauti/mlio huo.
v. Hamia eneo lingine mara mtoto anapokaribia kukugusa. Piga tena ngoma au makofi au filimbi mpaka atakapofanikiwa kukugusa.
vi. Mchague mtoto mwingine na mfunge kitambaa, kisha mteue mtoto mwingine badala yako atakayepiga ngoma, makofi au filimbi sehemu tofauti katika duara na mtoto aliyefungwa kitambaa amfuate.

**Tafakari**

i. Nini kilikuongoza kumgusa mwenzako ulipokuwa umefungwa kitambaa?
ii. Ni ugumu gani uliupata wakati wa kuufuata mlio wa ngoma au makofi?

**Husisha**

i. Kengele ya shule ikigongwa unatakiwa kufanya nini?
ii. Ni shughuli gani nyingine umewahi kuifanya kwa kufuata maelekezo? Ilikuwaje?

**Tumia**

i. Kwa nini ni vizuri kufuata maelekezo unayopewa?
ii. Utakapopewa maelekezo utafanya nini?

**c. Wimbo: Simama kaa**

Hatua za kufuata:

i. Imbisha wimbo huu na watoto wafuatilie bila matendo kwa mara ya kwanza.
ii. Waelekeze watoto kufanya matendo yanayoendana na wimbo wanaoimba.
iii. Angalia kama watoto wanatenda vitendo kulingana na wimbo.

*Simama kaa, simama kaa*
*Ruka, ruka, ruka, simama kaa*
*Tembea tembea, kimbia, kimbia x 2*
*Ruka, ruka, ruka, simama, kaa*

**Tafakari**

i. Ulielekezwa kutenda vitendo gani wakati unaimba?
ii. Ni nini kilikuongoza kutenda vitendo hivyo?

**Husisha**

i. Ni vitendo gani vingine unavyoweza kuvitenda?.
ii. Ni wakati gani mwingine huwa unafuata maelekezo?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 46 9/18/19 4:59 PM

**Tumia**

i. Kwa nini ni muhimu kufuata maelekezo?
ii. Utamsaidiaje mtoto mwenzako asiyependa kufuata maelekezo?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kufuata maelekezo na maagizo kwa usahihi na kutenda ipasavyo.

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kucheza mchezo wa kupashana habari**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja michezo ya kupashana habari wanayoijua;
ii. kusikiliza na kupashana habari iliyotolewa;
iii. kueleza ujumbe wa habari iliyotolewa; na
iv. kufanya vitendo vya kupashana habari kwa mambo yanayojitokeza nyumbani na shuleni.

Michezo inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Simu iliyovunjika
b. Mchezo wa simu

**a. Mchezo: Simu iliyovunjika**

Hatua za kufuata:

i. Wagawe watoto katika vikundi vya watoto kumi kumi.
ii. Wapange katika mstari mnyoofu.
iii. Mpe mtoto wa kwanza katika mstari ujumbe ambao atamnong'oneza jirani yake, na jirani atafanya hivyo hivyo kwa anayemfuata mpaka kwa mtoto wa mwisho katika mstari.
iv. Mtoto wa mwisho aseme ujumbe uliomfikia kwa sauti.
v. Mtoto wa kwanza aulizwe kama ujumbe uliotolewa na mtoto wa mwisho ni sawa na ule alioutoa yeye.

**Tafakari**

i. Je, ujumbe alioutoa mtoto wa kwanza ni sawa na alioupokea mtoto wa mwisho? Kama siyo,unafikiri ni kwa nini ujumbe umebadilika?
ii. Nini kingefanyika ili ujumbe ufike kwa usahihi?
iii. Ulifanya nini kufikisha ujumbe uliopewa kwa usahihi?

**Husisha**

Ni aina gani nyingine ya kupeleka taarifa unayoijua?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 47 9/18/19 4:59 PM

**Tumia**

i. Nini kitatokea usiposikiliza ujumbe kwa makini?
ii. Je, utafanya nini ili ufikishe ujumbe kwa usahihi?

**b. Mchezo: Mchezo wa simu**

Vifaa: Makopo, waya, uzi

Hatua za kufuata:

i. Tengeneza simu rahisi nne (4) au zaidi kwa kutumia makopo mawili yaliyounganishwa na waya au uzi wenye urefu wa mita moja.
ii. Chagua mtoto mmoja na uwasiliane naye kwa kutumia simu uliyotengeneza
iii. Wapange watoto katika jozi.
iv. Wape watoto simu wawasiliane kwa namna wanavyopenda.
v. Hakikisha idadi kubwa ya watoto wameweza kushiriki.

**Tafakari**

i. Je, umefurahia kuwasiliana na mwenzako kwa kutumia simu? Kwa nini?
ii. Uliongea nini na rafiki yako kwenye simu?

**Husisha**

i. Je, ulishawahi kuongea kwa simu na mtu mwingine?
ii. Ukirudi nyumbani huwa unamweleza nani habari za shule?

**Tumia**

Utatumia njia gani kupeleka ujumbe kwa mtu mwingine?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuchunguza kama kila mtoto ameweza kutoa/kupokea ujumbe uliokusudiwa kwa usahihi.

### 4.2.2.2 Kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kuzungumza

Kuzungumza ni sehemu muhimu ya kukuza uwezo wa kuwasiliana kwa mtu yeyote. Ili mtoto aweze kujenga stadi za kuzungumza, mwalimu huna budi kumpa fursa ya kuzungumza. Katika sehemu hii, mwalimu utamwezesha mtoto kuwa na urazini wa kutumia mazingira yake kwa kufanya vitendo mbalimbali vitakavyomwezesha kuzungumza kwa ufasaha ikiwemo kusalimiana, kutambulisha, kuimba, kujadiliana na kusimulia hadithi. Vilevile, unapaswa kumpa mtoto fursa ya kueleza vitu anavyovipenda na asivyovipenda.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 48 9/18/19 4:59 PM

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kuzungumza kwa ufasaha**

Hii ni stadi mojawapo ya lugha inayomwezesha mtoto kujenga uwezo wa kuwasiliana, kuhusiana, kujiamini na kujifunza kwa urahisi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Igizo dhima, nyimbo, hadithi, majadiliano, maswali na majibu, michezo, maigizo, midahalo na vitendawili. Mwalimu, unapaswa kuzingatia uwezo na uzoefu wa watoto katika kutega na kutegua vitendawili. Ni vema kutumia mazingira ya watoto na vitu walivyozoea kuviona na kuvisikia.

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Michoro, picha, simu, vitabu vya hadithi, runinga na kanda za video

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kufanya majadiliano/mazungumzo**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja mambo ya kuzingatia wakati wa kufanya majadiliano/mazungumzo;
ii. kufanya majadiliano/mazungumzo; na
iii. kucheza michezo ya kujibishana.

Michezo inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Rafiki kama mimi
b. Kadi za picha

**a. Mchezo: Rafiki kama mimi**

Hatua za kufuata:

i. Waelekeze watoto wasimame katika duara.
ii. Waelekeze wataje vitu ambavyo wanavipenda au kuvitenda na vinapendwa au kutendwa na watoto wengine.
iii. Mchezo utaanza kwa mtoto mmoja kusimama katikati ya duara na kutaja sifa au jambo lolote linalomhusu na analolipenda. Kwa mfano, "Nimevaa viatu vyeusi", "Ninapenda kula barafu", "Ninapenda kunywa maziwa", "Naipenda shule yangu" na kadhalika.
iv. Watoto wenye sifa au wanaopenda jambo hilo watahama kwa kubadilishana nafasi zao katika duara.
v. Toa mifano minne hadi mitano ili kujiridhisha kama watoto wanahamia kwenye nafasi nyingine ambazo sentensi zilizosemwa zinafanana na vitu au matendo wanayoyapenda.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 49 9/18/19 4:59 PM

vi. Watoto wanapouelewa mchezo vizuri, chagua mtoto mwingine asimame katikati ili kuendeleza mchezo kwa kufuata hatua zake.
vii. Chagua mtoto mwingine kila mara ili kutoa nafasi kwa watoto wengi zaidi kushiriki kulingana na muda unavyoruhusu. Wahamasishe watoto kutoa sentensi mpya kila mara wanapopata nafasi.
viii. Mchezo unamalizika pale idadi kubwa ya watoto au watoto wote watakapokuwa wameshiriki kwenye mchezo.

**Tafakari**

i. Ni vitu gani vilivyotajwa ambavyo unavipenda? Kwa nini?
ii. Ni matendo gani yaliyotajwa ambayo huyapendi? Kwa nini?

**Husisha**

i. Umeshawahi kuona watoto wengine wanaopenda vitu kama mlivyovitaja?
ii. Vitu hivyo vina sifa gani?

**Tumia**

i. Ni vitu gani unapenda kuwa navyo ukiwa mkubwa? Kwa nini?
ii. Ukitaka kitu unachokipenda utafanya nini?

## b. Mchezo: Kadi za picha

Vifaa: Kadi za picha na michoro

Hatua za kufuata:

i. Andaa kadi za picha kulingana na mazingira uliyopo na kujadili na watoto.
ii. Waelekeze watoto wakae katika makundi ya watoto 5 hadi 6, kisha gawa kadi ya picha kwa kila mtoto katika kikundi.
iii. Toa mfano wa namna ya kuelezea picha, (mfano picha ya paka utasema, nina picha ya paka, paka wangu ana miguu minne, ana macho mawili, ana masikio mawili, ana mkia mmoja, rangi yake ni nyeupe, nampenda paka huyu) Toa nafasi ya watoto katika kikundi kuoneshana picha na kuzijadili.
iv. Chagua baadhi ya watoto katika kila kikundi kuelezea picha walizo nazo.
v. Kwa mtoto atakayeshindwa kuielezea picha yake vizuri, toa nafasi kwa mtoto mwingine amsaidie kuielezea na kisha mtoto aliyeshindwa arudie maelezo.
vi. Mchezo utamalizika utakapoona inafaa.

**Tafakari**

i. Picha uliyoichagua ilikuwa na sifa zipi?
ii. Je, ilikuwa rahisi au vigumu kuielewa picha? Kwa nini?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 50 9/18/19 4:59 PM

**Husisha**

i. Picha ulizojadili ulishawahi kuziona sehemu nyingine? Elezea
ii. Umewahi kuona vitu/wanyama wanaofanana na picha ulizoziona? Wana sifa zipi?

**Tumia**

Endapo utapoteza kitu chako utamfahamishaje mtu mwingine?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza:

i. kutumia lugha kwa usahihi;
ii. kutamka maneno kwa usahihi; na
iii. kucheza kwa kujibishana.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kutega na kutegua vitendawili**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitendawili wanavyovifahamu;
ii. kutega vitendawili wanavyovifahamu; na
iii. kutegua vitendawili vilivyotegwa.

Wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Wimbo wa vitendawili

**Wimbo: Wimbo wa vitendawili**

Hatua za kufuata:

i. Andaa picha mbalimbali zinazohusisha vitendawili ulivyopanga kutegua na watoto.
ii. Waulize watoto kama wanafahamu vitendawili.
iii. Chagua watoto wawili au watatu wategе vitendawili kisha watoto wengine wategue.
iv. Kwa kutumia picha ulizoandaa waongoze watoto kutegua vitendawili. Kwa mfano: Waonyeshe picha ya kibiriti na utege kitendawili.
v. Endelea kufanya hivyo hadi utakapoona inafaa.

*Watoto kitendawili, tega*

*Watoto kitendawili, tega*

*Nyumba yangu ina watoto wengi = kiberiti*

*Kuku wangu katagia mibani = nanasi*

*Nina nyumba yangu ina nguzo moja = uyoga*

*Mlinzi mfupi kasimama mlangoni = kufuli*

*Mzungu katoka kwao na mkono mmoja = kikombe*



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 51 9/18/19 4:59 PM

**Tafakari**

i. Wimbo tulioimba unahusu nini?
ii. Ni vitendawili gani tumevitaja katika wimbo?

**Husisha**

i. Umewahi kusikia vitendawili vingine? vitaje
ii. Vitendawili gani vingine unavifahamu?

**Tumia**

i. Ni nani utaenda kumtegea vitendawili ulivyojifunza leo?
ii. Tega kitendawili chochote.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kutega na kutegua vitendawili.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kuimba nyimbo mbalimbali**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja nyimbo wanazozifahamu;
ii. kuimba nyimbo wanazozipenda na kueleza ujumbe ulio katika wimbo; na
iii. kuimba wimbo na kutenda matendo yanayohusiana na wimbo huo.

Nyimbo zinazopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Wimbo wa maua mazuri
b. Wimbo wa simama kaa

**a. Wimbo: Maua mazuri**

*Maua mazuri yapendeza x2*
*Ukiyatazama yanameremeeta,*
*hakuna mmoja asiyeyapenda*
*Zuum zuum zuum we mama nyuki lia weee*
*Toka mbali kutafuta ua zuri kwa chakula*
*Zuum zuum zuum*
*we mama nyuki lia weee*

Hatua za kufuata:

i. Anza kwa kuimba wimbo wakati watoto wanakusikiliza.
ii. Waongoze watoto kuimba wimbo mstari baada ya mstari.
iii. Waongoze watoto kuimba wimbo wote.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 52 9/18/19 4:59 PM

**Tafakari**

Kuna kitu kilichokufurahisha katika wimbo huu? Kwa nini?

**Husisha**

i. Je, ulishawahi kuona maua mahali popote? Yalikuwa na rangi gani?
ii. Ni nyimbo gani nyingine unazozifahamu? Zinaimbwaje? Ulizisikia wapi?

**Tumia**

i. Ungependa kumfundisha nani wimbo huu?
ii. Nyimbo gani nyingine utapenda kujifunza?

**b. Wimbo: Simama kaa**

*Simama kaa, simama kaa*
*Ruka, ruka, ruka, simama kaa*
*Tembea tembea, kimbia, kimbia x 2*
*Ruka, ruka, ruka, simama, kaa*

Hatua za kufuata:

i. Anza kuimba huku ukifanya vitendo na watoto wakisikiliza na kukutazama.
ii. Waongoze watoto kuimba wimbo huo kwa kuonyesha matendo.

**Tafakari**

i. Ulielekezwa kutenda vitendo gani wakati unaimba?
ii. Ni nini kilikuongoza kutenda vitendo hivyo?

**Husisha**

i. Ni vitendo gani vingine unavyoweza kuvitenda?.
ii. Ni wakati gani mwingine huwa unafuata maelekezo?

**Tumia**

i. Kwa nini ni muhimu kufuata maelekezo?
ii. Utamsaidiaje mtoto mwenzako asiyependa kufuata maelekezo?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kutamka maneno kwa usahihi katika wimbo;
ii. kuimba nyimbo; na
iii. kuelezea ujumbe wa wimbo ulioimbwa.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 53 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kusimulia hadithi mbalimbali**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja hadithi wanazozifahamu;
ii. kusimulia hadithi na kutaja wahusika waliojitokeza kwenye hadithi iliyosimuliwa;
iii. kuelezea ujumbe wa hadithi uliyosimuliwa; na
iv. kuigiza matendo katika hadithi iliyosimuliwa.

Mbinu inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Hadithi.

**Hadithi**

Vifaa: Vitabu vya hadithi

Hatua za kufuata:

i. Wasimulie wototo hadithi moja.
ii. Waongoze watoto wasimulie hadithi mbalimbali.

**Tafakari**

i. Hadithi yako inatufundisha nini?
ii. Ni nani wametajwa kwenye hadithi?

**Husisha**

i. Je, ulishawahi kusimulia hadithi kabla? ilihusu nini?.
ii. Tunaposimuliwa hadithi tunatakiwa tufanye nini?

**Tumia**

Ni mahali gani pengine unaweza kusimulia hadithi?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza:

i. kusimulia hadithi; na
ii. kuelezea ujumbe wa hadithi iliyosimuliwa.

**Shughuli ya 5: Kuwawezesha watoto kuelezea shughuli za kila siku**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja shughuli wanazozifanya kila siku nyumbani;
ii. kueleza shughuli wanazozifanya kila siku shuleni; na
iii. kuigiza shughuli wanazozifanya katika mazingira yao.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Kadi za picha



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 54 9/18/19 4:59 PM

**Mchezo: Kadi za picha**

Vifaa: Kadi zenye picha au michoro

Hatua za kufuata:

i. Chora au kusanya picha zenye matukio au shughuli za kawaida anazofanya mtoto kuanzia asubuhi mpaka jioni kwa mtiririko ufuatao:
   - Anapiga mswaki.
   - Ananawa uso.
   - Amevaa sare za shule, amebeba begi na anaelekea shuleni.
   - Anafagia uwanja wa shule.
   - Amekaa darasani anasoma.
   - Amerudi nyumbani na kubadilisha sare za shule.
   - Picha ya jua kuonesha muda mfano, asubuhi na mapema, saa sita mchana na jioni.

ii. Gawa watoto katika vikundi na gawia kila kikundi picha zote saba zinazoonesha mtiririko wa matukio kuanzia tukio la kwanza hadi la mwisho, kisha waoanishe na picha za jua zinazoashiria muda.

iii. Hakikisha kila kundi limeweza kupanga picha kwa usahihi.

**Tafakari**

Ni matukio gani umeyaona kwenye picha?

**Husisha**

i. Ni shughuli gani nyingine unazozifanya ukiwa nyumbani?
ii. Ni shughuli gani nyingine unazozifanya ukiwa shuleni?

**Tumia**

Ni shughuli gani ulikuwa hauifanyi kabla, ambayo utaanza kuifanya baada ya mchezo huu?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kueleza shughuli anazofanya kila siku.

**Shughuli ya 6: Kuwawezesha watoto kueleza vitu wanavyovipenda na wasivyovipenda**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitu vilivyopo kwenye mazingira yao;
ii. kueleza vitu wanavyovipenda na sababu za kupenda vitu hivyo; na
iii. kueleza vitu wasivyovipenda na sababu ya kutovipenda vitu hivyo.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 55 9/18/19 4:59 PM

Michezo inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Napenda
b. Kipi unachokipenda

**a. Mchezo: Napenda**

Vifaa: Mpira

Hatua za kufuata:

i. Gawa watoto katika vikundi vya watoto sita hadi nane (6-8) na kila kikundi kisimame katika duara.
ii. Mpe mtoto mmoja mpira katika kila kikundi.
iii. Mtoto mwenye mpira atauviringisha chini kwenda kwa mtoto mwingine katika duara.
iv. Mtoto aliyeviringisha mpira atasema sifa au jambo analolipenda au asilolipenda kuhusiana na mtoto aliyempelekea mpira. Mfano, "Nampenda Ali kwa sababu tunacheza pamoja", "Nampenda Mary kwa sababu ni mcheshi", "Napenda kucheza kwa sababu nacheza na wenzangu", "Napenda jinsi Mwinuka anavyocheka" "Sipendi tabia ya John kwa sababu ni mchoyo".
v. Mchezo unamalizika utakapoona inafaa.

**Tafakari**

i. Ni kitu gani kilichotajwa katika mchezo ambacho kimekufurahisha? Kwa nini?
ii. Ni kitu gani kilichotajwa katika mchezo ambacho hakikukufurahisha? Kwa nini?

**Husisha**

i. Ni vitu gani vingine ambavyo havikutajwa hapa na unavipenda?
ii. Ni vitu gani vingine ambavyo havikutajwa hapa na huvipendi?

**Tumia**

Utafanya nini ikiwa rafiki yako ana tabia usiyoipenda?

**b. Mchezo: Kipi unachokipenda?**

Hatua za kufuata:

i. Waelekeze watoto wajipange katika eneo la kuchezea wakiachiana nafasi yenye urefu wa mkono mmoja kutoka kwa mtoto mmoja mpaka kwa mwingine.
ii. Waelekeze wataje na kuigiza baadhi ya vitu wanavyovipenda.
iii. Waambie kwenye mchezo huu watazunguka katika eneo la kuchezea wakiigiza vitu/mambo wanayoyapenda.
iv. Kila baada ya sekunde 30 – 45 utataja kitu/kitendo ambacho watoto watatakiwa kukiigiza (mfano: kucheza mpira, kuruka kamba, kuimba, kucheza muziki, kupiga makofi, kunywa maziwa, kusoma, kula chungwa, kunywa juisi, kusaidia wazazi na kufanya usafi).



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 56 9/18/19 4:59 PM

v. Kila mtoto ataigiza kitu au kitendo kilichotajwa na wakati wowote utauliza, "Kipi unachokipenda?" na watoto watarudia kuigiza vitu au vitendo wanayovipenda zaidi.
vi. Wanaweza kubadili vitu au vitendo wanavyopenda wakati wowote wa mchezo unapouliza, "Kipi unachokipenda" ili kuwa na vitu vingi zaidi.
vii. Mchezo utamalizika pale utakapoona inafaa.

**Tafakari**

i. Ni vitu gani unavyovipenda vimetajwa katika mchezo huu?
ii. Ni vitu gani usivyovipenda vimetajwa katika mchezo huu?

**Husisha**

i. Ni vitu gani vilivyotajwa huwa unavifanya mara kwa mara?
ii. Ni vitu gani vingine huwa unapenda kuvifanya ukiwa na wenzako?

**Tumia**

Ni vitu gani unavyovipenda ambavyo utawashirikisha rafiki zako?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kuelezea vitu anavyovipenda na asivyovipenda na sababu zake.

### 4.2.2.3 Kumwezesha mtoto kumudu stadi za awali za kusoma

Hizi ni stadi ambazo mtoto anatakiwa kuzijenga kabla ya kuanza kusoma rasmi. Stadi hizi zinamwezesha kujenga uwezo wa kuwasiliana katika mambo mbalimbali. *Je, mwalimu utamwezeshaje mtoto kumudu stadi za awali za kusoma?* Pamoja na majibu uliyonayo, shughuli zifuatazo zitamjengea mtoto stadi za awali za kusoma: kupata fursa ya kuangalia picha mbalimbali, kuangalia machapisho, kutamka sauti za mwanzo za majina ya watu au vitu, kutaja majina ya vitu vyenye sauti za mwanzo zinazofanana na kutamka sauti za herufi za irabu na konsonanti.

Mwalimu, kumbuka kuwa herufi za konsonanti zimegawanyika katika makundi matatu ambayo ni (b, m, k, d, n), (l, t, p, s, f, j) na (g, y, z, h, r, w, v, ch). Hivyo unapaswa kuzifundisha kwa kuzingatia mtiririko wa makundi hayo.

**Umuhimu wa kumudu stadi za kusoma**

Stadi za awali za kusoma zitamsaidia mtoto kujifunza kusoma kwa kufuata hatua stahiki.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 57 9/18/19 4:59 PM

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Onesho mbinu, kisa mafunzo, michezo, kazi mradi, uchunguzi, hadithi, ziara za mafunzo na nyimbo

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Kadi na chati za irabu (a, e, i, o, u) na konsonanti (b,m,k,d,n) (l, t, p, s, f, g, y, v, h, r, w, ch, j, z), vitabu mbalimbali, magazeti na majarida pamoja na picha za vitu ambavyo majina yake yanaanza na irabu au konsonanti

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kusoma picha**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kukusanya picha mbalimbali;
ii. kuchagua picha wanazozipenda;
iii. kusoma picha walizozichagua kwa hisia;
iv. kuelezea picha walizozichagua; na
v. kuchora picha.

Wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Wimbo wa Hii ni picha ya nini?

**Wimbo: Hii ni picha ya nini?**

Vifaa: Picha kadi zenye picha za vitu na wanyama mbalimbali

*Hii ni picha ya nini, ni picha ya ng'ombe*
*Ng'ombe ng'ombe ni rafiki yetu anatupa maziwa*
*Hii ni picha ya nini, ni picha ya kiti*
*Kiti kiti kina faida kwetu tunakikalia*
*Hii ni picha ya nini, picha ya mbuzi*
*Mbuzi mbuzi ni rafiki yetu anatupa nyama*
*Hii ni picha ya nini, picha ya kuku*
*Kuku kuku ni rafiki yetu anatupa mayai*
*Beee beee*
*Hii ni picha ya nini, picha ya kondoo*
*Kondoo kondoo, ni rafiki yetu anatupa nyama*
*Hii hii ni picha ya nini*
*Ni picha ya nyumba*
*Nyumba nyumba ina faida kwetu, inatusitiri*



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 58 9/18/19 4:59 PM

**Tafakari**

i. Onesha picha za wanyama uliowasikia kwenye wimbo.
ii. Ng'ombe anatupatia nini?
iii. Nyumba ina faida gani kwetu?

**Husisha**

i. Ni vitu gani vingine unavifahamu?
ii. Je, ulishawahi kuona mbolea? ilikua mbolea ya nini?

**Tumia**

i. Je, utaweza kutofautisha picha za wanyama na vitu mbalimbali ukionyeshwa?
ii. Ni picha gani utapenda kuichora na kuionesha kwa wazazi wako?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kusoma picha kwa hisia;
ii. kuelezea picha aliyoichagua; na
iii. kuonesha hisia wakati wa kusoma picha.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kubainisha majina ya vitu mbalimbali katika mazingira**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja majina ya vitu mbalimbali wanavyovifahamu;
ii. kutaja majina ya vitu wanavyoviona katika mazingira yanayowazunguka; na
iii. kutaja majina ya vitu katika makundi.

Michezo inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Nachunguza kwa macho yangu
b. Kama vile

**a. Mchezo: Nachunguza kwa macho yangu**

Vifaa mfano: Mawe, majani, mafuta, maji, matunda

Hatua za kufuata:

i. Andaa eneo la watoto la kuchezea, hakikisha ni salama.
ii. Chunguza vitu mbalimbali vilivyopo kwenye mazingira yako kisha visambaze kwenye jamvi au mkeka.
iii. Wapeleke watoto uwanjani. Inaweza pia kuwa ndani ya darasa.
iv. Waambie watoto kuwa, "Kwa kutumia macho yako mawili unaona kitu gani ambacho sauti yake ya mwanzo inaanza na "m""?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 59 9/18/19 4:59 PM

v. Watoto wafikirie kitu hicho na kwenda kukigusa kisha kutaja jina kamili la kitu hicho.
vi. Baada ya kutaja vitu vitatu au vinne, chagua mtoto mmoja aongoze wenzake kuchunguza vitu kwa kutumia macho, kisha wenzake waguse na kutaja jina la kitu hicho.
vii. Hakikisha watoto wengi wameshiriki katika zoezi la kuchunguza vitu mbalimbali.

**Tafakari**

i. Je, umependa kitu gani katika mchezo huo?
ii. Taja majina ya vitu ulivyoviona leo

**Husisha**

i. Je, ni vitu gani vingine havikutajwa katika mchezo?
ii. Ni vitu gani vingine unavyovifahamu majina yake ambavyo havipo hapa?

**Tumia**

i. Kwa nini ni vizuri kujua majina ya vitu?
ii. Tutapata faida gani tukifuga wanyama waliotajwa?

**b. Mchezo: Kama vile**

Hatua za kufuata:

i. Waambie watoto wakae kwenye eneo la wazi uwanjani wakugeukie.
ii. Wagawe watoto katika vikundi, kisha wafuate maelekezo unayotoa kwa zamu:
   - Kwa mfano "Ruka ruka kama sungura". Hapo watoto watafanya kitendo hicho kwa kufuata maelekezo yako.
   - Ruka ruka kama chura.
   - Nguruma kama simba.
   - Tikisika kama mti.
   - Ruka kama ndege.
   - Lia kama ng'ombe.
   - Endesha gari kama dereva.
iii. Ongeza michezo mingi kadiri unavyoweza ili kubainisha majina mengi zaidi.
iv. Wape watoto nafasi ya kuongeza maneno yao.

**Tafakari**

i. Je, umependa kitu gani katika mchezo huo?
ii. Taja majina ya wanyama uliojifunza leo



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 60 9/18/19 4:59 PM

**Husisha**

i. Je, ni maeneo gani mengine umeona vitu vilivyotajwa katika mchezo?
ii. Ni vitu gani vingine unavyovifahamu majina yake ambavyo havikutajwa?

**Tumia**

i. Je, kuna faida gani kujua majina ya vitu?
ii. Je, tunapata nini kutoka kwa wanyama waliotajwa?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutaja majina ya watu, wanyama na vitu.

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kutamka sauti za irabu**

Mwalimu waongoze watoto:

i. kuangalia picha mbalimbali za vitu ambavyo majina yake yanaanza na herufi za irabu;
ii. kutamka sauti za mwanzo za majina ya picha hizo;
iii. kufanya mazoezi ya kutamka sauti za mwanzo za majina yanayoanza na herufi za irabu; na
iv. kuimba nyimbo kwa kutamka herufi za irabu.

Mchezo na wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Wimbo wa kutamka sauti za irabu.
b. Mchezo wa kuokota kadi.

**a. Wimbo wa kutamka sauti za irabu**

Vifaa: Kadi za picha ya andazi, embe, watoto wanaoimba, mtoto anayeoga na ua

Hatua za kufuata:

i. Mwalimu, waoneshe watoto picha ya andazi, embe, watoto wanaoimba, mtoto anayeoga na ua ambazo zinaanza na herufi za mwanzo za irabu (a, e, i, o, u).
ii. Waelekeze watoto wataje majina ya picha wanazoziona kwenye kadi.
iii. Waongoze watoto waimbe wimbo ufuatao unaotaja herufi za mwanzo za irabu katika picha hizo:

*Sauti ya mwanzo katika neno andazi "a" Tuimbe sote kwa pamoja sauti "a"*
*Sauti ya mwanzo katika neno embe ni "e" Tuimbe sote kwa pamoja sauti "e"*
*Sauti ya mwanzo katika neno imba ni "i" Tuimbe sote kwa pamoja sauti "i"*
*Sauti ya mwanzo katika neno oga ni "o" Tuimbe sote kwa pamoja sauti "o"*
*Sauti ya mwanzo katika neno ua ni "u" Tuimbe sote kwa pamoja sauti "u"*



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 61 9/18/19 4:59 PM

iv. Tumia picha nyingine ulizochora katika kadi zenye majina yanayoanza na herufi za irabu.

**Tafakari**

Taja sauti za herufi ulizojifunza.

**Husisha**

Je, ni majina gani mengine ya vitu unayoyafahamu yanayoanza na herufi ulizojifunza?

**Tumia**

Tamka sauti za mwanzo za herufi katika picha zifuatazo: ungo, askari, endesha, osha na ita.

**b. Mchezo: Kuokota kadi**

Vifaa: Kadi zenye picha mbalimbali zinazoanza na herufi za irabu na kadi zenye herufi za irabu hizo

Hatua za kufuata:

i. Andaa kadi zenye picha mbalimbali ambazo herufi ya mwanzo ni irabu.
ii. Andaa kadi zenye herufi za irabu hizo.
iii. Wagawe watoto katika vikundi kulingana na idadi ya watoto darasani.
iv. Gawia kila kikundi kadi za picha na herufi za irabu.
v. Kadi za picha zifunikwe uso chini.
vi. Kadi za herufi za irabu zipangwe pembeni.
vii. Kila mtoto kwa zamu katika kikundi afunue kadi moja, atamke ni picha gani kisha aioanishe na kadi moja ya irabu iliyo pembeni.
viii. Hakikisha kila mtoto ameshiriki katika mchezo.

**Tafakari**

i. Taja picha ulizoziona kwenye kadi.
ii. Taja herufi ulizoziona kwenye kadi.
iii. Je, uliokota kadi ngapi? Zilikuwa na herufi zipi?

**Husisha**

i. Ni sehemu gani nyingine tunaweza kuona picha kama hizi?
ii. Taja vitu vingine vyenye majina yanayoanza na herufi hizi.

**Tumia**

Kujua kusoma herufi itakusaidiaje?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutamka sauti za irabu

**Shughuli ya 5: Kuwawezesha watoto kuhusianisha herufi za irabu na sauti zake**

Mwalimu waongoze watoto:

i. kuangalia kadi za herufi za irabu;
ii. kuhusianisha herufi ya irabu na sauti yake; na
iii. kutamka sauti za irabu kwa mpangilio.

Nyimbo zinazopendekezwa kufundishia na kujifunza katika shughuli hii ni:

a. Iangalie kwa makini herufi
b. Hii ndiyo a

**a. Wimbo: Iangalie kwa makini herufi**

Vifaa: Kadi za Herufi za Irabu na kadi za picha

Hatua za kufuata:

i. Mwalimu waongoze watoto waimbe wimbo ufuatao unaotaja herufi za irabu ukihusisha kitu halisi au picha uliyoishika.

*Iangalie kwa makini herufi a, sauti yake a, a, a, na neno ni anga*
*Iangalie kwa makini herufi e, sauti yake e, e, e, na neno ni embe*
*Iangalie kwa makini herufi i, sauti yake i, i, i, na neno ni imba*
*Iangalie kwa makini herufi o, sauti yake o o o na neno ni oga*
*Iangalie kwa makini herufi u, sauti yake u u u na neno ni unga*

ii. Waoneshe watoto kadi za herufi za irabu (a, e, i, o, u) na kuhusisha na sauti zake.

iii. Wape watoto kadi za picha za vitu vinavyoanza na herufi za irabu, kisha wazioanishe na kadi za irabu kwa kutamka sauti ya mwanzo.

**Tafakari**

Je, kikombe kinafanana na herufi gani? (Uliza swali kama hili kwa kila herufi)

**Husisha**

Vitu gani vingine vinafanana na herufi ulizojifunza?

**Tumia**

i. Je, unapenda kutaja herufi gani nyingine?
ii. Taja majina ya watoto wenzako yanayoanza na herufi ulizojifunza?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 63 9/18/19 4:59 PM

**b. Wimbo: Hii ndiyo a**

Vifaa: Picha zenye herufi za irabu

Hatua za kufuata

i. Mwalimu waongoze watoto waimbe wimbo ufuatao unaotaja herufi za irabu ukihusisha na kitu halisi au picha husika.

*Hii ndiyo a, a, a, a ina mkia mfupi a a a*
*Hii ndiyo e, e, e, e ipo kama kata e e e*
*Hii ndiyo i, i, i, i ina kofia kichwani i i i*
*Hii ndiyo o, o, o, o ipo kama chungwa o o o*
*Hii ndiyo u, u, u, u, ipo kama kikombe u u u*

ii. Waoneshe watoto kadi za herufi za irabu (a, e, i, o, u) na kuhusisha na sauti zake.
iii. Wape watoto kadi za herufi za irabu kisha wazihusianishe na sauti zake.
iv. Wape watoto kadi za picha za vitu vinavyoanza na herufi za irabu, kisha wazioanishe na kadi za irabu kwa kutamka sauti ya mwanzo.

**Tafakari**

Je, herufi a inafanana na kitu gani? (Uliza swali kama hili kwa kila herufi)

**Husisha**

Vitu gani vingine vinafanana na herufi ulizojifunza?

**Tumia**

i. Mwalimu onesha kadi zenye herufi hizi na watoto wazitamke.
ii. Majina gani ya watoto wenzako yanayoanza na herufi ulizojifunza?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuchunguza kama kila mtoto ameweza:

i. kuhusisha herufi za irabu na sauti zake; na
ii. kutaja majina/maneno yanayoanza na herufi za irabu.

**Shughuli ya 6: Kuwawezesha watoto kutamka sauti za konsonanti (b, m, k, d, n)**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuangalia picha mbalimbali za vitu ambavyo majina yake yanaanza na herufi ya konsonanti hizo;
ii. kutamka sauti za mwanzo za majina ya picha hizo; na
iii. kufanya mazoezi ya kutamka sauti za mwanzo za majina yanayoanza na konsonanti.

Wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni wimbo wa kutamka sauti za konsonanti.

**Wimbo: Kutamka sauti za konsonanti**



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 64 9/18/19 4:59 PM

Vifaa: kadi za Picha ya bata, mti, kuku, dawati na nyinginezo ambazo zinaanza na herufi za mwanzo za konsonanti na kadi za herufi za konsonanti

Hatua za kufuata:

i. Mwalimu, waoneshe watoto picha za bata, mti, kuku, dawati na nyinginezo ambazo zinaanza na herufi za mwanzo za konsonanti.
ii. Waulize watoto wataje majina ya picha wanazoziona katika kadi.
iii. Waoneshe watoto kadi za herufi za konsonanti na kuhusisha na sauti zake.
iv. Wape watoto kadi za herufi za konsonanti kisha wazihusianishe na picha zake.
v. Waongoze watoto waimbe wimbo ufuatao unaotaja sauti za mwanzo za konsonanti katika picha hizo:

*Sauti ya mwanzo katika neno **bata** ni "**b**"*
*Tuimbe sote kwa pamoja sauti "**b**"*
*Sauti ya mwanzo katika neno **mti**, ni "**m**"*
*Tuimbe sote kwa pamoja sauti "**m**"*
*Sauti ya mwanzo katika neno **kuku** ni "**k**"*
*Tuimbe sote kwa pamoja sauti "**k**"*
*Sauti ya mwanzo katika neno **dawa** ni "**d**"*
*Tuimbe sote kwa pamoja sauti "**d**"*
*Sauti ya mwanzo katika neno **nazi** ni "**n**"*
*Tuimbe sote kwa pamoja sauti "**n**".*

vi. Tumia kadi za picha nyingine zenye majina yanayoanza na herufi za konsonanti zilizoainishwa.

**Tafakari**

Taja sauti za herufi ulizoziimba kwenye wimbo.

**Husisha**

Je, ni majina gani mengine ya vitu unayoyafahamu yanayoanza na sauti b, m, k, d, na n?

**Tumia**

Tamka sauti za mwanzo za maneno yafuatayo: babu, baba, bakuli, mama, maji, maua, mkeka, kaka, kabati, kisu, kofia, kijiko, dada, debe, doa, dirisha, dawati.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 65 9/18/19 4:59 PM

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutamka sauti za konsonanti (b, m, k, d, n) kwa usahihi.

**Shughuli ya 7: Kuwawezesha watoto kuhusianisha maumbo ya herufi za konsonanti (b, m, k, d, n) na sauti zake**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuangalia kadi za herufi za konsonanti hizo;
ii. kuhusianisha herufi za konsonanti na sauti zake; na
iii. kufanya mazoezi ya kuhusianisha herufi za konsonanti na sauti zake.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Kuokota kadi

**Mchezo: Kuokota kadi**

Vifaa: Kadi za picha mbalimbali ambazo herufi za mwanzo ni konsonanti na kadi zenye herufi za konsonanti hizo

Hatua za kufuata:

i. Andaa kadi zenye picha mbalimbali ambazo herufi za mwanzo ni konsonanti.
ii. Andaa kadi zenye herufi za konsonanti.
iii. Wagawe watoto katika vikundi kulingana na idadi yao darasani.
iv. Gawa kadi za picha na herufi za konsonanti kwa kila kikundi.
v. Kadi za picha zifunikwe uso chini.
vi. Kadi za herufi za konsonanti zipangwe pembeni.
vii. Kila mtoto kwa zamu katika kikundi afunue kadi moja, atamke ni picha gani kisha aioanishe na kadi moja ya konsonanti iliyo pembeni.
viii. Hakikisha kila mtoto ameshiriki katika mchezo.

**Tafakari**

Sauti ya mwanzo ya picha ulizoona zinatamkwaje?

**Husisha**

Taja majina ya vitu vingine yanayoanza na herufi ulizojifunza.

**Tumia**

Onesha picha inayoanza na herufi ulizojifunza?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 66 9/18/19 4:59 PM

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuchunguza kama kila mtoto ameweza kuhusianisha herufi za konsonanti (b, m, k, d, n) na sauti zake.

**Kumbuka:** Mwalimu, fundisha makundi mengine ya konsonanti (l, t, p, s, f, j) na (g, y, z, h, r, w, v, ch) kwa kufuata hatua kama shughuli ya 6 - 7 inavyoelekeza.

**Shughuli ya 8: Kuwawezesha watoto kubaini picha zenye maneno/majina yanayoanza na irabu au konsonanti**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuchunguza picha zenye maneno/majina yaliyoanza na irabu na konsonanti;
ii. kutaja majina ya vitu wanavyoviona yanayoanza na irabu na konsonanti;
iii. kuchora picha zenye maneno/majina yanayoanza na irabu na konsonanti; na
iv. kucheza michezo ya kubaini maneno/majina yanayoanza na irabu na konsonanti.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Kuokota kadi. Rejea mchezo huu kwenye shughuli ya 7 katika umahiri mahususi huu.

**Tafakari**

Sauti ya mwanzo ya picha uliyoiona inatamkwaje?

**Husisha**

Taja majina ya vitu vingine unavyovifahamu yanayoanza na herufi ulizojifunza.

**Tumia**

Onesha picha katika kadi inayoanza na herufi ulizojifunza.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutaja majina/maneno yanayoanza na herufi za irabu au konsonanti.

**4.2.2.4 Kumwezesha mtoto kujenga stadi za awali za kuandika**

Hii ni stadi mojawapo ya lugha ambayo huhusisha namna mtoto anavyomudu mkao, kushika viandikio na kuandika. Mtoto akiweza kutumia viandikio atakuwa na uwezo wa kuwasilisha mawazo yake kwa njia ya maandishi.

Ili kumwezesha mtoto kujenga stadi hizi, ni muhimu kumwongoza kuyamudu matendo ya awali ya kuandika, ikiwemo mazoezi ya vidole na mikono, kuchora mistari, kuchora michoro mbalimbali, kuumba/kuunda vitu mbalimbali, kufuatisha maumbo ya herufi na kuandika herufi.

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kujenga stadi za awali za kuandika**

Mtoto mwenye stadi za awali za kuandika, atakuwa na uwezo wa kuwasiliana kwa njia ya maandishi. Pia atakuwa na uwezo wa kutoa ujumbe au kuonesha hisia kupitia maandishi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Nyimbo, michezo, onesho mbinu, kazi mradi, igizo dhima na maswali na majibu

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Kanda za video, tarakilishi, vijiti, penseli, chaki, vifutio, vibao, vipande vya makasha, mchanga, kadi za herufi, maumbo ya herufi, kibao cha kuandikia, herufi mkwaruzo, stensili, mkasi, mbegu za mimea, shanga na bango kitita

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kufanya mazoezi mbalimbali ya kuimarisha misuli ya mikono na vidole**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja matendo yanayohusisha misuli ya mikono na vidole;
ii. kufanya mazoezi ya kuimarisha misuli ya mikono na vidole; na
iii. kucheza michezo mbalimbali itakayoimarisha misuli ya mikono na vidole.

Mchezo na wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Wimbo wa Mama Jamila
b. Mchezo wa kudosi

**a. Wimbo: Mama Jamila**

Hatua za kufuata:

i. Waelekeze watoto wasimame katika duara au nusu duara.
ii. Anza kuimba na kuonesha matendo yanayoendana na wimbo unaoimba kama ifuatavyo:

*Mama Jamila, mwambie Jamila, akoroge rangi, kwa vidole vyake,*
*Mama Jamila, mwambie Jamila, apake rangi kwa vidole vyake,*
*Mama Jamila, mwambie Jamila, asonge ugali, kwa mkono wa kulia,*
*Mama Jamila, mwambie Jamila, asonge ugali, kwa mkono wa kushoto,*
*Mama Jamila, mwambie Jamila, anawe mikono kwa maji safi,*
*Mama Jamila, mwambie Jamila, achore picha kwa mikono yake.*

iii. Ongeza matendo mengi kadiri uwezavyo ambayo yatamsaidia mtoto kuimarisha misuli ya mikono na vidole.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 68 9/18/19 4:59 PM

**Tafakari**

i. Je, ni vitendo gani ulivyovitenda vilivyohusisha vidole vyako?
ii. Je, ni vitendo gani ulivyovitenda vilivyohusisha mkono mzima?

**Husisha**

i. Je, ni kazi zipi zingine huwa unazifanya ambazo zinahusisha mikono yako?
ii. Je, ni kazi zipi zingine ambazo huwa unazifanya kwa vidole vya mikono yako?

**Tumia**

Je, utakwenda kufanya nini kwa kutumia mikono yako?

**b. Mchezo: Kudosi**

Hatua za kufuata:

i. Nyoosha mkono wa kulia kisha waoneshe watoto kidole gumba na cha kati ambavyo vitatumika katika mchezo huo.
ii. Gusanisha vidole hivyo ili watoto wavione.
iii. Waoneshe watoto namna ya kucheza mchezo wa *kudosi*. Hakikisha vinatoa mlio na watoto wausikie.
iv. Waelekeze watoto wafanye kama ulivyofanya. Hakikisha kila mtoto anashiriki.

**Tafakari**

Je, ni ugumu gani ulioupata wakati wa kucheza mchezo?

**Husisha**

Je, ni kazi gani nyingine ambazo hutumia vidole kuzifanya?

**Tumia**

Je, ni vitendo gani utafanya kwa kutumia vidole?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutenda vitendo vinavyoimarisha misuli ya mikono na vidole.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kutumia vichoreo/viandikio**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vichoreo/viandikio wanavyovifahamu;
ii. kushika na kutumia viandikio/vichoreo ipasavyo; na
iii. kufanya mazoezi ya kutumia viandikio/vichoreo.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Mwalimu kasema.

**Mchezo: Mwalimu kasema**

Vifaa: Vijiti/kalamu

Hatua za kufuata:

i. Andaa vijiti kwa muundo wa kalamu.
ii. Watoe watoto nje ya darasa wakae katika duara.
iii. Gawa vijiti /kalamu kwa kila mtoto.
iv. Chagua mtoto ataje kitu watakachochora aseme "Mwalimu kasema tuchore….."
v. Mwalimu akague kama wote wameshika kalamu/kijiti kwa usahihi.
vi. Ongoza watoto wachore picha ya kitu kilichotajwa.
vii. Atakayewahi kumaliza ndiye atakayetaja kitu kingine cha kuchora.

**Tafakari**

i. Tumechora vitu gani katika mchezo wetu?
ii. Kipi kilikuwa kigumu kuchora?
iii. Kipi kilikuwa kirahisi kuchora?

**Husisha**

i. Je, umewahi kuchora kitu gani kingine? Wapi?
ii. Umewahi kumuona nani akichora? Alichora nini?

**Tumia**

i. Unapenda kuchora nini kingine?
ii. Utakwenda kumweleza nani kitu ulichokichora leo?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kushika na kutumia viandikio/vichoreo ipasavyo.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kufanya mazoezi ya kuandika**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kufanya mazoezi ya kuchora mistari hewani na kwenye mchanga;
ii. kuchora mistari katika vibao, karatasi na makasha kutoka juu kwenda chini; na
iii. kuchora mistari katika vibao, karatasi na makasha kutoka kushoto kwenda kulia.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Kuandika herufi kwa kutumia mwili



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 70 9/18/19 4:59 PM

**Mchezo: Kuandika herufi kwa kutumia mwili**

Hatua za kufuata:

i. Andika herufi ‘a’ ubaoni ili watoto waione jinsi inavyoandikwa. Herufi iwe kubwa kwa umbo.

ii. Simama kwa kutazama ubaoni kisha waoneshe watoto namna unavyoiandika herufi hiyo hatua kwa hatua kwa kutumia mwili.

iii. Waelekeze watoto nao wafanye kama ulivyofanya wewe. Hakikisha kila mtoto anashiriki kikamilifu na anafuata hatua ulizowaelekeza.

iv. Watoto wakimudu kuandika herufi “a”, andika ubaoni herufi inayofuata na kuonesha namna inavyoandikwa. Fanya hivyo kwa herufi zote za irabu.

***Angalizo:*** Unaweza pia kuandika herufi hizo hewani kwa kutumia kidole.

**Tafakari**

i. Je, ni herufi gani ilikuwa rahisi kuandika?
ii. Je, ni herufi gani ilikuwa ngumu kuandika?
iii. Je, umeweza kuandika herufi ngapi?

**Husisha**

Je, umewahi kuandika herufi hizi mahali pengine? Wapi?

**Tumia**

Je, unaweza kutumia kidole au kijiti kuandika herufi hizo hewani? Ziandike.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutenda vitendo mbalimbali vya kujiandaa kuandika.

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kuumba/kuunda maumbo ya irabu**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kubaini makunzi watakayotumia kuumba/kuunda maumbo mbalimbali ya irabu;

ii. kuumba/kuunda maumbo ya irabu kwa kufuata hatua; na

iii. kufanya mazoezi ya kuumba/kuunda.

**Tafakari**

i. Taja makunzi uliyoyabaini ambayo yanaweza kutumika kuumba irabu.
ii. Taja maumbo ya irabu uliyoyaumba.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 71 9/18/19 4:59 PM

**Husisha**

Taja makunzi mengine ambayo unaweza kuyatumia kuumba maumbo ya irabu.

**Tumia**

Je, ukifika nyumbani utaumba maumbo gani ya irabu?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kuumba/kuunda maumbo ya irabu.

**Shughuli ya 5: Kuwawezesha watoto kufuatisha maumbo ya irabu**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kufuatisha maumbo ya irabu;
ii. kufuatisha maumbo ya irabu kwa kutumia vitu mbalimbali; na
iii. kupaka rangi maumbo ya irabu.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Mchezo wa kadi

**Mchezo: Mchezo wa kadi**

Vifaa: Kadi zenye herufi za irabu zenye nukta nukta

Hatua za kufuata:

i. Tayarisha kadi za maumbo ya irabu kulingana na idadi ya watoto, kisha andika maumbo ya irabu kwa kutumia nukta.
ii. Wagawe watoto katika vikundi kisha gawa kadi kwenye kundi.
iii. Mpe penseli au rangi kila mtoto.
iv. Elekeza namna ya kufuatisha herufi ya irabu iliyopo kwenye kadi kwa usahihi. Hakikisha kila mtoto anashiriki kikamilifu katika mchezo huu.
v. Mchezo utakamilika utakapoona inafaa.

**Tafakari**

Umejifunza kuandika herufi gani?

**Husisha**

Umewahi kuandika herufi kama hii? Wapi?

**Tumia**

Utamfundisha nani mwingine ulichoandika leo?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza:



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 72 9/18/19 4:59 PM

i. kufuatisha maumbo ya irabu yaliyoandaliwa; na
ii. kufuatisha maumbo ya irabu kwa kutumia vitu mbalimbali.

**Shughuli ya 6: Kuwawezesha watoto kuandika herufi za irabu (a, e, i, o, u) kwa kufuata hatua**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuandika herufi za irabu hewani kwa kufuata hatua;
ii. kuandika herufi za irabu kwenye mchanga kwa kufuata hatua;
iii. kuandika herufi za irabu kwenye vibao kwa kufuata hatua; na
iv. kuandika herufi za irabu kwenye karatasi kwa kufuata hatua.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni mchezo wa kadi

**Mchezo: Mchezo wa kadi**

Vifaa: Kadi zenye maumbo ya irabu

Hatua za kufuata

i. Tayarisha kadi za maumbo ya irabu kulingana na idadi ya watoto kisha chora maumbo ya irabu.
ii. Wagawe watoto katika vikundi kisha gawa kadi kwenye kundi.
iii. Mpe penseli au rangi kila mtoto.
iv. Elekeza namna ya kupaka rangi ukumbi wa herufi ya irabu iliyopo kwenye kadi kwa usahihi. Hakikisha kila mtoto anashiriki kikamilifu katika mchezo huu.
v. Mchezo utakamilika utakapoona inafaa.

**Tafakari**

Ulipaka rangi umbo gani?

**Husisha**

i. Kitu gani kingine umewahi kupaka rangi?
ii. Ni rangi gani nyingine unayoipenda?

**Tumia**

Utakapopewa picha nyingine utaweza kuipaka rangi?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kuandika herufi za irabu (a, e, i, o, u).



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 73 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 7: Kuwawezesha watoto kuumba/kuunda maumbo ya konsonanti (b, m, k, d, n)**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kubaini makunzi watakayotumia kuumba/kuunda maumbo mbalimbali ya konsonanti;
ii. kuumba/kuunda maumbo ya konsonanti kwa kufuata hatua; na
iii. kufanya mazoezi ya kuumba/kuunda.

Wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Wimbo wa kuandika

**Wimbo: Wimbo wa kuandika**

Hatua za kufundisha:

i. Anza kuimba kwa kuonesha matendo na watoto wakikusikiliza.
ii. Imba mstari mmoja baada ya mwingine na watoto wafuatishe.
iii. Waongoze watoto kuimba huku wakionesha hatua za uandishi kulingana na herufi husika.

*Kuandika napenda maumbo ya sauti mwalimu niongoze*
*Kuandika napenda maumbo ya sauti mwalimu nifundishe*
*Kwa kuliumba umbo la sauti ya "b" hatua 3 fuata*
*Kwa kuliumba umbo la sauti ya "m" hatua 6 fuata*
*Kwa kuliumba umbo la sauti ya "k" hatua 3 fuata*
*Kwa kuliumba umbo la sauti ya "d" hatua 4 fuata*
*Kwa kuliumba umbo la sauti ya "n" hat*ua 4 fuata

**Tafakari**

Ni maumbo ya herufi gani umeyasikia katika wimbo?

**Husisha**

i. Umewahi kusikia wapi maumbo ya herufi uliyoyataja?
ii. Taja maumbo mengine unayoyafahamu?

**Tumia**

Je, utaweza kuumba maumbo gani mengine ya herufi?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kuumba/kuunda maumbo ya konsonati (b, m, k, d, n).



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 74 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 8: Kuwawezesha watoto kufuatisha maumbo ya konsonanti (b, m, k, d, n)**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kufuatisha maumbo ya konsonanti;
ii. kufuatisha maumbo ya konsonanti kwa kutumia rangi/penseli; na
iii. kufanya mazoezi ya kufuatisha kwa kutumia rangi/penseli.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Mchezo wa kadi.

Rejea katika Shughuli ya 5 katika umahiri mahususi wa kujenga stadi za awali za Kuandika.

**Tafakari**

Umejifunza kuandika herufi gani?

**Husisha**

Herufi b, m, k, d, n umewahi kuziandika mahali gani pengine?

**Tumia**

Je, utajifunza kuandika maumbo gani ya herufi mengine?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza:

i. kufuatisha maumbo ya konsonanti yaliyoandaliwa; na
ii. kufuatisha maumbo ya konsonanti kwa kutumia rangi/penseli.

**Shughuli ya 9: Kuwawezesha watoto kuandika herufi za konsonanti (b, m, k, d, n) kwa kufuata hatua**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuandika herufi za konsonanti hewani kwa kufuata hatua;
ii. kuandika herufi za konsonanti kwenye mchanga kwa kufuata hatua;
iii. kuandika herufi za konsonanti kwenye vibao kwa kufuata hatua; na
iv. kuandika herufi za konsonanti kwenye karatasi kwa kufuata hatua.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Mwalimu kasema tuandike.

**Mchezo: Mwalimu kasema tuandike**

Vifaa: vijiti, vibao, chaki, karatasi na penseli



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 75 9/18/19 4:59 PM

Hatua za kufuata:

i. Andaa vijiti kwa muundo wa kalamu.
ii. Watoe watoto nje ya darasa wakae katika duara.
iii. Gawa vijiti /kalamu kwa kila mtoto.
iv. Chagua mtoto ataje kitu watakachoandika aseme “Mwalimu kasema tuandike ....”
v. Kagua kama wote wameshika kalamu/kijiti kwa usahihi.
vi. Ongoza watoto waandike herufi ya konsonanti iliyotajwa.
vii. Atakayewahi kumaliza ndiye atakayetaja herufi nyingine ya kuandika.

**Tafakari**

i. Tumeandika herufi gani katika mchezo huu?
ii. Herufi gani ilikuwa ngumu kwako kuandika?
iii. Herufi gani ilikuwa rahisi kwako kuandika?

**Husisha**

i. Umewahi kuandika herufi gani nyingine? Wapi?
ii. Umewahi kumuona nani mwingine akiandika herufi? Herufi gani?

**Tumia**

i. Utapenda kuandika herufi gani nyingine?
ii. Utakwenda kumweleza nani kuhusu herufi ulizoandika leo?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kuandika herufi za konsonati.

***Kumbuka:*** Mwalimu, fundisha makundi mengine ya konsonanti (l, t, p, s, f, j) na (g, y, z, h, r, w, v, ch) kwa kufuata hatua kama shughuli ya 7- 9 inavyoelekeza.

### 4.2.3 Kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kutunza afya

Sehemu hii inalenga kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kutunza afya yake. Mwalimu, unapaswa kufahamu kuwa, ili mtoto akue na kujifunza kwa ufanisi, ni muhimu awe na afya nzuri. Tafiti zinaonyesha kwamba, afya ya akili hutegemea afya ya mwili, hivyo basi, suala la kutunza afya ni muhimu kupewa kipaumbele. *Mwalimu, unawezaje kuwajengea watoto uwezo wa kutunza afya?* Bila shaka, ili kuwajengea watoto uwezo wa kutunza afya, unatakiwa uwawezeshe kutambua sehemu za mwili na namna ya kuzitunza, kutunza mavazi, kutunza vyombo vya chakula, kula chakula bora, kutambua magonjwa mbalimbali na jinsi ya kuyaepuka.

Mwalimu, kumbuka kuwa katika sehemu hii unashauriwa kufundisha sehemu za nje za mwili wa binadamu. Vilevile unapaswa kuzingatia mila na desturi za jamii husika.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 76 9/18/19 4:59 PM

Umahiri huu umejengwa na umahiri mahususi sita kama ifuatavyo:

### 4.2.3.1 Kumwezesha mtoto kubainisha sehemu za nje za mwili na kazi zake

Mwalimu, katika ujifunzaji na ufundishaji wa watoto unapaswa kuwawezesha kuzifahamu sehemu za nje za mwili na kazi zake.

**Umuhimu wa kuwawezesha watoto kubaini sehemu za nje za mwili**

Ni muhimu kwa mtoto kuzitambua sehemu za nje za mwili wake ili aweze kuzitunza.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Nyimbo, uchunguzi, majadiliano, maswali na majibu, bungua bongo, michezo, ngonjera, vitendawili na kisa mafunzo

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Picha, vitabu, vifani, bango kitita, michoro na chati zinazoonesha sehemu za nje za mwili

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kubaini sehemu za nje za mwili**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja sehemu mbalimbali za mwili;
ii. kubainisha sehemu za nje za mwili;
iii. kuonesha sehemu za nje za mwili; na
iv. kuimba nyimbo zinazotaja sehemu za nje za mwili.

Wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni wimbo wa Kichwa, mabega, magoti na vidole.

**Wimbo: Kichwa mabega, magoti na vidole**

Hatua za kufuata:

i. Wapange watoto katika duara huku wakikuangalia.
ii. Imba wimbo wa kichwa, mabega, magoti na vidole ili kila mtoto ausikie.

   *Kichwa, mabega, kifua, kiuno,*
   *Magoti, vidole, magoti, vidole,*
   *Kichwa, mabega, kifua, kiuno,*
   *Magoti, vidole, magoti, vidole,*
   *Macho, masikio, mdomo, pua*.

iii. Watoto waimbe wimbo huo huku wakionesha vitendo vya kugusa sehemu za mwili zinazotajwa. Imba pamoja na watoto mara kadhaa ili wapate kuelewa na kuuzoea.
iv. Unaweza kuongeza sehemu nyingi zaidi za mwili wa binadamu kadiri utakavyoona inafaa.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 77 9/18/19 4:59 PM

**Tafakari**

Wakati unaimba umegusa sehemu gani za mwili?

**Husisha**

i. Sehemu gani za mwili wa binadamu ulikuwa unafahamu majina yake kabla?
ii. Ulijifunzia wapi majina hayo?

**Tumia**

Tunatumia mikono kufanyia kitu gani kingine? (Mwalimu, endelea kuuliza kuhusu matumizi ya sehemu nyingine za mwili).

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kutaja sehemu za nje za mwili wake; na
ii. kuonesha sehemu za nje za mwili wake.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kubaini kazi za sehemu za nje za mwili**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja kazi za sehemu za nje za mwili wake;
ii. kutenda vitendo mbalimbali kwa kutumia sehemu za nje za mwili; na
iii. kuigiza kazi za kila sehemu za nje za mwili.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Majigambo ya sehemu za nje za mwili.

**Mchezo: Majigambo ya sehemu za nje za mwili**

Hatua za kufuata:

i. Waeleze watoto kuwa watacheza mchezo wa majigambo ya sehemu za nje za mwili.
ii. Onesha kila sehemu ya mwili ikijigamba kwa mfano.
*Mimi ni kichwa kazi yangu ni kutunza kumbukumbu.*
*Mimi ni macho kazi yangu ni kuona.*
*Mimi ni pua kazi yangu ni kunusa.*
*Mimi ni masikio kazi yangu ni kusikia*.
iii. Teua mtoto mmoja mmoja afanye majigambo ya sehemu moja ya nje ya mwili kama ulivyoelekeza huku darasa zima likifuatisha majigambo hayo.
iv. Mchezo utamalizika utakavyoona inafaa.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 78 9/18/19 4:59 PM

**Tafakari**

i. Sehemu gani za mwili zimetajwa wakati wa mchezo?
ii. Sehemu za nje za mwili zilizotajwa zinafanya kazi gani?

**Husisha**

i. Wakati gani umewahi kutumia sehemu za nje za mwili zilizotajwa?
ii. Je, ulizitumia kufanya nini?

**Tumia**

Taja matumizi ya sehemu moja ya nje ya mwili wako.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama mtoto ameweza kueleza kazi za sehemu za nje ya mwili wake.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kutumia milango ya fahamu kubaini vitu katika mazingira**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja milango ya fahamu;
ii. kuelezea kazi za milango ya fahamu; na
iii. kutumia milango ya fahamu kutambua vitu katika mazingira.

Wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni wimbo wa Milango ya fahamu

**Wimbo: Milango ya fahamu**

*Milango ya fahamu eeeh mingapi x2*
*Milango fahamu eeeh mitano*
*Wa kwanza macho kuona, kuonaa*
*Wa pili ulimi kuonja, kuonja*
*Wa tatu ngozi kuhisi, kuhisi*
*Wa nne sikio kusikia, kusikia*
*Wa tano pua kunusa, kunusa.*
*Milango ya fahamu eeeh mingapi*
*Milango ya fahamu eeeh mitano*

**Tafakari**

i. Umetaja milango mingapi ya fahamu?
ii. Mlango gani wa fahamu hutumika kusikia?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 79 9/18/19 4:59 PM

**Husisha**

i. Umewahi kuonja kitu gani? Kilikuwa kitamu au kichungu?
ii. Taja vitu ambavyo ni vitamu au vichungu.

**Tumia**

i. Utafanya nini utakapojisikia baridi?
ii. Utakaposikia sauti ya mbwa mkali anabweka utafanya nini?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutumia milango ya fahamu kutambua vitu katika mazingira.

**4.2.3.2 Kumwezesha mtoto kujenga stadi za kutunza mwili**

Mwalimu, mtoto anapaswa kujenga stadi za kutunza mwili, na anatakiwa kutambua vifaa vya kufanyia usafi wa mwili pamoja na kuvitumia. Stadi hizi zinahusisha pia kuwaongoza watoto kueleza taratibu za kuzingatia wakati wa kufanya usafi wa mwili.

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kujenga stadi za kutunza mwili**

Mwalimu, utunzaji wa mwili ni jambo muhimu kwa mtoto ili aweze kuwa na afya bora na kujikinga na maradhi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Nyimbo, igizo dhima, onesho mbinu, maswali na majibu, majadiliano, bungua bongo, uchunguzi, michezo na igizo

**Zana za Kufundishia na kujifunzia**

Chati, picha, vitabu, kanda za video, sabuni, maji, beseni, ndoo, dodoki, jiwe laini la kujisugulia, taulo na mafuta

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kubaini vifaa vya kufanyia usafi wa mwili**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vifaa wanavyotumia kufanya usafi wa mwili;
ii. kuchunguza vifaa mbalimbali vya kufanyia usafi wa mwili; na
iii. kuelezea matumizi ya vifaa vya kufanyia usafi wa mwili.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Duara la usafi

**Mchezo: Duara la usafi**

Vifaa: Picha au vifaa halisi vinne vya kufanyia usafi wa mwili

Hatua za kufuata:

i. Chora mstari wa kuanzia katika eneo la kuchezea.
ii. Wagawe watoto katika vikundi kulingana na idadi yao darasani, na wasimame nyuma ya mstari wa kuanzia.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 80 9/18/19 4:59 PM

iii. Chora maduara manne mbele ya kila kikundi umbali wa hatua 5 – 10 toka mstari wa kuanzia.
iv. Onesha picha au vifaa halisi vinne vya kufanyia usafi wa mwili na waambie watoto wataje jina na matumizi ya kifaa hicho. Mfano: Huu ni mswaki, unatumika kusafisha meno.
v. Weka picha au kifaa halisi kimoja katika kila duara mbele ya kila kundi (mswaki, taulo, kitana, sabuni).
vi. Anza kutaja tendo moja la usafi, mfano "Kunawa mikono yako" na mtoto mmoja kutoka kila kundi atakimbia mbele kwenye duara lenye kifaa kinachohitajika kwa ajili ya tendo hilo la usafi. Atakanyaga mguu mmoja ndani ya duara lenye kifaa kinachohitajika na kuigiza kama anatenda tendo ulilolitaja kwa muda wa sekunde 5 na kurudi kwenye mstari.
vii. Utaendelea kutaja matendo mengine ya usafi, mfano, kusukutua kinywa, kuosha nywele, kuoga, kunawa uso na kukata kucha.
viii. Maliza mchezo baada ya watoto wote kushiriki katika mchezo.

**Tafakari**

i. Je, umeonesha vitendo gani vya usafi wa mwili wakati wa mchezo?
ii. Taulo linatumika kufanya nini?

**Husisha**

i. Wakati gani huwa unafanya vitendo vya usafi wa mwili?
ii. Ni vitu gani vinavyotumika wakati wa kuoga?

**Tumia**

Unapomaliza kuoga unatakiwa kufanya nini?

Utamsaidiaje rafiki yako asiyependa kuoga?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kutaja vifaa mbalimbali anavyotumia kufanya usafi wa mwili wake; na
ii. kueleza kazi ya kila kifaa.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kufanya usafi wa mwili**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kueleza namna wanavyofanya usafi wa mwili;
ii. kuchunguza namna usafi wa mwili unavyofanyika kwa usahihi; na
iii. kuonesha namna ya kufanya usafi wa mwili kwa hatua.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 81 9/18/19 4:59 PM

Wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni wimbo wa Kagere keupe

**Wimbo: Kagere keupe**

Hatua za kufuata:

i. Waongoze watoto kusimama mbele ya darasa au nje ya darasa wakiwa katika nusu duara.

ii. Anza kuimba huku ukionesha matendo na watoto wakikusikiliza

iii. Imba mstari mmoja baada ya mwingine na watoto wakufuatishe

iv. Waongoze watoto kuimba huku wakionesha matendo.

*Tujioshe mwili mzima twende safi shuleni*
*Tujioshe mwili mzima twende safi shuleni*
*Na Kagere Keupe mwalimu anapenda*
*Meno tusugue pia nguo tufue*
*Nywele tuzichane pia kucha tukate*
*Na Kagere Keupe mwalimu anapenda*
*Tusafishe masikio pia na macho*
*Tusafishe pua zetu tunawe uso*
*Na Kagere Keupe mwalimu anapenda*

**Tafakari**

i. Ni sehemu gani za mwili zimetajwa katika wimbo?
ii. Ni sehemu gani za mwili tunatakiwa kuzisafisha?

**Husisha**

i. Tunatumia nini kusafisha sehemu za mwili?
ii. Ni wakati gani tunatakiwa kupiga mswaki?

**Tumia**

i. Tunatakiwa kufanya nini kila tuamkapo?
ii. Tunatakiwa kufanya nini kila tunapochafuka?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kufanya usafi wa mwili kwa kufuata hatua.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 82 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kueleza umuhimu wa kufanya usafi wa mwili**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuonesha vitendo vya kufanya usafi wa mwili;
ii. kueleza umuhimu wa kufanya usafi wa mwili; na
iii. kutenda vitendo vinavyoonesha madhara ya kutofanya usafi wa mwili.

**Tafakari**

i. Taja vitendo vya kufanya usafi wa mwili ulivyoonesha.
ii. Eleza umuhimu wa kufanya usafi wa mwili.

**Husisha**

Ni wakati gani tunatakiwa kunawa mikono?

**Tumia**

Nini kitatokea kama usipooga?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kueleza umuhimu wa kufanya usafi wa mwili.

**4.2.3.3 Kumwezesha mtoto kujenga stadi za kutunza mavazi**

Stadi za utunzaji wa mavazi humwezesha mtoto kujenga tabia ya kuwa msafi na kutunza mavazi yake. Ili kumwezesha mtoto kujenga stadi hizo, mwongoze kutambua vifaa vya kufanyia usafi wa nguo, kufua na kukunja nguo pamoja na kuwa na mazoea ya kuvaa viatu.

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kujenga stadi za kutunza mavazi**

Stadi za kutunza mavazi zinamsaidia mtoto kuwa nadhifu na kumwepusha na maradhi. Ni muhimu kwa mtoto kuwa na tabia ya kufua nguo zake na kuzihifadhi mahali panapostahili.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Onesho mbinu, kisa mafunzo, hadithi, ngonjera, maigizo, nyimbo, michezo, maswali na majibu, matembezi ya galari, changanya kete na fikiri-jozisha-shirikisha

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Runinga, kanda za video, redio, picha, sabuni, maji, ndoo, beseni, taulo, pasi, kabati, sanduku na kikapu



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 83 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kubaini vifaa vya kufanyia usafi wa nguo.**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vifaa wanavyofanyia usafi wa nguo nyumbani;
ii. kueleza namna ya kutumia vifaa vya kufanya usafi wa nguo; na
iii. kutenda vitendo vinavyoonesha namna ya kufanya usafi wa nguo.

**Tafakari**

Taja vifaa vya kufanyia usafi ulivyovifahamu.

**Husisha**

Beseni hutumika kufanyia nini?

**Tumia**

Je, ukifika nyumbani utatumia vifaa gani kufua nguo?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kutaja vifaa vya kufanyia usafi wa nguo; na
ii. kueleza matumizi ya kila kifaa.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kufua nguo ndogondogo na nyepesi**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kueleza namna ya kufua na kuanika nguo ndogondogo na nyepesi;
ii. kufua nguo ndogondogo na nyepesi kwa kufuata hatua;
iii. kuanika nguo mahali panapostahili; na
iv. kueleza umuhimu wa kufua nguo.

**Tafakari**

Taja nguo ndogondogo unazoweza kuzifua.

**Husisha**

Ni vifaa gani ambavyo mnatumia nyumbani wakati wa kufua nguo?

**Tumia**

Baada ya kufua nguo, unazihifadhi sehemu gani?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kufua nguo kwa kuzingatia hatua na kuzianika.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 84 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kukunja nguo ndogondogo**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kueleza umuhimu wa kupiga pasi;
ii. kuonesha vitendo vya kukunja nguo ndogondogo;
iii. kueleza faida za kukunja nguo;
iv. kutaja mahali wanapohifadhi nguo; na
v. kueleza umuhimu wa kutunza nguo

**Tafakari**

Taja kifaa kinachotumika kupigia pasi.

**Husisha**

Baada ya kufua nguo, mnazianika sehemu gani?

**Tumia**

i. Je, ni kwanini tunapiga pasi nguo zetu?
ii. Je, ni kitu gani kitatokea tusipohifadhi nguo zetu sehemu inayostahili?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kukunja nguo ndogondogo.

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kufanya vitendo vya kuvaa na kuvua viatu**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitu wanavyovaa miguuni;
ii. kuonesha namna ya kuvaa na kuvua viatu kwa usahihi;
iii. kueleza umuhimu wa kuvaa viatu; na
iv. kueleza madhara ya kutovaa viatu.

**Tafakari**

Taja aina za viatu unavyovifahamu.

**Husisha**

Wakati wa kuoga unavaa nini miguuni?

**Tumia**

Je, ni nini kitatokea tusipovaa viatu?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza

i. kuvaa na kuvua viatu kwa usahihi; na
ii. kueleza umuhimu wa kuvaa viatu.

#### 4.2.3.4 Kumwezesha mtoto kujenga stadi za kutunza vyombo vya chakula

Kuwajengea stadi za kutunza vyombo vya chakula kutawasaidia watoto kulinda afya zao na kujiepusha na magonjwa yatokanayo na uchafu. Mwalimu, unapaswa kuwawezesha watoto kutambua vyombo vinavyotumika kwa chakula, vifaa vinavyotumika kusafisha vyombo vya chakula, pamoja na kusafisha vyombo hivyo.

**Umuhimu wa kujenga stadi za kutunza vyombo vya chakula**

Mwalimu, ni muhimu watoto kujenga stadi za kutunza vyombo vya chakula ili kujikinga na maradhi yatokanayo na uchafu.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Onesho mbinu, nyimbo, uchunguzi, michezo, maigizo na fikiri jozisha-shirikisha

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Runinga, kanda za video, chati, picha mbalimbali za vyombo, picha ya kabati la vyombo, vyombo vya chakula na vitabu

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kubaini vyombo vinavyotumika kwa chakula**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vyombo wanavyotumia kwa chakula nyumbani;
ii. kuchunguza vyombo mbalimbali vya chakula;
iii. kubainisha vyombo vya chakula;
iv. kuchora picha za vyombo vya chakula; na
v. kutaja matumizi ya kila chombo cha chakula.

**Tafakari**

Taja vyombo vya kulia chakula unavyovifahamu.

**Husisha**

i. Je, ni chombo gani mnatumia kunywea chai nyumbani?
ii. Je, ni vyombo gani mnavitumia kulia chakula mkiwa nyumbani?

**Tumia**

Taja vyombo utakavyotumia kupika chakula.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutaja vyombo vya chakula na matumizi yake.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kuosha vyombo vya chakula**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vifaa vinavyotumika kusafishia vyombo;
ii. kuelezea jinsi ya kusafisha vyombo vya chakula;



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 86 9/18/19 4:59 PM

iii. kufanya usafi wa vyombo vya chakula; na
iv. kufuta vyombo vya chakula.

**Tafakari**

Taja vifaa vinavyotumika kusafishia vyombo vya chakula.

**Husisha**

Je mnatumia nini kufuta vyombo vya chakula nyumbani?

**Tumia**

Je, vyombo vya chakula vikichafuka tunapaswa kufanya nini?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kufanya usafi wa vyombo vya chakula.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kuhifadhi vyombo vya chakula**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja mahali wanapohifadhi vyombo vya chakula;
ii. kuelezea jinsi ya kuhifadhi vyombo vya chakula;
iii. kupanga vyombo vya chakula mahali panapostahili; na
iv. kueleza umuhimu wa kuhifadhi vyombo vya chakula mahali panapostahili.

**Tafakari**

Je, ni mahali gani tunahifadhia vyombo vya chakula.

**Husisha**

Je, ni sehemu gani mnahifandhi vyombo vya chakula muwapo nyumbani?

**Tumia**

Je, kuna umuhimu gani wa kuhifadhi vyombo vya chakula mahali panaopostahili?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kuhifadhi vyombo vya chakula mahali panapostahili.

**4.2.3.5 Kumwezesha mtoto kubaini chakula bora**

Chakula bora husaidia kuufanya mwili kuwa na afya bora. Chakula bora ni kile kilicho na mchanganyiko wa viini lishe muhimu na vya msingi kwa ajili ya mahitaji ya mwili. Mwalimu, unapaswa kuwajengea watoto uwezo wa kutambua chakula bora kwa



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 87 9/18/19 4:59 PM

kuelezea vyakula wanavyokula, kubainisha chakula bora na kula kwa kufuata taratibu zinazokubalika.

***Tahadhari:*** Mwalimu, kumbuka kuwa kumshirikisha mtoto kuandaa chakula haimaanishi kwenda jikoni kupika.

**Umuhimu wa Kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kubaini chakula bora**

Ufahamu wa watoto kuhusu chakula bora ni muhimu kwa sababu unawahamasisha kula chakula bora kwa ajili ya kuimarisha afya zao.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Onesho mbinu, nyimbo, uchunguzi, ngonjera, michezo, igizo dhima, ziara za mafunzo na kualika mgeni

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Picha, vyakula, maji, kanda za video, vitabu, bango, bango kitita, redio, runinga

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kubainisha vyakula vinavyopatikana katika mazingira wanamoishi**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vyakula wanavyovifahamu;
ii. kueleza vyakula wanavyokula nyumbani; na
iii. kutumia picha kubaini aina za vyakula.

Wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni wimbo wa Aina za vyakula

**Wimbo: Aina za vyakula**

Hatua za kufuata:

i. Waambie watoto wataje aina za vyakula wanavyovijua.
ii. Imba wimbo wa vyakula bora unaoujua au unaweza kutumia wimbo ufuatao mara kadhaa;

*Parachichi x2*
*Mahindi x2*
*Nyama na karanga x2*
*Aina za vyakula x2*

iii. Waongoze watoto waimbe wimbo wa aina za vyakula mara kadhaa na hakikisha kila mtoto anaimba kama inavyotakiwa.

**Tafakari**

Je, umetaja vyakula gani katika wimbo uliouimba?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 88 9/18/19 4:59 PM

**Husisha**

i. Je, umeshawahi kula chakula chochote kati ya vilivyotajwa?
ii. Je, tunatakiwa kufanya nini kabla ya kula?

**Tumia**

i. Je, kwa nini tunakula?
ii. Je, utamweleza nani mwingine aina za vyakula ulizojifunza?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kubaini vyakula mbalimbali vinavyopatikana katika mazingira anamoishi.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kubaini chakula bora**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vyakula mbalimbali;
ii. kubainisha chakula bora kwa kuhusisha makundi mbalimbali ya vyakula; na
iii. kueleza umuhimu wa kula chakula bora.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Vyakula vyote

**Mchezo: Vyakula vyote**

Vifaa: Kadi zenye picha za vyakula bora tofauti

Hatua za kufuata:

i. Andaa kadi za picha za vyakula tofauti vya lishe bora kama parachichi, nyama, mahindi na karanga, kisha waoneshe watoto kadi hizo.
ii. Wagawe watoto katika vikundi na kila kikundi kikae katika duara.
iii. Kila mtoto apewe jina la chakula kwa kuhesabu 1-4, mfano ,namba 1 waitwe parachichi, namba 2 waitwe nyama, namba 3 waitwe mahindi na namba 4 waitwe karanga.
iv. Weka kiti katikati ya kila kikundi.
v. Waelekeze kuwa utakapotaja jina la chakula, wahusika watasogea katikati ili kuwahi kiti na atakayekosa kiti atakuwa mhitaji wa chakula. (mfano ukitaja mahindi wenye jina la mahindi kutoka kila kikundi watasogea).
vi. Mchezo utaendelea mpaka utakapotaja vyakula vyote.

**Tafakari**

i. Umesikia aina gani za vyakula zilizotajwa katika mchezo huu?
ii. Vyakula gani umevipenda zaidi? Kwa nini?

**Husisha**

Je, ni aina gani nyingine ya chakula unachokifahamu?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 89 9/18/19 4:59 PM

**Tumia**

Utafanya nini ili uwe na afya njema?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kutaja chakula bora; na
ii. kueleza umuhimu wa kula chakula bora.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kuandaa chakula bora**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuainisha vifaa vitakavyotumika kuandaa chakula;
ii. kutaja hatua za kuandaa chakula; na
iii. kushiriki kuandaa na kula chakula walichoandaa.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni mchezo wa Vyakula vyote. Rejea katika shughuli ya 2 katika umahiri mahususi wa kubaini chakula bora.

**Tafakari**

i. Ni aina gani za vyakula vilivyotajwa katika mchezo huu?
ii. Vyakula gani umevipenda zaidi?

**Husisha**

Taja vyakula mnavyokula nyumbani.

**Tumia**

Utafanya nini ili uwe na afya njema?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kueleza namna ya kuandaa chakula bora.

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kula kwa kufuata taratibu**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja nyakati mbalimbali za kula chakula;
ii. kutaja taratibu zinazofaa wakati wa kula;
iii. kula kwa kufuata taratibu zinazokubalika; na
iv. kueleza umuhimu wa kula kwa kufuata taratibu zinazokubalika.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 90 9/18/19 4:59 PM

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni mchezo wa Vyakula vyote. Rejea katika shughuli ya 2 katika umahiri mahususi wa kubaini chakula bora.

**Tafakari**

i. Ni aina gani za vyakula zilizotajwa katika mchezo huu?
ii. Vyakula gani umevipenda zaidi? kwanini?

**Husisha**

Taja vyakula vingine ulivyowahi kula.

**Tumia**

Utafanya nini ili uwe na afya njema?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kutaja taratibu zinazofaa wakati wa kula; na
ii. kula kwa kufuata taratibu zinazokubalika.

**4.2.3.6 Kumwezesha mtoto kubaini magonjwa mbalimbali**

Mwalimu, ili mtoto awe na afya bora na aweze kujikinga na maradhi ni muhimu kumwezesha kujenga uwezo wa kutambua magonjwa, vyanzo vyake na jinsi ya kujikinga.

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kujikinga na magojwa**

Ni muhimu kwa mtoto kujikinga na magonjwa kwa kubaini vyanzo vyake na namna ya kujiepusha na magonjwa hayo.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Igizo dhima, nyimbo, igizo, kisa mafunzo, bungua bongo, maswali na majibu, hadithi, uchunguzi, ziara za mafunzo na michezo

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Kanda za video, bango kitita, picha, vipeperushi, vitabu na chati za picha

**Shughuli ya 1: Kuwaongoza watoto kueleza magonjwa wanayoyafahamu katika Mazingira yao**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja magonjwa waliyowahi kuugua;



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 91 9/18/19 4:59 PM

ii. kuelezea dalili za magonjwa waliyowahi kuugua;
iii. kutaja magonjwa wanayoyafahamu; na
iv. kuigiza dalili za magonjwa mbalimbali.

**Tafakari**

Taja magonjwa unayoyafahamu.

**Husisha**

Taja ugonjwa ambao umewahi kuugua.

**Tumia**

Eleza dalili za ugonjwa wa malaria.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza:

i. kutaja magonjwa; na
ii. kueleza dalili za magonjwa.

**Shughuli ya 2: Kuwaongoza watoto kubaini vyanzo vya magonjwa**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vyanzo vya magonjwa;
ii. kubaini mazingira yanayoweza kusababisha magonjwa; na
iii. kuigiza matendo yanayosababisha magonjwa.

**Tafakari**

Taja vyanzo vya magonjwa ulivyosoma kwenye kitabu.

**Husisha**

Taja sababu inayoweza kusababisha uumwe tumbo.

**Tumia**

Je, utafanya nini ukimkuta rafiki yako anakula tunda bila kuliosha?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kubaini vyanzo vya magonjwa.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kueleza jinsi ya kujikinga na magonjwa**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja njia za kujikinga na magonjwa;
ii. kueleza umuhimu wa kujikinga na magonjwa; na
iii. kuonesha vitendo vya kujikinga na magonjwa.

**Tafakari**

Taja njia za kujikinga na magonjwa ulizoziona katika picha.

**Husisha**

Je, huwa mnafanya nini kabla ya kula chakula mkiwa nyumbani?

**Tumia**

Je, unapaswa kufanya nini ili kujikinga na ugonjwa wa malaria?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kubaini jinsi ya kujikinga na magonjwa.

### 4.2.4 Kumwezesha mtoto kutunza mazingira

Mazingira ni jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka mwanadamu ikiwa ni pamoja na vitu vyenye uhai (mimea na wanyama) na visivyo na uhai. Mtoto akijengewa uwezo wa kutunza mazingira atayajali na kuyathamini. Mwalimu, unapaswa kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kutambua vitu vilivyomo katika mazingira yake, kusafisha mazingira hayo na kuchukua tahadhari anapotumia mazingira husika kwa shughuli mbalimbali.

Mwalimu, kumbuka kuwa katika kumwezesha mtoto kujenga stadi za utunzaji wa mazingira zingatia umri na usalama wa watoto. Umahiri huu umejengwa na umahiri mahususi tatu kama ifuatavyo

#### 4.2.4.1 Kumwezesha mtoto kubaini vitu vilivyomo katika mazingira

Mtoto ataweza kubaini vitu katika mazingira yake ikiwa atajengewa uwezo wa kutambua vitu vilivyomo katika mazingira hayo. Aidha, mtoto anatakiwa kuwa na urazini wa kutunza mazingira ikiwa ni pamoja na kufanya usafi wa mazingira na kubaini vitu vinavyochafua mazingira.

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kubaini vitu vilivyomo katika mazingira**

Mtoto akiwa na uwezo wa kutambua vitu katika mazingira atavithamini na kuvitunza.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Igizo dhima, kazi mradi, maswali na majibu, igizo, nyimbo, uchunguzi, kisa mafunzo, michezo na ziara za mafunzo

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Vitabu, picha, kanda za video, redio, runinga na chati za picha

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kubaini vitu vilivyomo katika mazingira**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitu vilivyomo katika mazingira yanayowazunguka;
ii. kubaini vitu, watu na wanyama katika mazingira; na
iii. kueleza matumizi ya vitu mbalimbali vilivyomo katika mazingira.

**Tafakari**

Taja vitu vilivyomo darasani.

**Husisha**

Je, ni vitu gani vingine unavyovijua ambavyo havipo katika mazingira ya shule?

**Tumia**

Taja vitu vingine unavyoviona katika mazingira ya shule

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama watoto wameweza kubaini vitu mbalimbali vilivyomo katika mazingira.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kuchunguza na kueleza sifa na matumizi ya vitu alivyovichunguza katika mazingira**

Mwalimu waongoze watoto:

i. kueleza sifa za vitu mbalimabali alivyoviona katika mazingira; na
ii. kueleza matumizi ya vitu mbalimbali alivyoviona.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Kuchunguza mazingira

**Mchezo: Kuchunguza mazingira**

Hatua za kufuata:

i. Waelekeze watoto kuwa watatoka darasani kwenda nje kuangalia na kusikiliza vitu vilivyopo katika mazingira.
ii. Kila mtoto azingatie kitu kimoja. Baada ya dakika 10 hivi watoto warudi darasani.
iii. Mwalimu aulize kila mtoto kitu alichoona. Mfano, mwembe, darasa, mti, n.k.
iv. Mwalimu, tenga walioona au kusikia mlio wa gari, walioona mimea, walioona nyumba na walioona wanyama.
v. Waulize sifa na faida za mimea. Mfano: miti, maua na mahindi.
vi. Waulize sifa za magari na faida zake.
vii. Fanya hivyo kwa makundi yote.

**Tafakari**

Mliona nini mlipotoka nje ya darasa?

**Husisha**

i. Je, kitu gani ulichokiona nje ya darasa? Je, ulishawahi kukiona sehemu nyingine?
ii. Mihogo/mahindi yanatumika kupikia nini?

**Tumia**

i. Ukirudi nyumbani utawaeleza wazazi/walezi umejifunza nini leo?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kuchunguza vitu mbalimbali katika mazingira.

**4.2.4.2 Kumwezesha mtoto kujenga stadi za kusafisha mazingira**

Kusafisha mazingira ni kitendo cha kuondoa takataka na vitu visivyohitajika katika eneo husika. Kumwezesha mtoto kujenga stadi za kusafisha mazingira kunahusisha kutambua vifaa vya kufanyia usafi na namna ya kuvitumia katika kusafisha mazingira.

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kujenga stadi za kusafisha mazingira**

Stadi za usafi wa mazingira ni muhimu kwa mtoto kwani zitamwezesha kulinda afya yake na kujikinga na magonjwa.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Nyimbo, uchunguzi, michezo, kisa mafunzo, igizo dhima, igizo, ziara za mafunzo na onesho mbinu

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Chati, picha, kanda za video, vitabu, runinga, redio, maji, fagio, sabuni, reki, kizoleo na pipa la taka

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kubaini vifaa vya kusafishia mazingira.**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vifaa vya kusafishia mazingira;
ii. kuelezea matumizi ya vifaa vya kusafishia mazingira;
iii. kuchora vifaa vya kusafishia mazingira; na
iv. kueleza namna ya kutumia vifaa vya usafi wa mazingira.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Kazi yangu nini?

**Mchezo: Kazi yangu nini?**

Vifaa: Vifaa mbalimbali vya kufanyia usafi na picha zinazoonyesha vitendo mbalimbali vya usafi

Hatua za kufuata:

i. Andaa vifaa mbalimbali vya usafi, chora picha zinazoonesha vitendo mbalimbali vya usafi, kisha weka picha hizo kwenye kasha.
ii. Waweke watoto katika nusu duara.
iii. Weka vifaa vya usafi pamoja na kasha lenye picha mbele ya watoto.
iv. Elekeza kuwa kila mtoto atachukua mchoro wa picha katika kasha na kuelezea wenzake picha hiyo inaonesha nini.
v. Mwambie mtoto aigize tendo hilo kwa kuchukua kifaa kinachostahili na kuwaonesha wenzake namna ya kukitumia kama inavyoonesha kwenye picha.
vi. Hakikisha kila mtoto ameshiriki kikamilifu.

**Tafakari**

i. Ni kifaa gani ulichotumia katika kuonesha namna ya kufanya usafi?
ii. Vifaa gani vingine vilikuwa katika kasha?

**Husisha**

i. Ni vifaa gani ambavyo huwa unatumia nyumbani kufanya usafi?
ii. Ni vifaa gani vingine ambavyo huwa unatumia shuleni kufanya usafi?

**Tumia**

i. Kwa nini tunafanya usafi?
ii. Ukirudi nyumbani ni maeneo gani utapenda kuyasafisha?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kubaini vifaa vya kufanyia usafi wa mazingira.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kusafisha mazingira**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kueleza namna ya kusafisha mazingira;
ii. kueleza vitu vya kuzingatia wakati wa kusafisha mazingira;
iii. kuonesha jinsi ya kusafisha mazingira;
iv. kueleza umuhimu wa kusafisha mazingira; na
v. kusafisha mazingira.

Michezo inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Zoa taka
b. Timu za usafi



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 96 9/18/19 4:59 PM

**a. Mchezo: Zoa taka**

Vifaa: Viroba, kapu, makasha na mifuniko

Hatua za kufuata:

i. Wagawe watoto katika vikundi vya watoto 6-8.
ii. Wagawie kila kikundi vifaa vya kuwekea takataka kama vile kiroba, kapu au mfuko.
iii. Elekeza vikundi vizunguke katika eneo la kuchezea na kuokota karatasi, majani au chupa na kuweka kwenye viroba, kapu au mifuko.
iv. Kikundi kitakachokuwa kimeokota taka nyingi watakuwa washindi.

***Angalizo:*** Hakikisha watoto hawakusanyi takataka nje ya eneo ulilolelekeza. Pia kuwa mwangalifu ili watoto wasikusanye taka hatarishi kama vile vipande vya chupa au vitu vingine vyenye ncha kali.

**Tafakari**

i. Ni aina gani ya takataka ulizoziokota?
ii. Ulijisikiaje kushirikiana na wenzako kuweka takataka katika chombo mlichopewa?
iii. Mlifanya nini kuhakikisha mnaokota takataka nyingi kuliko wengine?

**Husisha**

i. Umewahi kuwasaidia watu kuzoa takataka? Tueleze ilikuwaje.
ii. Vifaa gani huwa unatumia kuzolea takataka?

**Tumia**

Utakapoziona takataka katika maeneo ya shule utaziweka wapi?

**b. Mchezo: Timu za usafi**

Vifaa: Kapu, karatasi, chupa za plastiki na kopo

Hatua za kufuata

i. Wagawe watoto katika timu mbili zilizo sawa.
ii. Weka kapu moja kila upande wa timu katika sehemu ya kuchezea.
iii. Tawanya karatasi na chupa za plastiki au aina nyingine ya taka salama zinazopatikana kwa idadi sawa katika eneo lote la kuchezea.
iv. Eleza na onesha kuwa kapu moja litatumika kwa ajili ya kuwekea karatasi na jingine kwa ajili ya chupa.
v. Gawa timu moja ikusanye chupa na timu nyingine ikusanye karatasi na kuweka kwenye kapu linalostahili.
vi. Mtoto mmoja kutoka kila timu anaruhusiwa kuchukua karatasi au chupa moja kwa wakati mmoja na kuipeleka kwenye kapu la timu husika.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 97 9/18/19 4:59 PM

vii. Utaanzisha mchezo kwa kusema, “Anza” na timu zote zitashindana kukusanya taka haraka na kuziweka kwenye kapu husika.
viii. Mchezo utamalizika watoto watakapomaliza kukusanya taka. Tangaza mshindi kwa watakaowahi kumaliza kuokota takataka zote.

**Tafakari**

i. Je, ni taka zipi ulizoziokota wakati wa kusafisha mazingira?
ii. Je, ni tofauti gani uliyoiona katika eneo la shule baada ya kufanya usafi?

**Husisha**

i. Je, huwa unasaidia kufanya usafi nyumbani?
ii. Ni maeneo gani mengine huwa unafanya usafi?
iii. Je, huwa unatumia vifaa gani unapofanya usafi?

**Tumia**

i. Kwa nini tunasafisha mazingira?
ii. Je, ukiona mazingira ni machafu utafanya nini?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kueleza umuhimu wa kusafisha mazingira; na
ii. kusafisha mazingira.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kubaini matendo yanayosababisha uchafuzi wa mazingira**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuchunguza picha zinazoonesha uchafuzi wa mazingira;
ii. kuigiza matendo yanayosababisha uchafuzi wa mazingira; na
iii. kuelezea madhara ya uchafuzi wa mazingira.

**Tafakari**

i. Ni matendo uliyoigiza yanayosababisha uchafuzi wa mazingira?
ii. Taja madhara ya mazingira machafu

**Husisha**

Ni mahali gani pengine umewahi kuona matendo ya uchafuzi wa mazingira yakifanyika?

**Tumia**

Je, ukimuona mtu anachafua mazingira utafanya nini?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kubaini matendo yanayosababisha uchafuzi wa mazingira.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 98 9/18/19 4:59 PM

#### 4.2.4.3 Kumwezesha mtoto kuchukua tahadhari

Kutambua vitu na maeneo hatarishi katika mazingira kunamwezesha mtoto kuchukua tahadhari. Katika eneo hili mtoto atashirikishwa kusafisha mazingira kwa kuondoa vitu hatarishi, kubainisha alama za tahadhari na kutenda matendo yanayohusisha kuchukua tahadhari.

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kuchukua tahadhari**

Kumwezesha mtoto kuchukua tahadhari kutamsaidia kulinda usalama wake na wa watu wengine.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Nyimbo, uchunguzi, michezo, igizo dhima, ngonjera, onesho mbinu, hadithi, ziara za mafunzo na fikiri-jozisha-shirikisha

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Nyembe, sindano, mikasi, miiba, pini, picha, visu, vimbaka, misumari, moto, vipande vya chupa, mapulizo ya kuokota na vipande vya mabati

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kubaini vitu na maeneo hatarishi katika mazingira**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitu hatarishi katika mazingira;
ii. kutaja maeneo hatarishi katika mazingira;
iii. kueleza athari za vitu na maeneo hatarishi katika mazingira;
iv. kuigiza namna ya kutoa taarifa kuhusu uwepo wa vitu hatarishi katika mazingira; na
v. kuondoa vitu hatarishi katika mazingira kwa tahadhari na kwa kuzingatia usalama.

**Tafakari**

Taja vitu hatarishi ulivyoviona kitabuni.

**Husisha**

Taja vitu vingine hatarishi ambavyo vipo katika mazingira ya nyumbani.

**Tumia**

Je, utafanya nini ili kuepukana na vitu hatarishi?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza:

i. Kubaini vitu na maeneo hatarishi katika mazingira yake; na
ii. Kuondoa vitu hatarishi katika mazingira yake.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 99 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kubaini alama za tahadhari**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuelezea alama za tahadhari wanazozijua;
ii. kuchunguza alama mbalimbali za tahadhari;
iii. kubaini alama za tahadhari; na
iv. kueleza umuhimu wa alama za tahadhari.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Taa ya kijani, taa ya njano, taa nyekundu.

**Mchezo: Taa ya kijani, taa ya njano, taa nyekundu**

Vifaa: Kadi za rangi nyekundu, njano na kijani

Hatua za kufuata:

i. Waeleze watoto wasimame kwenye duara.
ii. Eleza kuwa wataongozwa na ishara tatu:
   - TAA YA KIJANI maana yake tembea.
   - TAA YA NJANO maana yake punguza mwendo.
   - TAA NYEKUNDU maana yake simama.
iii. Wambie watoto wote walioko kwenye duara kugeukia upande wa kulia.
iv. Chagua mtoto mmoja ili awe kiongozi na mpe maelekezo
v. Mwongozaji ataanza kwa kuonyesha kadi ya kijani kisha watoto watatembea kwa kasi. Atakapooneshа kadi ya njano watoto watatembea taratibu. Akionesha kadi Nyekundu, watasimama. Chagua watoto wengine nao waongoze.
vi. Mchezo unamalizika pale unapoona inafaa. Sisitiza kuwa kadi zilizotumika katika mchezo zinawakilisha taa za barabarani.

**Tafakari**

i. Je, umejifunza alama zipi wakati wa mchezo?
ii. Je, ni kadi ipi ilikutaka usimame?
iii. Je, ni kadi ipi ilikutaka kutembea?

**Husisha**

i. Je, ni alama gani nyingine huwa unaziona barabarani?
ii. Je, kuna alama barabarani inayoonesha kuwa sehemu hii kuna shule? Ni alama ipi?

**Tumia**

i. Je, alama hizi zinatufundisha nini?
ii. Je, utafanya nini wakati unataka kuvuka barabara?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kubaini alama za tahadhari.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 100 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kutenda matendo yanayohusisha kuchukua tahadhari**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja matendo ya kuchukua tahadhari katika mazingira;
ii. kueleza umuhimu wa kuchukua tahadhari;
iii. kueleza namna ya kuchukua tahadhari; na
iv. kuigiza vitendo vya kuchukua tahadhari.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Chukua tahadhari.

**Mchezo: Chukua tahadhari**

Vifaa/zana: Mawe madogo, makasha, bango kitita, chaki, kalamu rashasha

Hatua za kufuata:

i. Andaa mawe madogo, kata makasha katika duara nne, chora duara nne na mengine kwenye bango kitita na duara nne ardhini.
ii. Wapange watoto katika makundi manne.
iii. Kila kundi hakikisha lina duara, duara la kasha lililoandikwa 'matope', duara la bango kitita lipakwe rangi nyekundu na liandikwe moto na duara la ardhini liwekewe mawe madogo.
iv. Ongeza kuchora duara tatu kila kikundi kwa mstari uliopinda yaani duara kavu, duara la moto, duara kavu, duara la tope na kasha kavu.
v. Elekeza watoto kuruka na kukanyaga sehemu kavu ( ndiyo sehemu salama). Agiza wasikanyage moto, tope, wala mawe ni hatari.
vi. Rudia makundi yote ya watoto ili waweze kushiriki katika mchezo.
vii. Mchezo utamalizika utakapoona inafaa.

**Tafakari**

i. Je, ungekanyaga moto ungefanya nini?
ii. Je, ungekanyaga matope ungefanya nini?

**Husisha**

i. Je, moto una madhara gani?
ii. Kwa nini ni vizuri kuwa waangalifu tunapotembea?

**Tumia**

i. Je, utachukua tahadhari gani ukiona moto.
ii. Je, utafanya nini ili matope yasikuchafue.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 101 9/18/19 4:59 PM

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kuonesha namna ya kuchukua tahadhari.

### 4.2.5 Kumwezesha mtoto kumudu stadi za kisanii

Sanaa ni jumla ya shughuli zote zinazotendwa na mwanadamu kwa ufundi/ubunifu na kwa kuzingatia ujumi unaojitokeza ili kuleta uhalisia. Eneo hili limejikita katika utendaji, hivyo mtoto awezeshwe kuwa na mpangilio, kufuata utaratibu na kuwa mbunifu katika kutumia fursa zilizopo zitakazomwezesha kuwa mtendaji wa shughuli za kisanii. *Mwalimu, utamwezeshaje mtoto kujenga stadi za kisanii?* Pamoja na majibu yako, unapaswa kuwawezesha watoto kumudu sanaa za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mikono na mwili na kumudu sanaa za ubunifu wa sauti.

Mwalimu, kumbuka kuwa ni muhimu kuzingatia mahitaji ya watoto pamoja na usafi, usalama na mpangilio katika kazi za watoto. Umahiri huu umejengwa na umahiri mahususi tatu kama ifuatavyo:

#### 4.2.5.1 Kumwezesha mtoto kujenga stadi za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mikono

Sanaa za utendaji wa mikono zinalenga katika kupata maumbo mbalimbali yenye ujumi unaojitokeza. Mwalimu, waongoze watoto kutambua maumbo mbalimbali ya vitu, kutofautisha rangi mbalimbali, kuchunguza na kuelezea vitu, kuumba maumbo mbalimbali, kuchora na kupaka rangi, kuunda vitu mbalimbali, kutengeneza vifani, kutunga vitu katika uzi/kamba, kusuka pamoja na kutia nakshi.

**Umuhimu wa kujenga stadi za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mikono**

Watoto waliojengewa stadi za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mikono huwa ni wepesi kutenda, kuiga na kubuni kazi mbalimbali za sanaa huku wakitambua na kuthamini mazingira yao kama nyenzo kuu.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Changanya kete, matembezi ya galari, nyimbo, oneshombinu, michezo, hadithi, kazi mradi, visa mafunzo, fikiri-jozisha shirikisha na kualika mgeni

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Maji/unga, mimea, brashi, magome ya miti, mbegu za mimea, udongo wa mfinyanzi, plastisini/kinyunya, ngoma, stenseli, shanga, nyuzi, kamba za katani, ukindu



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 102 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kubaini sanaa za utendaji wa mikono**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja kazi za sanaa zilizotengenezwa kwa mikono zinazopatikana katika mazingira yao;
ii. kuchunguza kazi za sanaa zilizoandaliwa; na
iii. kueleza namna sanaa tofauti za utendaji wa mikono zilivyotengenezwa.

**Tafakari**

Taja vitu vya sanaa vinavyohusisha utendaji wa mikono ulivyoviona katika kitabu.

**Husisha**

Taja vitu vingine ulivowahi kuviona vimetengenezwa kwa kutumia mikono.

**Tumia**

Je, utaweza kutengeneza kitu gani ukirudi nyumbani?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji ili kuona kama kila mtoto ameweza kubaini sanaa zinazotengenezwa kwa mikono.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kuumba maumbo ya vitu mbalimbali**

Mwalimu waongoze watoto:

i. kubaini makunzi yafaayo kwa ajili ya ufinyanzi;
ii. kukusanya makunzi ya ufinyanzi;
iii. kuchunguza vitu vilivyofinyangwa; na
iv. kufinyanga maumbo mbalimbali kwa kutumia makunzi stahiki.

**Tafakari**

Taja makunzi yanayotumika kufinyanga vitu ulivyoviona.

**Husisha**

Taja vifaa vinavyotumika nyumbani ambavyo vimefinyangwa.

**Tumia**

Kitu ulichofinyanga kinatumika kufanyia nini?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji ili kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kubaini makunzi yanayofaa kwa ajili ya ufinyanzi; na
ii. kufinyanga maumbo mbalimbali kwa kutumia makunzi stahiki.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 103 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kubainisha rangi katika vitu**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja rangi mbalimbali;
ii. kutaja rangi za msingi;
iii. kuonesha rangi nyekundu, bluu na njano; na
iv. kuchora picha na kupaka rangi.

Michezo inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Tafuta rangi yako
b. Kuhusisha rangi

**a. Mchezo: Tafuta rangi yako**

Vifaa: Vitu vyenye rangi mbalimbali (Nyekundu, nyeusi, nyeupe, bluu, njano na kijani)

Hatua za kufuata:

i. Waeleze watoto kuwa mchezo huu unahusu rangi.
ii. Wagawe watoto katika vikundi vya watoto kati ya sita na nane.
iii. Waambie watoto wataje rangi mbalimbali wanazozijua.
iv. Weka vitu vya rangi mbalimbali katika kila kikundi.
v. Taja rangi yoyote iliyopo darasani, kisha elekeza kuwa mtoto mmoja mmoja kutoka katika kila kikundi, atapata nafasi ya kugusa/kuchukua kitu chochote chenye rangi iliyotajwa. Chunguza kama watoto wameweza kutambua rangi uliyoitaja.
vi. Hakikisha kila mtoto ameshiriki kikamilifu katika mchezo huu.

**Tafakari**

i. Wakati wa mchezo, ni rangi gani uliyoigusa?
ii. Je, rangi gani ilikuwa ngumu kuitambua?
iii. Je, rangi gani ilikuwa rahisi kuitambua?

**Husisha**

i. Je, ni rangi zipi ulizokuwa unazifahamu kabla?
ii. Je, nywele zako zina rangi gani?
iii. Je, ni vitu gani vingine ulivyonavyo nyumbani vyenye rangi sawa na ulizoziona leo?

**Tumia**

Tunatumia rangi kufanya kazi gani?

**b. Mchezo: Kuhusisha rangi**

Vifaa: Kadi za rangi



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 104 9/18/19 4:59 PM

Hatua za kufuata:

i. Simama na watoto katika duara. Waoneshe kadi za rangi Nyekundu, Bluu na Njano (rangi za msingi). Hakikisha watoto wote wametambua rangi hizo.
ii. Waeleze kuwa kila rangi inawakilisha kitendo fulani. Mfano Nyekundu maana yake ruka ruka, Bluu maana yake tembea, Njano maana yake piga makofi.
iii. Fanya mazoezi katika kila rangi ili kuhakikisha watoto wanaelewa kila rangi inawakilishwa na kitendo gani.
iv. Wagawe watoto katika vikundi vitatu, kisha kila kikundi kichague kiongozi.
v. Wape viongozi wa vikundi kadi zote tatu za rangi.
vi. Kiongozi wa kikundi aoneshe kadi moja baada ya nyingine na wenzake wafanye vitendo vinayoendana na rangi hizo.
vii. Kiongozi wa kwanza akimaliza kuonesha kadi zote tatu, chagua mtoto mwingine awe kiongozi.
viii. Hakikisha kila mtoto anashiriki kikamilifu.
ix. Ongeza rangi zaidi na vitendo zaidi baada ya kuelewa rangi tatu za mwanzo.

**Tafakari**

i. Je, umeweza kufanya vitendo vyote kulingana na rangi husika?
ii. Taja rangi ulizoziona wakati wa mchezo?
iii. Je, unapenda rangi gani kati ya hizo ulizoziona? Kwa nini?

**Husisha**

Ni vitu gani vingine unavyovifahamu vyenye rangi ya njano, nyekundi na bluu?

**Tumia**

Taja matumizi ya rangi.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji ili kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kutaja rangi mbalimbali; na
ii. kuonyesha vitu vyenye rangi mbalimbali

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kuchora picha na maumbo na kupaka rangi**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kubaini vifaa vya uchoraji na vya kupaka rangi vinavyopatikana katika mazingira yake;
ii. kutaja vitu anavyotaka kuchora na kuvipaka rangi;
iii. kuchora picha mbalimbali;



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 105 9/18/19 4:59 PM

iv. kuelezea kitu alichochora;
v. kueleza namna ya kupaka rangi; na
vi. kupaka rangi kwa kufuata hatua.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Kuokota kadi

**Mchezo: Kuokota kadi**

Vifaa: Kadi za maumbo bapa

Hatua za kufuata:

i. Andaa vipande vikubwa vya karatasi na tengeneza kadi nyingi za picha zenye maumbo mbalimbali kama vile pembe nne (mraba), duara na pembetatu.
ii. Wagawe watoto katika vikundi.
iii. Gawa idadi sawa ya kadi za picha za maumbo pamoja na karatasi ya kuandikia kwa kila kikundi.
iv. Waelekeze watoto wafunike kadi hizo.
v. Mtoto mmoja baada ya mwingine aokote kadi na kuifunua, awaulize watoto wenzake amepata picha ya umbo gani.
vi. Waelekeze kila mtoto achore kwenye karatasi picha ya umbo alilookota na ashirikishe wenzake picha aliyochora.
vii. Himiza kila mtoto aweze kushiriki.

**Tafakari**

i. Je, umechora picha gani?
ii. Picha ya umbo gani ilikuwa rahisi kuchora?

**Husisha**

i. Je, ni vitendo gani vingine huwa unavitenda kwa kutumia mikono yako?
ii. Je, ni rangi gani nyingine unayoifahamu?

**Tumia**

i. Utatumia vifaa gani kuchora maumbo?
ii. Utachora umbo gani lingine?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji ili kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kuchora picha mbalimbali; na
ii. kuelezea kitu alichochora.

**Shughuli ya 5: Kuwawezesha watoto kuunda vitu mbalimbali**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitu mbalimbali vilivyoundwa:
ii. kubaini makunzi yaliyotumika kuunda vitu hivyo:
iii. kuelezea namna ya kuunda maumbo mbalimbali:
iv. kuunda vitu kwa kutumia makunzi yaliyotayarishwa; na
v. kukusanya makunzi ya kuundia maumbo mbalimbali.

**Tafakari**

Taja vitu mlivyoviona ambavyo vimeundwa kwa mikono.

**Husisha**

Taja makunzi mengine unayoweza kutumia kuunda kifani cha gari.

**Tumia**

Unaweza kutumia vitu gani kutengeneza kifani cha nyumba?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kuunda maumbo mbalimbali kwa kutumia makunzi stahiki.

**Shughuli ya 6: Kuwawezesha watoto kutunga vitu katika uzi/kamba**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitu vinavyoweza kutungwa;
ii. kuonesha namna ya kutunga vitu mbalimbali; na
iii. kutunga vitu katika uzi/kamba.

**Tafakari**

i. Taja vitu vinavyoweza kutungwa unavyovifahamu.
ii. Umetunga kitu gani katika zoezi tulilofanya?

**Husisha**

Umewahi kutunga vitu gani vingine mbali na tulivyotunga leo?

**Tumia**

Ukifika nyumbani utamtajia mama vitu gani ulivyotunga shuleni?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutunga vitu katika uzi/ kamba.

**Shughuli ya 7: Kuwawezesha watoto kutia nakshi katika vitu mbalimbali**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kubaini vitu vilivyotiwa nakshi;
ii. kutaja vitu vinavyoweza kutiwa nakshi;
iii. kutayarisha vitu vinavyotakiwa kutiwa nakshi;
iv. kueleza namna wanavyotia nakshi katika vitu mbalimbali; na
v. kutia nakshi.

**Tafakari**

Taja kitu ulichotia nakshi.

**Husisha**

Taja vitu vilivyotiwa nakshi mnavyotumia nyumbani.

**Tumia**

Taja kitu unachoweza kukichora na kutia nakshi.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutia nakshi katika vitu.

**Shughuli ya 8 : Kuwawezesha watoto kusuka vitu mbalimbali**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kubaini vitu vilivyosukwa;
ii. kubaini makunzi yatakayotumika katika ususi;
iii. kuonesha namna ya kusuka vitu mbalimbali; na
iv. kusuka vitu kwa kufuata hatua.

**Tafakari**

i. Taja makunzi yanayotumika kusuka mkeka.
ii. Taja kitu ulichosuka.

**Husisha**

Taja vitu vingine unavyoweza kusuka.

**Tumia**

Utamsaidiaje rafiki yako asiyejua kusuka ukili?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kusuka vitu mbalimbali.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 108 9/18/19 4:59 PM

### 4.2.5.2 Kumwezesha mtoto kujenga stadi za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mwili

Sanaa za utendaji wa mwili hukuza uwezo wa mtoto kufikiri na kufanya shughuli zake kwa umakini. Sanaa hizi huwafanya watoto kuwa wepesi katika kutenda kwa kutumia viungo vyao vya mwili. Katika kufanikisha jambo hili, unapaswa kuwaongoza watoto kufanya mazoezi ya kuvuta pumzi, mijongeo mbalimbali, kucheza michezo mbalimbali na kulenga shabaha.

**Umuhimu wa Kumwezesha mtoto kujenga stadi za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mwili**

Ubunifu katika sanaa za utendaji wa mwili ni muhimu katika kumsaidia mtoto kuimarisha afya yake na kujifunza kwa wepesi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Onesho mbinu, ziara za mafunzo, michezo, maswali na majibu, hadithi, kazi mradi na maigizo

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Mipira, kamba, vibao fumbo, bembea, gololi, tiara, viunzi, matairi, vijiti, upinde na mishale, vitufe, ngoma, manati na kombeo na picha za wanyama wenye mijongeo tofauti

**Shughuli ya 1: Kuwaongoza watoto kubaini sanaa zinazohusisha utendaji wa mwili**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja sanaa za utendaji wa mwili;
ii. kuonesha namna sanaa hizo zinavyotendwa; na
iii. kueleza umuhimu wa sanaa zinazohusisha utendaji wa mwili.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Kuwa mrefu, mdogo na mkubwa.

**Mchezo: Kuwa mrefu, mdogo na mkubwa**

Hatua za kufuata:

i. Waelekeze watoto wasimame eneo la wazi walau umbali wa mkono mmoja kutoka mtoto mmoja hadi mwingine wakikutazama.
ii. Eleza na onesha kwa vitendo namna ya kufanya:
   - Kusimama kwa vidole vya miguu na kunyoosha mikono juu. Hii itaashiria mrefu kama twiga.
   - Kuchuchumaa, kukumbatia miguu na kuinamisha kichwa kwenye magoti. Hii inaashiria mdogo kama sungura.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 109 9/18/19 4:59 PM

- Kutanua mikono na miguu kwa kadiri wawezavyo, hii inaashiria mkubwa kama tembo.

iii. Fananisha matendo unayoyafanya na vitu halisi. Mfano kuwa mrefu kama mti, twiga au mnara; kuwa mdogo kama sungura, kuwa mkubwa kama tembo.

iv. Anza kutoa maelekezo kwa watoto watende kama unavyotenda. Katika kila kitendo, hakikisha watoto wataganda angalau sekunde sita hadi nane.

v. Himiza kila mtoto ashiriki kikamilifu.

**Tafakari**

i. Je, umetumia viungo gani vya mwili wakati wa mazoezi?

ii. Je, umepata ugumu gani wakati wa kufanya mazoezi?

**Husisha**

i. Je, umewahi kufanya mazoezi mengine tofauti na haya?

ii. Ni kitu gani kingine umewahi kukiona ambacho ni kirefu?

**Tumia**

i. Ni sehemu gani nyingine tunaweza kufanyia mazoezi?

ii. Ni nani mwingine utafanya naye mazoezi?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kubaini sanaa za utendaji wa mwili.

**Shughuli ya 2: Kuwaongoza watoto kufanya mazoezi ya kuvuta pumzi**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuonesha namna tofauti ya uvutaji wa pumzi;

ii. kufanya mazoezi ya kuvuta pumzi; na

iii. kueleza umuhimu wa mazoezi ya kuvuta pumzi.

**Tafakari**

Taja namna za kuvuta pumzi mlizozifanya

**Husisha**

Je, umewahi kufanya mazoezi ya kuvuta pumzi sehemu nyingine?

**Tumia**

Unawezaje kuvuta pumzi ukiwa unakimbia?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini iwapo kila mtoto ameweza kuvuta pumzi kwa namna tofauti.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 110 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kufanya mazoezi ya mijongeo**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja mijongeo mbalimbali ya mwili;
ii. kuonesha namna mijongeo hiyo inavyofanyika;
iii. kufanya mazoezi ya mijongeo mbalimbali ya mwili; na
iv. kufanya mijongeo mbalimbali ya wanyama kama bata, chura, kinyonga.

**Tafakari**

Taja mijongeo ya mwili uliyoiona kitabuni

**Husisha**

Taja mijongeo mingine ya mwili ambayo umewahi kuifanya ukiwa nyumbani.

**Tumia**

Je, unawezaje kutofautisha aina za mijongeo?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kufanya mijongeo mbalimbali ya mwili.

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kulenga shabaha**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja michezo ya kulenga shabaha;
ii. kutaja vifaa vinavyotumika katika michezo hiyo;
iii. kuonesha namna ya kucheza michezo ya kulenga shabaha; na
iv. kucheza michezo ya kulenga shabaha.

**Tafakari**

i. Taja michezo ya kulenga shabaha uliyojifunza.
ii. Taja vifaa ulivyotumia wakati wa kulenga shabaha.

**Husisha**

Taja michezo mingine ya kulenga shabaha uliyokuwa unaifahamu kabla ya kujifunza.

**Tumia**

Utamsaidiaje rafiki yako ili aweze kulenga shabaha?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kucheza michezo ya kulenga shabaha.

**Shughuli ya 5: Kuwawezesha watoto kucheza michezo mbalimbali**

Mwalimu, waongoze watoto:


Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 111 9/18/19 4:59 PM

i. kutaja michezo inayochezwa katika mazingira yao;
ii. kuainisha vifaa vinavyotumika wakati wa kucheza michezo hiyo;
iii. kuonesha namna michezo hiyo inavyochezwa;
iv. kubainisha michezo mingine na vifaa vyake; na
v. kucheza michezo mbalimbali kwa kufuata taratibu.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Kuvuta kamba

**Mchezo: Kuvuta kamba**

Vifaa: Kamba

Hatua za kufuata:

i. Watoe watoto nje ya darasa.
ii. Wagawe katika timu mbili kulingana na idadi yao darasani.
iii. Chora mstari ardhini unaogawa eneo la kuchezea katika sehemu mbili.
iv. Weka alama inayoonekana katikati ya mstari.
v. Weka alama inayogawa kamba katika sehemu mbili zilizo sawa.
vi. Waelekeze namna ya kuvuta kamba pamoja kila timu kuelekea upande wao.
vii. Waelekeze watoto waanze kuvuta kamba kuelekea upande wao.
viii. Wahimize watoto wa pande zote mbili kuvuta kamba.
ix. Upande mmoja ukivutwa ukavuka alama utakuwa mwisho wa mchezo.

**Tafakari**

i. Je, timu yako ilifanya nini kuhakikisha inashinda?
ii. Je, ulijisikiaje baada ya timu yako kushinda katika mchezo wa kuvuta kamba? Kwa nini?
iii. Je, ulijisikiaje baada ya timu yako kushindwa katika mchezo wa kuvuta kamba?
iv. Unadhani nini kingetokea kama ungevuta kamba peke yako?

**Husisha**

i. Ni michezo gani mingine huwa unacheza na wenzako?
ii. Tofauti na michezo, je, kazi gani nyingine huwa unafanya na wenzako unapokuwa nyumbani?

**Tumia**

i. Kwa nini ni vizuri kucheza na wenzako?
ii. Kwa nini ni vizuri kufanya kazi pamoja?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kucheza michezo mbalimbali.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 112 9/18/19 4:59 PM

### 4.2.5.3 Kumwezesha mtoto kumudu stadi za ubunifu wa sauti

Kumudu stadi za ubunifu wa sauti humsaidia mtoto kujifunza kuhusu milio ya vitu na sauti za viumbe mbalimbali. Mwalimu, huna budi kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kuimba nyimbo, kutamba ngonjera, kughani mashairi, kuigiza sauti na milio, kuchekesha na kusimulia hadithi.

**Umuhimu wa kuwawezesha watoto kumudu stadi za ubunifu wa sauti**

Ubunifu wa sauti ni muhimu katika kumwezesha mtoto kutumia ala za sauti katika kukuza stadi za kuzungumza na kuimba.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Onesho mbinu, nyimbo, visa mafunzo, kualika mgeni, majadiliano, ziara za mafunzo, michezo, maswali na majibu, hadithi na kazi mradi

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Ngoma, filimbi, njuga, manyanga, kayamba, kinanda, zeze, tarakilishi, runinga, vinasa sauti na vipaza sauti, marimba, vuvuzela

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kuimba nyimbo**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja nyimbo wanazozifahamu;
ii. kubaini vifaa vitakavyotumika wakati wa kuimba;
iii. kuimba nyimbo na kuigiza matendo mbalimbali yanayoendana na nyimbo hizo; na
iv. kueleza ujumbe unaotokana na nyimbo walizoimba.

Nyimbo zinazopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Bendera yetu
b. Bendera yetu yapepea
c. Shule yetu ni nzuri
d. Shule naipenda shule
e. Kijani kibichi cha Mtanzania

**a. Bendera yetu**

*Bendera yetu sasa ina rangi nne*
*Nyeusi sisi wenyewe*
*Kijani mazao yetu*
*Bluu bahari yetu*
*Njano madini yetu*



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 113 9/18/19 4:59 PM

**b. Bendera yetu yapepea**

*Bendera yetu yapepea Tanzania*
*Ina rangi ya bluu,*
*nyeusi, kijani na njano*
*Nyimbo za shule yetu*

**c. Shule Yetu ni nzuri**

S*hule yetu ni nzuri imepambwa maua*
*Ukienda hovyo hovyo utayumba yumba wee*
*Mazingira mazuri yanayopendeza*,
*Ukienda hovyo hovyo utayumba yumba wee*

**d. Shule naipenda shule**

*Shule naipenda shule aa x2*
*Na macho yangu mawili ya kusomea kitabu, shule aa*
*Shule naipenda shule aa*
*Miguu yangu miwili ya kuendea shuleni, shule aa*
*Shule naipenda shule aa*
*Mikono yangu miwili ya kushikia kitabu, shule aa*
*Kiuno changu chembamba cha kuvalia mkanda, shule aa*

**e. Kijani kibichi cha mtanzania**

*Kijani kibichi cha Mtanzania,*
*shule yetu ina raha weee,*
*Ilivyokaa juu ya mlima,*
*huku na kule mteremko,*
*Tushangilie eeeeeeh,*
*tufurahie eeeeeh,*
*Shule yetu inaraha eeeeeeh,*

**Tafakari**

i. Bendera yetu ina rangi ngapi? Taja rangi hizo.
ii. Mlipokuwa mnaimba, mlikuwa mnataja maneno gani?

**Husisha**

i. Taja nyimbo nyingine ambazo mmewahi kuimba
ii. Rangi zilizopo kwenye bendera yetu, unaweza kuziona kwenye vitu gani vingine?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 114 9/18/19 4:59 PM

**Tumia**

Ukifika nyumbani utamwimbia nani wimbo? Wimbo gani? Imba.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kuimba nyimbo.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kutamba ngonjera**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja ngonjera wanazozifahamu;
ii. kujifunza ngonjera zilizoandaliwa;
iii. kutamba ngonjera; na
iv. kuelezea ujumbe unaotokana na ngonjera.

**Tafakari**

Ngonjera uliyoiimba inahusu nini?

**Husisha**

Ni mahali gani pengine umewahi kusikia wakitamba ngonjera?

**Tumia**

Je, utamsaidiaje mtoto asiyeweza kutamba ngonjera?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutamba ngonjera.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kughani mashairi**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja mashairi wanayoyafahamu;
ii. kujifunza mashairi ya watoto yaliyoandaliwa;
iii. kughani mashairi; na
iv. kuelezea ujumbe unaotokana na mashairi.

**Tafakari**

i. Taja shairi tulilojifunza leo.
ii. Taja ujumbe wa shairi tuliloimba leo.

**Husisha**

Taja mashairi mengine uliyowahi kuimba.

**Tumia**

Utamsaidiaje mwenzako ili aweze kuimba shairi.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kughani mashairi.

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kuigiza sauti na milio**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja sauti na milio mbalimbali wanayoifahamu;
ii. kubaini sauti na milio mbalimbali wanayoisikia; na
iii. kuigiza sauti na milio mbalimbali.

Wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni wimbo wa Hii sauti ya nini? Rejea katika shughuli ya 2 katika umahiri mahususi wa kusikiliza.

**Tafakari**

i. Ni maneno gani uliyoyasikia wakati ukiimba?
ii. Ni wanyama/ndege gani umewasikia kwenye wimbo?

**Husisha**

Ni sauti gani zingine za wanyama umewahi kuzisikia?

**Tumia**

Igiza milio tofauti tofauti unayoifahamu.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kuigiza sauti na milio mbalimbali.

**Shughuli ya 5: Kuwawezesha watoto kufanya vichekesho**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vichekesho wanavyovifahamu;
ii. kuigiza matendo ya kuchekesha; na
iii. kueleza umuhimu wa vichekesho.

**Tafakari**

Ni matendo gani yalikufanya ukacheka wakati mnacheza?

**Husisha**

Taja matendo mengine umewahi kuyaona yakakufanya ukacheka?

**Tumia**

Utamsaidiaje rafiki yako ambaye hapendi kufurahi?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kufanya matendo ya kuchekesha.

**Shughuli ya 6: Kuwawezesha watoto kusimulia hadithi**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja hadithi wanazozifahamu;
ii. kusimulia hadithi fupifupi;
iii. kutaja wahusika katika hadithi; na
iv. kuelezea ujumbe unaotokana na hadithi iliyosimuliwa.

**Tafakari**

Taja wahusika katika hadithi uliyosimulia

**Husisha**

Taja hadithi nyingine ambayo umewahi kusimuliwa.

**Tumia**

Ukifika nyumbani utawasimulia rafiki zako hadithi gani?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kusimulia hadithi.

### 4.2.6 Kumwezesha mtoto kutumia dhana za kihisabati

Dhana za kihisabati hutumika katika maisha ya kila siku. *Mwalimu, utamwezeshaje mtoto kumudu dhana za kihisabati?* Pamoja na majibu uliyonayo, unatakiwa kumwezesha mtoto kujenga dhana za kihisabati zinazojumuisha matendo ya kuhesabu, kupanga, kuoanisha, kuunganisha, kutambua mahusiano ili kufanya kazi za namba, maumbo, nafasi na vipimo. Mwalimu katika eneo hili wawezeshe watoto kuainisha vitu mbalimbali katika mazingira, kufahamu dhana ya wakati, kumudu stadi za vipimo na kujenga dhana ya namba.

Dhana za kihisabati zinahusisha uwezo wa mtoto kufikiri na kutenda. Mwalimu zingatia upatikanaji wa vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia zitokanazo na mazingira husika, bila kusahau matumizi ya TEHAMA. Zana hizo zimwezeshe mtoto kujenga dhana za kihisabati.

#### 4.2.6.1 Kumwezesha mtoto kutumia mazingira kujenga dhana ya namba

Mwalimu, ni muhimu kutambua kuwa mazingira ya mtoto yana nafasi kubwa katika ujifunzaji wa dhana za kihisabati. Mwalimu unatakiwa kumwezesha mtoto kutambua vitu katika mazingira kupitia shughuli mbalimbali kama vile kutambua rangi, kupanga vitu kulingana na sifa na kucheza michezo ya kufananisha vitu kwa sifa zake. Umahiri huu umejengwa na umahiri mahususi nne kama ifutavyo:



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 117 9/18/19 4:59 PM

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kuainisha vitu katika mazingira**

Mtoto akiweza kutambua na kuainisha vitu vilivyomo katika mazingira yake atakuwa na urazini wa kuyatumia mazingira yake katika ujifunzaji wa dhana za kihisabati.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Ziara za mafunzo, kualika mgeni, hadithi, michezo, onesho mbinu, kazi mradi na majaribio

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Rangi tofauti za maji/unga, rangi zinazotokana na mimea, vihesabio, vibao fumbo, magome ya miti, mbegu za mimea, udongo wa mfinyanzi/plastisini, ngoma na picha

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kuainisha vitu vinavyojenga dhana za kihisabati katika mazingira yanayowazunguka**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitu mbalimbali wanavyovijua;
ii. kuchunguza vitu vilivyoko ndani na nje ya darasa;
iii. kutaja vitu walivyoviona; na
iv. kuelezea vitu walivyoviona.

Mchezo na nyimbo zinazopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Shule yetu ni nzuri
b. Mchezo wa kadi

**a. Wimbo: Shule yetu ni nzuri**

Hatua za kufuata:

i. Waongoze watoto kusimama wakiwa nje au ndani ya darasa.
ii. Anza kuimba wimbo watoto wakikusikiliza.
iii. Imba mstari mmoja baada ya mwingine huku wakikufuatisha.
iv. Waongoze watoto kuimba wimbo wote.

*Shule yetu ni nzuri imepambwa maua*
*Ukienda hovyo hovyo utayumba yumba wee x2*
*Shule yangu ni nzuri imeoteshwa miti, Ukienda hovyo hovyo utayumba yumba wee x2*

*Shule yangu ni nzuri kuna meza na viti, Ukienda hovyo hovyo utayumba yumba wee x2*

**b. Mchezo wa kadi**

Hatua za kufuata:

i. Andaa kadi kulingana na mahitaji ya darasa lako. Kadi hizo ziwe na picha za vitu mbalimbali vinavyopatikana katika mazingira yao.
ii. Wagawe watoto katika vikundi kulingana na idadi ya watoto ulio nao.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 118 9/18/19 4:59 PM

iii. Waongoze watoto kuchagua kiongozi katika kila kikundi.
iv. Gawa kadi katika kila kikundi.
v. Elekeza viongozi wa vikundi wafunike kadi hizo.
vi. Mtoto mmoja mmoja katika kila kikundi aokote kadi kisha aelezee ameokota picha ya nini.
vii. Hakikisha kila mtoto ameshiriki kikakimilifu.

**Tafakari**

Je ni picha gani ulizoziona katika kadi?.

**Husisha**

Picha za vitu ulivyoviona kwenye kadi ulishaviona tena? Uliviona wapi?

**Tumia**

Utamsaidiaje mtoto mwenzako ambaye ameshindwa kuelezea picha yake?.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kubainisha vitu katika mazingira vinavyojenga zana za kihisabati.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kubaini maumbo mbalimbali**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja maumbo mbalimbali wanayoyafahamu;
ii. kuchunguza picha za maumbo mbalimbali;
iii. kubainisha maumbo ya pembe tatu, pembe nne (mraba) na duara;
iv. kubainisha vitu vyenye maumbo ya pembe tatu, pembe nne (mraba) na duara katika mazingira waliyopo;
v. kuchora maumbo na kupaka rangi maumbo hayo; na
vi. kupanga maumbo kwa mfuatano unaofanana.

Michezo inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Kopo la maumbo
b. Ipe umbo

**a. Mchezo: Kopo la maumbo**

Vifaa: Karatasi, manila, makopo

Hatua za kufuata:

i. Chora maumbo mengi ya duara, pembetatu na mraba katika karatasi ya manila,



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 119 9/18/19 4:59 PM

kisha yakate na kuyatunza katika chombo kimoja.

ii. Weka makopo matatu mbele ya watoto na kila kopo liwakilishe umbo moja. Unaweza kuchora picha ya umbo hilo kwenye karatasi na kubandika katika kopo au kuweka vitu halisi vinavyofanana na maumbo hayo karibu na makopo.
iii. Elekeza kila mmoja kuja mbele kuchukua umbo moja katika chombo, awaoneshe wenzake na kuliweka katika kopo la umbo husika. Iwapo mtoto atashindwa, apewe nafasi nyingine ya kujaribu.

**Tafakari**

i. Je, umeona maumbo mangapi? Je, unaweza kuyataja?
ii. Je, ilikuwa rahisi kutambua umbo ulilotakiwa kuchukua?

**Husisha**

i. Je, umbo ulilochagua linafanana na kitu gani?
ii. Je, chungwa linafanana na umbo gani?

**Tumia**

Je, unaweza kuwaonesha watoto wengine namna ya kutengeneza umbo kwa kutumia mwili?

**b. Mchezo: Ipe umbo**

Vifaa: Vitu vyenye maumbo mbalimbali.


Hatua za kufuata:

i. Waoneshe watoto vitu vyenye maumbo mbalimbali.
ii. Anza kwa kuelekeza watoto namna unavyounda umbo kwa kutumia mwili wako.
iii. Wagawe watoto katika vikundi kulingana na maumbo uliyoyachora.
iv. Taja jina la umbo, kisha kila kikundi husika kiunde umbo hilo kwa kutumia miili yao. Wanaweza kufanya hivyo kwa kusimama au kulala chini.
v. Hakikisha watoto wote wanashiriki na wanaunda umbo kwa usahihi.
vi. Hakikisha kila kikundi kinaunda kila aina ya umbo kupata uelewa wa maumbo hayo.

Angalia kielelezo kifuatacho kwa ufafanuzi zaidi kwa mchezo huu:



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 120 9/18/19 4:59 PM



**Tafakari**

i. Je, ni umbo gani lilikuwa rahisi kuliunda?
ii. Je, ni umbo gani lilikuwa gumu kuliunda?

**Husisha**

Je, ni vitu gani vingine vinafanana na maumbo mliyoyaunda?

**Tumia**

Je, unaweza kuunda maumbo haya kwa kutumia vitu vingine? Vitu gani?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kubaini na kuunda maumbo mbalimbali.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kubainisha vitu kulingana na sifa zake**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kukusanya vitu mbalimbali;
ii. kubainisha vitu walivyokusanya;
iii. kupanga vitu hivyo kulingana na sifa zake; na
iv. kucheza michezo ya kupanga na kupangua vitu.

Mchezo unaopendekezwa kufundisha na kujifunzia katika shughuli hii ni Sifa za mtu

**Mchezo: Sifa za mtu**

Hatua za kufuata:

i. Andaa eneo nje ya darasa ambalo ni salama kwa watoto.
ii. Tawanya vitu vya aina mbalimbali katika eneo hilo.
iii. Wagawe watoto katika makundi kulingana na idadi ya watoto.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 121 9/18/19 4:59 PM

iv. Andaa vyombo kulingana na makundi hayo.
v. Waongoze watoto katika makundi yao kukusanya vitu hivyo na kundi liweke kwenye chombo chake.
vi. Waongoze watoto katika vikundi vyao kupanga vitu walivyokusanya kulingana na sifa zake.
vii. Zungukia kila kikundi pale wanapohitaji msaada.

**Tafakari**
Ni vitu gani ulivyoviokota?. Taja vitu hivyo.

**Husisha**
Je, vitu ulivyoviokota uliwahi kuviona tena? Uliviona wapi.

**Tumia**
Siku nyingine ukiwa unacheza mchezo huu utafanya nini ili uokote vitu vingi zaidi.

**Upimaji**
Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kupanga vitu kulingana na sifa zake.

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kupanga vitu kwa mfuatano unaofanana**
Mwalimu, waongoze watoto:
i. kutaja rangi za vitu mbalimbali;
ii. kupanga vitu katika makundi ya rangi zinazofanana;
iii. kutaja rangi za vitu walivyonavyo; na
iv. kupanga vitu kwa mfuatano unaofanana.

**Tafakari**
Taja vitu mlivyovipanga kwenye kikundi chenu.

**Husisha**
Taja vitu vinavyofanana ambayo umewahi kuviona sehemu nyingine.

**Tumia**
Taja vitu unavyoweza kuvipanga ukiwa nyumbani.

**Upimaji**
Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kupanga vitu kwa mfuatano unaofanana.

**Shughuli ya 5: Kuwawezesha watoto kucheza michezo ya kufananisha na kutofautisha vitu**
Mwalimu, waongoze watoto:
i. kutaja michezo mbalimbali wanayoifahamu;


Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 122 9/18/19 4:59 PM

ii. kubaini michezo ya kufananisha na kutofautisha vitu;
iii. kucheza michezo ya kufananisha vitu; na
iv. kucheza michezo ya kutofautisha vitu.

**Tafakari**

Taja mchezo wa kufananisha na kutofautisha vitu unaooufahamu

**Husisha**

Ulishawahi kucheza mchezo kama huu sehemu gani?

**Tumia**

Mchezo wa kufananisha na kuofautisha vitu utakusaidiaje wakati wa kuchagua vitu?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kufananisha vitu; na
ii. kutofautisha vitu.

**4.2.6.2 Kumwezesha mtoto kutambua dhana ya wakati**

Mwalimu, ili mtoto aweze kujenga dhana ya wakati ni vema akashirikishwa katika kufuata utaratibu wa shughuli za kila siku. Hivyo basi, katika eneo hili mwalimu utawaongoza watoto kuigiza matendo mbalimbali kulingana na nyakati, kutaja nyakati tofauti, kueleza shughuli zinazofanyika katika mazingira mbalimbali kwa nyakati tofauti, kutaja siku za juma na kutofautisha siku katika juma.

**Umuhimu wa mtoto kujenga dhana ya wakati**

Mwalimu, kumbuka kuwa dhana ya wakati ni muhimu sana kwa watoto kuweza kujua muda, mpangilio, utaratibu na kuwa makini katika shughuli zao za ujifunzaji wa kila siku. Watoto wakielewa vema dhana ya wakati itawawezesha kuwa wenye kujali, kuthamini na kutekeleza majukumu yao kulingana na muda uliopangwa.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Nyimbo, hadithi, michezo, maigizo, majadiliano ya vikundi na kazi mradi

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Vibao fumbo, saa, kanda za video, runinga, redio, simu, tarakilishi, picha, michoro, vitu halisi na kalenda



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 123 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kubainisha nyakati tofauti za siku**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja matendo mbalimbali wanayofanya kila siku shuleni na nyumbani;
ii. kutaja nyakati wanazofanya matendo hayo; na
iii. kuigiza matukio yanayoashiria nyakati.

**Tafakari**

Taja matendo unayofanya ukiwa shuleni.

**Husisha**

Taja matendo unayofanya ukiwa nyumbani.

**Tumia**

Je, wakati wa usiku huwa unafanya nini?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kutaja nyakati tofauti; na
ii. kuonesha matendo kulingana na nyakati.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kubainisha matendo yanayofanywa kulingana na wakati**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuigiza matendo kulingana na nyakati;
ii. kuimba nyimbo zinazoelezea matendo katika nyakati mbalimbali; na
iii. kucheza michezo inayohusisha matendo katika nyakati tofauti.

**Tafakari**

Ni matendo gani uliyoyaona kitabuni?

**Husisha**

Ni matendo gani ambayo unayafanya kila siku?

**Tumia**

Ukipewa nafasi uigize utaigiza matendo gani?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto anaweza kutenda kulingana na wakati.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kubainisha siku za juma**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja siku mbalimbali za juma wanazozijua;
ii. kutaja majina ya siku katika juma kwa mpangilio; na
iii. kucheza michezo ya kutaja siku za juma.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 124 9/18/19 4:59 PM

Wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni wimbo wa Siku za juma.

**Wimbo: Siku za juma**

*Jumatatu aaaaa, Jumanne aaaaaa, Jumatano aaaaaa, Alhamisi kuleeeeee, Ijumaa aaaaaa, Jumamosi k*uleeeee, *Jumapili aaaaaaa.*

Hatua za kufuata:

i. Waelekeze watoto wasimame.

ii. Anza kuimba wimbo wa siku za juma kwa kuonesha vitendo. Kwa mfano, unaposema ni muhimu mikono yako iwe inapishana kama ishara ya kukataa na unapoimba kuleeee unaruka juu kwa furaha huku mikono iko juu hewani.

iii. Waambie watoto waanze kuimba kwa kuonesha vitendo vya kukataa kama sio siku husika na kukubali kama ni siku husika. Mfano, kama siku si ya shule au ni ya shule.

iv. Hakikisha watoto wote wanaimba kama inavyotakiwa.

**Tafakari**

i. Je, umesikia siku gani zinatajwa katika wimbo uliouimba?

ii. Je, zimetajwa siku ngapi?

**Husisha**

i. Siku ya Jumamosi huwa unafanya kazi gani nyumbani?

ii. Jana ilikuwa siku gani?

iii. Ni siku zipi ambazo huwa huendi shule?

**Tumia**

Kwa nini ni muhimu kuzijua siku za juma?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutaja siku za juma kwa mpangilio.

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kutofautisha siku katika juma**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja siku za shule na zisizo za shule;

ii. kutaja siku za ibada; na

iii. kuonesha vitendo vinavyotofautisha siku za juma.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 125 9/18/19 4:59 PM

Wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni wimbo wa Siku za juma. Rejea katika Shughuli ya 3 katika Umahiri Mahususi huu.

**Tafakari**

i. Je, umesikia siku ngapi zinatajwa katika wimbo uliouimba?
ii. Zimetajwa siku ngapi?

**Husisha**

i. Je, siku ya Jumamosi huwa unafanya kazi gani nyumbani?
ii. Jana ilikuwa siku gani?
iii. Je, ni siku zipi ambazo huwa huendi shule?

**Tumia**

Kwa nini ni muhimu kuzijua siku katika juma?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. Kutofautisha siku za juma.
ii. Kufanya vitendo vinavyotofautisha siku za juma.

**4.2.6.3 Kumwezesha mtoto kumudu stadi za vipimo**

Mwalimu ili mtoto aweze kumudu stadi za vipimo ni vyema umwezeshe kujenga dhana ya vipimo. *Je, utatumia vifaa gani katika mazingira yako kumwezesha mtoto kumudu stadi za vipimo?* Bila shaka unaweza kutumia vitu mbalimbali vinavyosaidia kulinganisha vitu kwa sifa zake kama vile unene, wembamba, urefu, ufupi, wingi, uchache, wepesi na uzito.

**Umuhimu wa mtoto kumudu stadi za vipimo**

Stadi hizi zitamwezesha mtoto kufanya vitendo mbalimbali vinavyohusisha vipimo katika maisha yake ya kila siku.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Onesho mbinu, uchunguzi, kazi mradi, nyimbo, michezo na ziara za mafunzo

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Rula, kamba, mizani, futi kamba, picha, michoro, runinga, kanda za video, mchanga, maji, mawe madogo madogo, kopo



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 126 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kulinganisha vitu kutokana na sifa zake**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitu mbalimbali katika mazingira yao;
ii. kukusanya vitu vyenye sifa tofauti vilivyoko katika mazingira yanayomzunguka;
iii. kulinganisha vitu kwa wingi na uchache;
iv. kulinganisha vitu kwa unene na wembamba;
v. kulinganisha vitu kwa ukubwa na udogo;
vi. kulinganisha vitu kwa urefu na ufupi;
vii. kucheza michezo ya kulinganisha vitu kwa kuzingatia sifa anuai; na
viii. kupanga vitu kwenye makundi kulingana na sifa zake.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Nichambue

**Mchezo: Nichambue**

Vifaa: Makasha, vitu mbalimbali

Hatua za kufuata:

i. Andaa vitu vingi vinavyopatikana kwenye mazingira yako na uviweke kwenye makasha manne kwa idadi sawa katika kila kasha.
ii. Wapange watoto katika vikundi vinne (4), kisha gawa kasha moja katika kila kundi.
iii. Elekeza watoto katika kila kundi kuchambua vitu katika kasha kutokana na sifa zake na kuvipanga pembeni.
iv. Chagua mtoto mmoja kutoka katika kila kundi kuelezea sifa za vitu walivyochambua na kuvipanga.
v. Wasaidie watoto kufafanua vitu wakati wanaelezea endapo watashindwa.

**Tafakari**

i. Umepanga vitu katika makundi mangapi?
ii. Kwa nini umepanga vitu katika makundi hayo?

**Husisha**

i. Ni vitu gani ambavyo ulikuwa unavifahamu kabla?
ii. Ni vitu gani ulikuwa huvifahamu?

**Tumia**

Je, ni vizuri kupanga vitu vinavyofanana katika kundi moja? Kwa nini?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kulinganisha vitu kwa sifa zake.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 127 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kupima vitu mbalimbali**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kupima vitu mbalimbali;
ii. kupima vitu vyenye urefu tofauti;
iii. kupima vitu vyenye upana tofauti; na
iv. kupima vitu vyenye uzito tofauti

**Tafakari**

Taja vitu ulivyovipima ukiwa nje ya darasa

**Husisha**

Taja vitu vingine ambavyo umewahi kupima ukiwa nyumbani.

**Tumia**

Kipi kizito kati ya jiwe na kipande cha karatasi?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kupanga vitu katika makundi kulingana na sifa zake.

### 4.2.6.4 Kumwezesha mtoto kujenga dhana ya namba

Matumizi ya namba yanaonekana katika maisha ya kila siku ya binadamu. *Mwalimu, utawawezeshaje watoto kutambua na kutumia dhana ya namba katika maisha ya kila siku?* Pamoja na majibu uliyonayo unaweza kutumia vitu mbalimbali katika mazingira kujenga dhana ya namba.

**Umuhimu wa kumwezesha mtoto kujenga dhana ya namba**

Ni muhimu kumwezesha mtoto kujenga dhana ya namba kwa kuwa anatumia namba katika ujifunzaji na katika maisha yake ya kila siku.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

Nyimbo, kazi mradi, changanya kete, kisa mafunzo, hadithi, michezo, bungua bongo, maswali na majibu na majadiliano

**Zana za kufundishia na kujifunzia**

Kadi za namba, vihesabio, vibao fumbo, kanda za video, runinga, redio, simu, tarakilishi, chati za namba, kadi za namba



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 128 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 1: Kuwawezesha watoto kubainisha vitu vinavyosaidia kujenga dhana ya namba**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kukusanya vitu mbalimbali katika mazingira;
ii. kubainisha vitu vinavyojenga dhana ya namba;
iii. kutaja vitu vilivyomo katika mazingira yao kwa idadi;
iv. kufanya matendo kwa mpangilio/mfuatano ili kujenga dhana ya namba; na
v. kuchunguza picha zenye mpangilio/mfuatano unaofanana.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Nyoka na ngazi.

**Mchezo: Nyoka na ngazi**

Vifaa : Kadi, manila, kasha, ubao, vichezeo, kopo

Hatua za Kufuata:

i. Tumia kadi/manila/kasha/ubao kutengeneza mchezo wa Nyoka na Ngazi.
ii. Tengeneza dadu kwa kutumia kitu kidogo chenye umbo la mraba ili upate nyuso sita.
iii. Andaa vichezeo vyenye rangi tofauti mfano; visoda, vizibo vya chupa za plastiki na vikopo vya kuchezeshea dadu.
iv. Wagawe watoto katika vikundi vya watoto sita hadi nane.
v. Wape kila kundi dadu moja, kopo moja la kuchezea dadu na vichezeo vyenye rangi tofauti kulingana na idadi ya watoto katika kundi.
vi. Waoneshe watoto namna ya kucheza:
   - Wote waweke vichezeo vyao sehemu ya kuanzia. Kila mtoto afahamu rangi ya kichezeo chake.
   - Wambie wachukue dadu na kuiweka ndani ya kikopo.
   - Mtoto anayeanza anaweka dadu ndani ya kikopo na kutikisa, kisha anafunika na kuondoa kikopo. Uso wa dadu utaonesha idadi ya vidoti ambavyo mtoto atavihesabu. Kisha anachukua kihesabio chake na kuhesabu hatua sawa na idadi ya vidoti alivyoviona kwenye dadu na kukiweka juu ya namba inayolingana na vidoti hivyo.
   - Wataendelea kucheza kwa zamu mpaka mshindi atakapopatikana.
   - Kichezeo kikiwa kwenye ngazi mtoto anapandishwa juu, lakini kikiwa kwenye kichwa cha nyoka anamezwa na kushushwa chini mpaka kwenye mkia.
   - Mshindi ni yule atakayekuwa wa kwanza kufika kwenye namba ya mwisho (Sehemu ya kumalizia)

vii. Hakikisha kila mtoto anashiriki.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 129 9/18/19 4:59 PM

**Tafakari**

i. Umeona namba zipi wakati wa mchezo?
ii. Ulipomezwa na nyoka, ulijisikiaje? Kwa nini?
iii. Ulipopanda ngazi, ulijisikiaje? Kwa nini?
iv. Taja namba kubwa kuliko zote iliyopo kwenye dadu.

**Husisha**

i. Ni vitu gani vingine vinatumia namba?
ii. Ni sehemu gani nyingine tunaweza kuona namba?
iii. Ni wakati gani mwingine umewahi kuwa na furaha au huzuni?

**Tumia**

Kujua namba kutakusaidia nini?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kutaja vitu vinavyosaidia kujenga dhana ya namba;
ii. kutaja vitu katika mazingira kwa idadi; na
iii. kufanya matendo kwa mpangilio/mfuatano ili kujenga dhana ya namba.

**Shughuli ya 2: Kuwawezesha watoto kutamka namba 1 - 10**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutamka namba 1-10;
ii. kuimba wimbo wa namba 1 -10;
iii. kutamka namba 1-10 kwa mfuatano na kwa usahihi;
iv. kutamka namba kwa mfuatano unaofanana; na
v. kutaja namba inayokosekana katika mfuatano wa namba.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Mingo mingo

**Mchezo: Mingo mingo**

Hatua za kufuata:

i. Watoto wasimame sehemu ya wazi ya kuchezea.
ii. Waambie kuwa mchezo huu utahusu kuimba na kucheza kwa kutembeatembea.
iii. Waongoze kuimba wimbo wa "mingo mingo" na kucheza huku wakifuatisha kila unachotaja.
iv. Waongoze watoto kujitenga kwa idadi kulingana na namba inayotajwa bila kutawanyika mpaka utakapoanza kuimba tena mingo mingo kama ifuatavyo;



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 130 9/18/19 4:59 PM

| Mwalimu | Watoto |
|---|---|
| Mingo mingo eeeeeh × 4 | Mingo × 4 |
| Moja moja eeeeeh × 4 | Moja × 4 |
| Mbili mbili eeeeeh × 4 | Mbili × 4 |

vi. Endelea na wimbo mpaka utakapomaliza kutaja namba unazotaka watoto wajifunze.
vii. Chunguza watoto wanaoweza kujitenga katika idadi kulingana na namba iliyotajwa.

**Tafakari**

i. Umesikia namba zipi zinatajwa kwenye wimbo?
ii. Ni namba ipi ilikuwa rahisi kwako kuitambua na kuunda kikundi kwa urahisi?

**Husisha**

i. Ni vitu gani vingine umewahi kuvihesabu?
ii. Ni sehemu gani nyingine umeona namba zimeandikwa?

**Tumia**

i. Je, ni vizuri kujua kuhesabu namba? Kwa nini?
ii. Unaweza kuhesabu 1 - 10? Hesabu.

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutamka namba 1-10 kwa usahihi na kwa mfuatano.

**Shughuli ya 3: Kuwawezesha watoto kutenda vitendo rahisi vya kutamka namba 1-10**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitendo vinavyowezesha kutamka namba 1-10;
ii. kuonesha vitendo mbalimbali vya kutamka namba 1-10;
iii. kucheza michezo ya kutamka namba 1-10; na
iv. kutenda matendo ya kuhesabu kwa kurudi nyuma (10-1).

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni mchezo wa Mingo mingo. Rejea katika Shughuli ya 2 katika Umahiri Mahususi huu.

**Tafakari**

i. Umesikia namba zipi zinatajwa kwenye wimbo?
ii. Ni namba ipi ilikuwa rahisi kwako kuitambua na kuunda kikundi kwa urahisi?



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 131 9/18/19 4:59 PM

**Husisha**

i. Ni vitu gani vingine umewahi kuvihesabu?
ii. Ni sehemu gani nyingine umeona namba zimeandikwa?

**Tumia**

Je, ni vizuri kujua kuhesabu namba? Kwa nini?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kutenda vitendo vya kutamka namba 1 - 10.

**Shughuli ya 4: Kuwawezesha watoto kuhesabu namba 1-10 kwa kutumia vitu**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kukusanya vitu mbalimbali vitakavyotumika kuhesabu namba;
ii. kuhesabu vitu katika mazingira kuanzia kitu kimoja hadi vitu kumi;
iii. kutumia vihesabio kuhesabu namba; na
iv. kucheza michezo ya kuhesabu namba kwa kutumia vitu.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Shamba la wanyama

**Mchezo: Shamba la wanyama**

Vifaa: Kadi za picha

Hatua za kufuata:

i. Wagawe watoto katika timu mbili – Timu A na Timu B.
ii. Waambie watoto kwamba wanyama wametoroka katika shamba na wanatakiwa kumsaidia mtunza shamba kuwatafuta.
iii. Gawa eneo la kuchezea katika sehemu mbili, kila timu iwe na upande wake. Chora duara dogo upande wa mwisho wa kila timu (shamba la wanyama) likiwa na kadi za picha za wanyama .
iv. Timu zitakusanya wanyama waliotoroka shambani kwa kukimbia upande wa mwisho wa timu nyingine na kuchukua picha za wanyama na kuzileta katika duara lililo upande wao. Watafanya hivyo huku wakilinda wanyama wao wasichukuliwe na timu nyingine.
v. Mtoto mmoja anaruhusiwa kuokota kadi moja kwa wakati mmoja.
vi. Timu zote zitakuwa zinakimbia na kukusanya wanyama kwa wakati mmoja.
vii. Watafanya hivi mara nyingi hadi uone kwamba inatosha na kusimamisha mchezo.
viii. Timu zitahesabu na kusema ni wanyama wangapi wamekusanya.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 132 9/18/19 4:59 PM

**Tafakari**

i. Timu yako imekusanya wanyama wangapi?
ii. Mlifanya nini kukusanya wanyama wengi katika mchezo?
iii. Kwa nini mmeshindwa kukusanya wanyama wengi?

**Husisha**

i. Umeshawahi kuhesabu wanyama sehemu yoyote? Walikuwa wangapi?
ii. Ni vitu gani vingine huwa unavihesabu?

**Tumia**

Utafanya nini ili uweze kuhesabu kwa usahihi?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kuhesabu vitu kuanzia kitu kimoja hadi vitu kumi(1-10).

**Shughuli ya 5: Kuwawezesha watoto kuoanisha idadi ya vitu na namba.**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kukusanya vitu katika mazingira;
ii. kuweka vitu walivyokusanya katika makundi kwa idadi isiyozidi 10;
iii. kuoanisha idadi ya vitu katika makundi na namba; na
iv. kutenda vitendo vya kuoanisha vitu na namba.

Michezo inayopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Makofi ya namba
b. Wimbo wa Naweza kuhesabu namba
c. Uza na nunua

**a. Mchezo: Makofi ya namba**

Waelekeze watoto wacheze mchezo wa makofi ya namba kwa kutamka namba moja hadi tano (1-5)

Hatua za kufuata:

i. Wagawe watoto katika timu mbili na kila timu iwe na pande mbili.
ii. Upande mmoja wa timu utamke namba na upande wa pili upige makofi kulingana na idadi ya namba iliyotamkwa kwa kubadilishana vitendo vinavyofanyika.
iii. Timu itakayoweza kuhusisha namba zote itakuwa imeshinda.
iv. Pitia na hakikisha kila kundi au timu inatenda kulingana na maelekezo.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 133 9/18/19 4:59 PM

**b. Wimbo: Naweza kuhesabu namba**

*Naweza kuhesabu namba, moja mpaka kumi,*
*Naanza kuhesabu namba, moja, mbili, tatu,*
*Nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi,*

**Tafakari**

i. Umetaja namba zipi katika wimbo uliouimba/mchezo ulioucheza?
ii. Kati ya namba zilizotajwa, ipi ni ndogo? Ipi ni kubwa?

**Husisha**

Una wimbo au mchezo mwingine unaotusaidia kuhesabu namba? Imba nasi tuimbe.

**Tumia**

Unafikiri ni vizuri kuweza kutaja namba 1-10? Kwa nini?

**c. Mchezo: Uza na nunua**

Vifaa: Domino, vihesabio

Hatua za kufuata:

i. Wagawe watoto katika vikundi vya watoto kati ya 8 – 10 ili kupata uwiano wa makundi mawili ya kushindana.
ii. Gawa domino tano zenye vidoti kuanzia moja mpaka tano na vihesabio vitano kwa kila kundi.
iii. Eleza na onesha kwamba kila kundi litauza na kununua domino kwa zamu.
iv. Kundi litauza domino linayotaka kwa kuionesha kwa kundi lingine ambalo litalinganisha idadi ya vihesabio na idadi ya vidoti viliyomo kwenye domino iliyooneshwa.
v. Kikundi kitahesabu vihesabio hivyo na kutaja ni namba ngapi. Wakipata wanakuwa wamefanikiwa kununua domino hiyo.
vi. Mchezo utaendelea hadi domino zote zitakapokuwa zimetumika na kikundi kitakachofanikiwa kununua domino nyingi kitakuwa kimeshinda.

**Tafakari**

i. Kikundi chenu kimefanikiwa kununua domino ngapi?
ii. Mliwezaje kununua domino hizo?
iii. Kwa nini hamkuweza kununua domino nyingi zaidi ?

**Husisha**

i. Umeshawahi kulinganisha idadi ya vitu? Ilikuwaje?
ii. Ni vitu gani vingine unaweza kulinganisha idadi yake?

**Tumia**

Utaweza kulinganisha namba na idadi ya vitu? Kwa namna gani?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kuoanisha idadi ya vitu na namba.

**Shughuli ya 6: Kuwawezesha watoto kutenda vitendo vya kuongeza na kupunguza vitu**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kukusanya vitu mbalimbali katika mazingira;
ii. kutenda matendo ya kuongeza kwa kutumia vitu;
iii. kucheza michezo mbalimbali inayojenga dhana ya kuongeza;
iv. kufanya matendo ya kupunguza kwa kutumia vitu; na
v. kucheza michezo mbalimbali inayojenga dhana ya kupunguza.

Nyimbo zinazopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni:

a. Wimbo wa sabina wa kuongeza
b. Wimbo wa vidole kumi punguza

**a. Wimbo : Wimbo wa Sabina wa kuongeza**

| **Mwalimu** | **Watoto** |
|---|---|
| *Saabina* | *Sabina* |
| *Sabina mama* | *Sabina* |
| *Njoo tusome/tucheze* | *Sabina* |
| *Michezo ya kwetu* | *Sabina* |
| *Moja na moja ni ngapi Sabina?* | *Moja na moja ni mbili Mwalimu* |
| *Mbili na moja ni ngapi Sabina* | *Mbili na moja ni tatu Mwalimu* |
| *Saabina* | *Sabina* |
| *Cheza kidogo* | *Sabinaaaa sabinaaa* |



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 135 9/18/19 4:59 PM

**Tafakari**

i. Ulitaja namba zipi wakati wa kuimba?
ii. Ulikuwa unafanya nini wakati wa kuimba?

**Husisha**

i. Umewahi kuhesabu namba mpaka ngapi?
ii. Je, una wimbo mwingine wa namba unaoufahamu? kama ndiyo tuimbie wimbo huo.

**Tumia**

Taja namba nyingine unazozifahamu.

**b. Wimbo : Vidole kumi punguza**

*Vidole kumi punguza kimoja utapata vidole vingapi?*
*Utapata vidole tisa, vidole tisa mkononi*
*Vidole tisa punguza kimoja utapata vidole vingapi?*
*Utapata vidole nane, vidole nane mkononi*
*Vidole nane punguza kimoja utapata vidole vingapi?*
*Utapata vidole saba, vidole saba mkononi*
*Kidole kimoja punguza kimoja utapata vidole vingapi?*
*Hakuna kidole, hakuna kidole, hakuna kidole mkononi*

**Tafakari**

i. Umetaja namba zipi katika wimbo uliouimba?
ii. Namba ipi ni kubwa kati ya saba na tano?

**Husisha**

Wimbo gani mwingine wa kupunguza namba unaufahamu? Tuimbe sote.

**Tumia**

Unafikiri ukipewa machungwa 5, kisha ukapunguzia rafiki yako machungwa 2, utabakiwa na machungwa mangapi?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza kufanya matendo ya kuongeza na kupunguza vitu.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 136 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 7: Kuwawezesha watoto kubainisha maumbo ya namba kwa kutumia vitu mbalimbali**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kutaja vitu vinavyofanana na maumbo ya namba;
ii. kucheza michezo ya kuoanisha maumbo ya namba na vitu; na
iii. kuoanisha maumbo ya namba na vitu.

Wimbo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni wimbo wa Andika kama.

**Wimbo: Andika kama**

*Andika moja kama fimbo iliyosimama*
*Andika mbili kama bata anaogelea*
*Andika tatu kama paka amekaa kitako*
*Andika nne kama kiti cha mwalimu wetu*
*Andika tano kama boga na kikonyo chake*
*Andika sita kama kata ya kuteka maji*
*Andika saba kama bendera inayopepea*
*Andika nane kama vyungu vilivyobebana*
*Andika tisa kama rungu lililoegeshwa*

**Tafakari**

i. Namba zipi ulizitaja wakati wa kuimba wimbo?
ii. Namba zipi zilikuwa rahisi/ngumu kwako kuzitaja?

**Husisha**

i. Namba zipi nyingine unazifahamu?
ii. Namba 1- 9 imefanana na umbo gani unalolifahamu?

**Tumia**

Maumbo gani mengine utayafananisha na namba 1 - 9

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kubaini kama kila mtoto ameweza:

i. kubainisha maumbo ya namba; na
ii. kuoanisha maumbo ya namba na vitu.

**Shughuli ya 8: Kuwawezesha watoto kuumba/kuunda maumbo ya namba**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kubaini makunzi watakayotumia kuumba/kuunda maumbo mbalimbali ya namba;
ii. kuumba/kuunda maumbo ya namba kwa kufuata hatua; na
iii. kupaka rangi maumbo ya namba waliyoyaumba/waliyoyaunda.

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni Ipe namba.

**Mchezo: Ipe namba**

Hatua za kufuata:

i. Waoneshe watoto namba tofauti tofauti.
ii. Anza kwa kuwaonesha watoto namna unavyounda namba kwa kutumia mwili wako au vitu vyovyote katika mazingira.
iii. Wagawe watoto katika vikundi kulingana na namba ulizoandika.
iv. Taja jina la namba, kisha kila kikundi husika kiunde umbo la namba hiyo kwa kutumia miili yao au vifaa ulivyoviandaa.
v. Hakikisha watoto wote wanashiriki na wanaunda umbo la namba kwa usahihi.
vi. Hakikisha kila kikundi kinaunda maumbo mbalimbali ya namba.

**Tafakari**

i. Je, ni umbo gani la namba lilikuwa rahisi kuliunda?
ii. Je, ni namba gani ilikuwa ngumu kuandika?

**Husisha**

Je, ni vitu gani vingine vinafanana na namba mlizoandika/mlizoumba?

**Tumia**

Je, unaweza kuunda namba kwa kutumia vitu gani vingine? Ni vitu gani hivyo?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kuumba/kuunda maumbo ya namba.

**Shughuli ya 9: Kuwawezesha watoto kufuatisha maumbo ya namba 1-9**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kufuatisha maumbo ya namba;
ii. kupaka rangi maumbo ya namba; na
iii. kuchapa maumbo mbalimbali.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 138 9/18/19 4:59 PM

Mchezo unaopendekezwa kufundishia na kujifunzia katika shughuli hii ni mchezo Ipe namba. Rejea katika shughuli ya 8 katika umahiri mahususi huu.

**Tafakari**

i. Je, ni umbo gani la namba lilikuwa rahisi kuliunda?
ii. Je, ni namba gani ilikuwa ngumu kuandika?

**Husisha**

Je, ni vitu gani vingine vinafanana na namba mliziandika/mlizoumba?

**Tumia**

Je, unaweza kuunda namba kwa kutumia vitu gani vingine? Ni vitu gani hivyo

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza:

i. kufuatisha maumbo ya namba yaliyoandaliwa; na
ii. kupaka rangi maumbo ya namba kwa usahihi.

**Shughuli ya 10: Kuwawezesha watoto kuandika namba 1- 9 hewani , mchangani, kwenye kibao na daftari**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuandika namba hewani kwa kufuata hatua;
ii. kuandika namba kwenye mchanga kwa kufuata hatua;
iii. kuandika namba kwenye vibao kwa kufuata hatua; na
iv. kuandika namba kwenye karatasi kwa kufuata hatua.

**Tafakari**

Taja namba uliyoandika mchangani

**Husisha**

Taja namba zingine ambazo umewahi kuandika kwenye daftari.

**Tumia**

Utamsaidiaje rafiki yako ambaye hawezi kuandika namba mchangani?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kuandika namba 1-9 kwa kufuata hatua.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 139 9/18/19 4:59 PM

**Shughuli ya 11: Kuwawezesha watoto kutenda vitendo vinavyojenga dhana ya sifuri**

Mwalimu, waongoze watoto:

i. kuweka idadi tofauti ya vitu, mfano, vijiti, mawe, visoda au pipi kwenye visahani tofauti. Kati ya hivyo pawepo na kisahani kisichokuwa na kitu. Kutaja idadi ya vitu katika kila kisahani. Kisahani kisichokuwa na kitu ndio sifuri yaani hakuna kitu;

ii. kutenda vitendo vingine vya kujenga dhana ya sifuri kwa kutumia zana tofauti; na

iii. kutumia michezo/nyimbo/maigizo mbalimbali kujenga dhana ya sifuri.

**Tafakari**

Je ulipoondoa chupa zote ulibakiwa na chupa ngapi?

**Husisha**

Je umewahi kuwapa rafiki zako vitu vyako vyote? Je ulibakiwa na nini?

**Tumia**

Baba akikupa madaftari matano kisha ukigawa yote utabakiwa na madaftari mangapi?

**Upimaji**

Tumia zana za upimaji kuona kama kila mtoto ameweza kutenda vitendo vinavyojenga dhana ya sifuri.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 140 9/18/19 4:59 PM

## REJEA

Aga Khan Foundation. (2014). *Stregthening education system in East Africa*: Bridging Curriculum (Draft).

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2013a). *Mwongozo wa kuandaa na kutumia Vifaa vya michezo kwa watoto wadogo*: *Programu ya Mafunzo kazini kwa walezi wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na walimu wa Elimu ya Awali.* Dar es Salaam: WyEST.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2013b). *Mwongozo wa utambuzi wa mapema wa watoto wenye mahitaji maalum na afua stahiki umri 0 – 8*. *Programu ya mafunzo kazini kwa walezi wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na walimu wa Elimu ya Awali*. Dar es Salaam: WyEST.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2014). *Sera ya elimu na mafunzo (2014).* Dar es Salaam: WyEST.

Madrasa Early Childhood Program. (2014). *Uongozi na usimamizi wa darasa la maandalizi*: Zanzibar: Draft

Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania. (TECDEN). (2013), *Kiunzi cha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto Tanzania.* Dar es Salaam: TECDEN

Naudeau, S., Kataoka, N., Valerio, A., Neuman, M. J. & Elder, L. K. (2010). *Investing in young children*: *An early childhood development guide for policy dialogue and project preparation.* Washington: The World Bank.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2003). *Mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti.* Dar es Salaam: Inter Press of Tanzania Limited.

Tassoni, P., Beith, K., Eldridge, H. & Gough, A. (2002). *Diploma in child care and education*. Oxford: Heineman Educational Publishers.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. (2013). *Ujuzi wa malezi changamshi kwa watoto wadogo*. Dar es Salaam: WyEST.



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 141 9/18/19 4:59 PM

# Viambatisho

## Viambatisho A

### Azimio la Kazi

**Jina la shule**.................................................................... **Jina la mwalimu** ..................................................

**Darasa** ................................ **Muhula** ................................................ **Mwaka** ..................................................

**Umahiri mkuu**.........................................................................................................................................................

| Umahiri mahususi | Shughuli kuu za kutendwa na mtoto | Shughuli ndogo za kutendwa na mtoto | Mwezi | Wiki | Idadi ya vipindi | Zana za kufundishia na kujifunzia | Zana za upimaji | Rejea | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 142
9/18/19 4:59 PM

# Kiambatisho B

## Andalio Ia Somo

Jina la shule.................................... Jina la mwalimu: ..................................

Darasa: ........................................ Tarehe :.................................................

Kipindi cha: ................................. Muda: ...................................................

| ldadi ya watoto | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Walioandikishwa | | | Waliohudhuria | | |
| Wasichana | Wavulana | Jumla | Wasichana | Wavulana | Jumla |
| | | | | | |

Umahiri Mkuu: ..........................................................................................

Umahiri Mahususi: ....................................................................................

Shughuli Kuu: ...........................................................................................

Shughuli Ndogo : .......................................................................................

Vifaa/Zana : ..........................................................................................

Rejea : ......................................................................................................

Shughuli za kutendwa na mwalimu

i. : ........................................................................................................

ii. : ........................................................................................................

iii. : ........................................................................................................

iv. : ........................................................................................................

v. : ........................................................................................................

Shughuli za kutendwa na mtoto

i. : ........................................................................................................

ii. : ........................................................................................................

iii. : ........................................................................................................

iv. : ........................................................................................................

v. : ........................................................................................................



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 143 9/18/19 4:59 PM

Viashiria pendekezwa vya utendaji

i. : ............................................................................................................
ii. : ............................................................................................................
iii. : ............................................................................................................
iv. : ............................................................................................................
v. : ............................................................................................................

Tafakuri : ..........................................................................................................

Tathmini ya ujifunzaji na ufundishaji : ............................................................

Maoni: ............................................................................................................



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 144 9/18/19 4:59 PM

# Kiambatisho C

# Orodha hakiki

Jina la mwalimu: ................................... Darasa: .......................................

Tarehe :.................................................... Muda: .........................................

Umahiri Mkuu : Kuhusiana

Umahiri Mahususi : Kujali

Shughuli Kuu : Kutambulishana

Shughuli ndogo za kutendwa na mtoto

i. Kujitambulisha majina kamili na jinsi zao.
ii. Kutambulisha majina ya wazazi/walezi na watu wengine anaoishi nao.
iii. Kueleza mahali wanapoishi.
iv. Kutaja jina la shule anayosoma.
v. Kuwatambulisha watoto wengine kwa majina yao.
vi. Kutaja majina ya watu wengine yanayoonesha uhusiano.

| Jina la mtoto | **Viashiria pendekezwa vya upimaji** | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kutaja jina lake | | | | Kutaja mahali anapoishi | | | | Kutaja jina la shule | | | | Kutambulisha wengine | | | |
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 |
| Esta | | ✓ | | | ✓ | | | | | | ✓ | | | | ✓ | |
| Jamila | | | ✓ | | ✓ | | | | ✓ | | | | ✓ | | | |
| Maiko | | ✓ | | | | ✓ | | | | ✓ | | | | | | ✓ |
| Jafari | | | ✓ | | | | | ✓ | | ✓ | | | | | ✓ | |

**Mwalimu unaweza kutumia alama ya vema (✓) kuonesha kiwango alichofikia mtoto** katika kutenda shughuli husika kwa kuzingatia viwango vifuatavyo:

1 = Hafifu 2 = Wastani 3 = Vizuri 4 = Vizuri sana

# Kiambatisho D

# Hojaji

1. Jina la mzazi/mlezi ......................................................................................
2. Uhusiano na mtoto ................................ Namba ya simu ...........................
3. Mtoto wako anaitwa nani?
4. Ana umri wa miaka mingapi?
5. Ni mtoto wa ngapi kuzaliwa?
6. Je, mtoto wako anaendelea kuhudhuria kliniki?
7. Je, mtoto wako ana tatizo lolote la kiafya? Kama ndiyo, ni tatizo gani? Hatua gani zilizochukuliwa ?
8. Tatizo linapotokea, huduma gani ya kwanza huwa unampatia?
9. Je, mnaishi wapi?
10. Je, ni nani atakayekuwa anamleta mtoto shule au kumfuata wakati wa kurudi nyumbani?

# Kiambatisho E

## Fomu ya maendeleo ya watoto wa elimu ya awali

Jina la shule ........................................ Jina la Mwalimu .................................
Mwaka ................................................ Mwezi ................................................
Muhula .............................. Umri wa watoto .............................................

**Sehemu A: Maendeleo katika kujenga umahiri**

Mwalimu unaweza kutumia alama ya vema (✓) kuonesha kiwango alichofikia mtoto katika kutenda shughuli husika kwa kuzingatia viwango vifuatavyo:

**Umahiri wa Kuhusiana**

| Jina la mtoto | Jinsi | **Viwango vya utendaji katika umahiri mahususi** | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kujali | | | | Kuheshimiana | | | | Kujitawala | | | |
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 |
| Esta | | | | | | | | | | | | | |
| Jamila | | | | | | | | | | | | | |
| Maiko | | | | | | | | | | | | | |
| Jafari | | | | | | | | | | | | | |

**Umahiri wa Kuwasiliana**

| Jina la mtoto | Jinsi | **Viwango vya utendaji katika umahiri mahususi** | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kusikiliza | | | | Kuzungumza | | | | Kumudu stadi za awali za kusoma | | | | Kumudu stadi za awali za kuandika | | | |
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 |
| Esta | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Jamila | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Maiko | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Jafari | | | | | | | | | | | | | | | | | |

## Umahiri wa Kutunza Afya

| Jina la mtoto | Jinsi | Viwango vya utendaji katika umahiri mahususi | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubainisha sehemu za nje za mwili na kazi zake | | | | Kutunza mwili | | | | Kutunza mavazi | | | | Kutunza vyombo vya chakula | | | | Kubainisha chakula bora | | | | Kubainisha magonjwa | | | |
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 |
| Esta | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Jamila | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Maiko | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Jafari | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |

## Umahiri wa Kutunza Mazingira

| Jina la mtoto | Jinsi | Viwango vya utendaji katika Umahiri mahususi | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubainisha vitu vilivyomo katika mazingira | | | | Kusafisha mazingira | | | | Kuchukua tahadhari | | | |
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 |
| Esta | | | | | | | | | | | | | |
| Jamila | | | | | | | | | | | | | |
| Maiko | | | | | | | | | | | | | |
| Jafari | | | | | | | | | | | | | |

## Umahiri wa Kumudu Stadi za Kisanii

| Jina la mtoto | Jinsi | Viwango vya utendaji katika Umahiri mahususi | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kumudu sanaa za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mikono | | | | Kumudu stadi za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mwili | | | | Kumudu stadi za ubunifu wa sauti | | | |
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 |
| Esta | | | | | | | | | | | | | |
| Jamila | | | | | | | | | | | | | |
| Maiko | | | | | | | | | | | | | |
| Jafari | | | | | | | | | | | | | |



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 148 9/18/19 4:59 PM

## Umahiri wa Kutumia Dhana za Kihisabati

| Jina la mtoto | Jinsi | Viwango vya utendaji katika Umahiri mahususi | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kutumia mazingira kujenga dhana za kihisabati | | | | Kujenga dhana ya wakati | | | | Kumudu stadi za vipimo | | | | Kujenga dhana ya namba | | | |
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 |
| Esta | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Jamila | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Maiko | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Jafari | | | | | | | | | | | | | | | | | |

## Sehemu B: Maendeleo ya mtoto kitabia na kiafya

| Jina la mtoto | Jinsi | Viwango vya utendaji | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Maendeleo ya mtoto kitabia | | | | Maendeleo ya mtoto kiafya | | | |
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 |
| Esta | | | | | | | | | |
| Jamila | | | | | | | | | |
| Maiko | | | | | | | | | |
| Jafari | | | | | | | | | |

Maoni ya Mwalimu.........................................................................................................

Mwalimu unaweza kutumia alama ya (✓) kuonesha kiwango alichofikia mtoto katika kutenda shughuli husika. Zingatia viwango vifuatavyo:

1= Hafifu 2= Wastani 3= Vizuri 4= Vizuri sana



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 149 9/18/19 4:59 PM

# Kiambatisho F

## Fomu ya taarifa ya maendeleo ya mtoto wa Elimu ya Awali

Jina la mtoto:.................................. Jina la shule:................................

Umri wa mtoto:............................... Jinsi : ...........................................

| I | Maendeleo katika kujenga umahiri | Kiwango cha mafanikio | Maoni |
|---|---|---|---|
| | Kuhusiana | | |
| | Kuwasiliana | | |
| | Kutunza Afya | | |
| | Kutunza Mazingira | | |
| | Kutumia dhana za Kihisabati | | |
| II | Maendeleo ya Tabia | | |
| III | Maendeleo ya Afya | | |

Mwalimu unaweza kutumia yafuatayo kuonesha kiwango alichofika mtoto

katika kujifunza: Vizuri sana, Vizuri, Wastani, Hafifu.

Maoni ya Mwalimu :..........................................................................................

Jina la Mwalimu Mkuu:..........................Sahihi:..................Tarehe:.................



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 150 9/18/19 4:59 PM

# Kiambatisho G

## Utaratibu wa siku katika Shule ya Awali

| SIKU | 2:00 2:10 | 2:10 2:15 | 2:15 2:25 | 2:25 2:45 | 2:45 3:05 | 3:05 3:25 | 3:25 4:00 | 4:00 4:20 | 4:20 4:40 | 4:40 5:20 | 5:20 5:30 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumatatu** | Michezo | Ukaguzi wa Afya | Mduara wa Asubuhi | Kuwasi liana | Kumudu Stadi za Kisanii | Kuhu siana | Mapumziko | Kutunza Afya | Kuwasi liana | Kona za Ujifunzaji | Mduara wa Kuagana |
| **Jumanne** | Michezo | Ukaguzi wa Afya | Mduara wa Asubuhi | Kutunza Afya | Kutunza Mazingira | Kumudu Stadi za Kisanii | Mapumziko | Kuwasi liana | Kutumia Dhana za Kihisabati | Kona za Ujifunzaji | Mduara wa Kuagana |
| **Jumatano** | Michezo | Ukaguzi wa Afya | Mduara wa Asubuhi | Kumudu Stadi za Kisanii | Kuwasi liana | Kutunza Afya | Mapumziko | Kutumia Dhana za Kihisabati | Kutunza Afya | Kona za Ujifunzaji | Mduara wa Kuagana |
| **Alhamisi** | Michezo | Ukaguzi wa Afya | Mduara wa Asubuhi | Kutumia Dhana za Kihisabati | Kutunza Afya | Kuwasi liana | Mapumziko | Kumudu Stadi za Kisanii | Kutunza Mazingira | Kona za Ujifunzaji | Mduara wa Kuagana |
| **Ijumaa** | Michezo | Ukaguzi wa Afya | Mduara wa Asubuhi | Kuhu siana | Kutumia Dhana za Kihisabati | Kumudu Stadi za Kisanii | Mapumziko | Kutunza Afya | Kuwasi liana | Kona za Ujifunzaji | Mduara wa Kuagana |



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 151 9/18/19 4:59 PM

# Kiambatisho H

**Fomu ya viasharia vya utayari wa mtoto wa miaka 3 na 4 kujiunga na darasa la Elimu ya Awali**

Jina la mtoto………………...............……… Umri……….………Jinsi……………

| Vigezo vya Kuzingatia | Anamudu | Hajamudu |
|---|---|---|
| 1. Uwezo wa kujitegemea | | |
| Kuvaa mwenyewe | | |
| Kwenda chooni | | |
| Kutoa kamasi | | |
| Kula/kunywa mwenyewe | | |
| Kucheza michezo rahisi | | |
| 2. Uwezo wa kujieleza | | |
| Kusalimia, kutaja jina lake, jina la mzazi/mlezi au ndugu zake katika familia | | |
| Kueleza anakoishi | | |
| Kueleza hali ya afya yake | | |
| Kueleza shida aliyo nayo | | |
| Kuomba kitu | | |
| 3. Uwezo wa kufuata maelekezo rahisi | | |
| Simama/kaa/njoo/nenda | | |
| 4. Hamasa ya mtoto mwenyewe | | |
| Jinsi anavyojibu maswali | | |
| Kuonesha furaha/uchangamfu | | |
| Kushirikiana na wenzake | | |
| Kucheza na wenzake | | |

Maoni ya mwalimu…………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………………………….



Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 152 9/18/19 4:59 PM

Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 153 9/18/19 4:59 PM

ISBN 978-9976-61-906-5

Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 154 9/18/19 4:59 PM

# Mwongozo wa Mwalimu wa Kufundishia

## Elimu ya Awali

Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwongozo wa mwl. kufundishia EA.indd 155 9/18/19 4:59 PM